**30 AGOSTI, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Nne – Tarehe 30 Agosti, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

Maelezo ya Waziri Mkuu kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Ulinzi wa Mtoto wa Mwaka 2024 *[The Child Protection Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024]*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Ustawi na Maendeleo ya Jamii. Kwa niaba yake. *(Makofi)*

**MHE. TECLA M. UNGELE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Ulinzi wa Mtoto wa mwaka 2024 *[The Child Protection Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024]*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa niaba ya Mwenyekiti, Mheshimiwa Ungele.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Maswali. Tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Namwita Mheshimiwa Felista Deogratius Njau, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 50

### Ujenzi wa Barabara ya Kisomboko hadi Zahanati ya Mawela – Moshi

**MHE. FELISTA D. NJAU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya kutoka Kisomboko kwenda Zahanati ya Mawela – Moshi Vijijini kwa kiwango cha changarawe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa niaba yake, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Katimba.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Kisomboko – Mawela Zahanati inakadiriwa kuwa na kilomita tatu, barabara hiyo ambayo haijasajiliwa katika mtandao wa barabara zinazohudumiwa na *TARURA* ni mpya. Barabara hii ni moja kati ya barabara zinazoelekea katika Zahanati ya Mawela ikiwa ni pamoja na Barabara za Uru Seminari – Kifumbuni ambayo ni kilomita 4.5 na Molangi – *Kisarika High School – AMCOS* kilomita tatu ambayo kwa mwaka 2024/2025 itafanyiwa matengenezo ya kawaida kwa gharama ya shilingi milioni 900.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2024/2025 Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kushirikiana na wananchi wa maeneo husika itahakikisha Barabara ya Kisomboko – Zahanati ya Mawela inafanyiwa matengenezo ili iweze kupitika na kutoa huduma kama inavyokusudiwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deogratius Njau swali la nyongeza.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nitauliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, mwezi wa Pili nilisimama kwenye Bunge lako Tukufu nikauliza juu ya barabara inayotokea Mawela kuelekea Kituo cha Walemavu mpaka Kituo cha Afya cha Uru Kusini nikajibiwa kwamba barabara hiyo itatengewa bajeti 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kwenye takwimu za Mheshimiwa Waziri, barabara hiyo haipo. Ni lini sasa barabara hiyo itajengwa ili kunusuru maisha ya wananchi wa Moshi Vijijini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Wakati *TARURA* wanaingiza barabara nyingi kwenye mfumo, barabara nyingi za Moshi Vijijini ziliachwa nje ya mfumo kwa kusahaulika. Ni lini sasa Serikali itaainisha barabara hiyo na kuzitengea bajeti ili ziweze kutengenezwa? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kupaza sauti kuhakikisha kwamba wananchi wanapata barabara nzuri. Kuhusu swali lake la kwanza, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mwaka huu wa fedha 2024/2025 Barabara hii ya Mawela Kanisani kwenda Zahanati ya Mawela itafanyiwa matengenezo ili iweze kupitika na iweze kutoa huduma iliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili ambalo amezungumza kuhusiana na kuweka katika mtandao, kuingiza katika mfumo au mtandao wa barabara zinazosimamiwa na *TARURA*, barabara katika jimbo alilolitaja, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba utaratibu wa kusajili barabara hizi za Wilaya kuziingiza katika mtandao unaosimamiwa na kuhudumiwa na *TARURA,* mchakato huo unaanza kwenye Halmashauri kupeleka katika *Road Board* (Bodi ya Barabara) ya Mkoa na baada ya hapo inawasilishwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi ili waweze kupitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuhakikishie tayari vikao hivyo vimeshaketi, Tarehe 13/11/2023 Kikao cha Bodi ya Barabara cha Mkoa kilikaa na kupitisha barabara zenye urefu wa kilomita 413. Haya ni maombi kabisa kwa ajili ya kupitishwa ili yaweze kuingia katika mtandao utakaohudumiwa na *TARURA*. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika swali lake alilouliza, Serikali inachukua hatua. Barabara hizi tayari zimeshapitishwa katika utaratibu, bado tu kuthibitishwa ili zianze kuhudumiwa na *TARURA*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi ni Diwani katika Halmashauri ya Moshi *DC*. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake, lakini ni lini hasa barabara hiyo ya kutoka Mawela kwenda Shule ya Okaseni

kupitia kambini ikiunganisha na hicho Kituo cha Walemavu pamoja na hiyo *dispensary* nayo itatajwa katika barabara ambazo zimewekewa bajeti? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake lenye tija kubwa sana kwa wananchi wa *Moshi DC*. Kama nilivyotangulia kujibu ni kwamba, Serikali inafanya jitihada na tayari imeshafanya mchakato wa kuingiza na kutambua barabara katika Halmashauri ya Moshi, katika Wilaya ya *Moshi DC* ambazo zitaingia na kuanza kuhudumiwa na *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejibu kwamba, katika mwaka huu wa fedha barabara hii ya Mawela Kanisani kwenda zahanati ya Mawela zitafanyiwa ukarabati ili ziweze kuwahudumia wananchi. Kwa hiyo, naomba nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, mchakato upo, yaani unaendelea. Barabara hii itaingizwa rasmi katika barabara zinazotambulika na kuhudumiwa na *TARURA,* lakini katika mwaka wa fedha huu tayari kuna mchakato wa kuhakikisha kwamba hii barabara inakarabatiwa na inaweza kuhudumia watu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, imeeleweka. Mheshimiwa Jackson Kiswaga, swali la nyongeza.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Barabara ya kutoka Magunga, Kata ya Maboga, kwenda Wasa imeharibika sana.

Je, ni lini sasa Serikali itaitengeneza hiyo barabara kwa kiwango cha changarawe? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu kwa kifupi, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni

dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba inahudumia barabara, hasa hizi za *TARURA* ambazo zinabeba umuhimu mkubwa sana kuwahudumia wananchi kiuchumi na kijamii. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kama vile ambavyo Serikali tayari imeanza kuhudumia barabara hizi, barabara yake hii na yenyewe itahudumiwa ili iweze kuwa katika hadhi nzuri na iweze kuwahudumia wananchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selemani Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Barabara ya Ikola kwenda Kata ya Isengule, Vijiji vya Isengule, Shukura na Kasangatongwe ni barabara ambayo imeharibika kwa kiwango kikubwa sana baada ya mvua zilizonyesha na kuwafanya wanafunzi kushindwa kusoma kwa sababu ya kuvunjika kwa daraja. Ni lini Serikali itaenda kuikarabati hiyo barabara ili wananchi waweze kupata huduma? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa barabara hizi, hasa kiuchumi na kijamii; na kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii na daraja hili ambalo lipo linawezesha watoto kwenda shule, basi naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ipo kazini na itahakikisha inafika na inaihudumia barabara hii ya Ikola – Isengule na hasa katika eneo hili la daraja ambalo linawasaidia wanafunzi kuweza kufika katika shule.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa vipande vya barabara kutoka Sangisi – Akeli hadi Ndoobo na Sangisi – Chuo cha Jeshi Duluti hadi Nelson Mandela? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikikarabati na kujenga barabara zetu hizi za *TARURA* kwa awamu. Mheshimiwa Mbunge katika jimbo lake barabara hizi za Wilaya ambazo zinasimamiwa na *TARURA* zimekuwa zikiendelea kutengewa fedha kila mwaka wa bajeti. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itahakikisha barabara hizi alizozitaja katika jimbo lake zinaweza kukarabatiwa na kujengwa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea. Swali linalofuata, namwita Mheshimiwa Janeth Maurice Massaburi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 51

**Kukamilisha Ujenzi na Miundombinu ya Kituo cha Mabasi cha Magufuli, Mbezi**

**MHE. JANETH M. MASSABURI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha kwa asilimia 100 ujenzi na miundombinu ya Kituo Kikuu cha Mabasi cha Magufuli, Mbezi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Mradi wa Kituo cha Mabasi cha Magufuli ulianza Oktoba, 2017 na kuzinduliwa Septemba, 2019. Mradi huu ulikuwa ukijengwa na mkandarasi *Hainan International Ltd.* kwa mkataba wa gharama ya shilingi bilioni 54.6 ambapo fedha toka ruzuku ya Serikali Kuu ni shilingi bilioni 50.9 na mapato ya ndani ya Halmashauri ya Ubungo ni shilingi bilioni 3.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Agosti, 2024 jumla ya shilingi bilioni 49.8 zimetumika katika kutekeleza mradi

huo na umefikia asilimia 97. Aidha, baadhi ya kazi zilizopangwa kutekekelezwa zimekamilika na nyingine zipo hatua mbalimbali za ujenzi, kama ujenzi wa *basement one and two*, ujenzi wa ghorofa ya tatu eneo la abiria na ujenzi wa eneo la kuingilia magari. Katika mwaka 2023/2024, Serikali kupitia mapato ya ndani ya halmshauri imelipa shilingi milioni 545 na shilingi bilioni 1.6 zipo kwenye utaratibu wa kumlipa mkandarasi ili kuendelea na ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu na uhitaji wa kituo hiki cha mabasi kwa wamiliki wa mabasi, abiria na wafanyabiashara, kwa mwaka 2024/2025, Serikali kupitia mapato ya ndani ya halmashauri imetenga shilingi bilioni 4.6 kwa ajili ya ukamilishaji wa kazi ambazo hazikukamilika ili kituo hiki kikamilike kwa asilimia 100, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Janeth Massaburi, swali la nyongeza.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya kituo hiki kiwe kivutio cha utalii ili kiweze kuongeza mapato? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Je, Serikali imeshindwa kuweka utaratibu wa mabasi yaendayo mikoani kuanza safari zao katika kituo hiki ili kuwe na utaratibu ambao utaweza kukiongezea mapato, ukifananisha na vituo kama reli na *airport* walivyoweka utaratibu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Kituo kile cha Mabasi cha Magufuli pale Mbezi ni moja ya vituo ambavyo vimejengwa kwa ubora sana katika nchi yetu na kinaendelea kukamilishwa kwa ubora unaostahili ili kiweze kuwa sehemu ya vituo ambavyo vinavutia utalii. Ndiyo maana kile kituo kinatumika na mabasi ya ndani ya nchi na mabasi ya kutoka nje ya nchi yetu na tunaamini

tutaendelea kuboresha huduma ili kituo kile kiweze kukidhi hali ya kuvutia wateja wengi, pia kuvutia hata watalii kujifunza namna ambavyo tunakitumia katika kusafirisha wananchi katika eneo letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, eneo hilo kwa ubora wake wa majengo, *design* yake na umaliziaji ambao tutaufanya kitakuwa ni kituo ambacho kinavutia sana na kitaleta tija kubwa kwa wananchi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tunaendelea na mazungumzo. Tunafahamu yapo mabasi yanayoanzia kwenye kituo cha mabasi cha Magufuli, lakini yapo mabasi ambayo yanaanzia kwenye vituo vyao maeneo mbalimbali. Tunaendelea kufanya mazungumzo na wamiliki wa mabasi na baada ya kukamilisha kile kituo cha mabasi tuone uwezekano wa mabasi yaliyo mengi, kama sio yote, kuanzia katika kituo kile cha Magufuli pale Mbezi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mbali ya kwamba Serikali imekuwa ikijenga vituo vya kisasa vya mabasi kwenye miji, na Mji wa Bunda ni mji ambao unakua, na hali ya Stendi ya Mabasi ya Bunda ni hatarishi kwa abiria na kwa wananchi wanaozunguka pale wakifanya biashara zao, na Serikali imetuahidi mara kadhaa kutujengea stendi ya kisasa katika Mji wa Bunda. Ni lini sasa Serikali itatujengea kama ambavyo imeahidi?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mji wa Bunda ni mji ambao unaokua kwa haraka, na Kituo cha Mabasi cha Bunda bado hakikidhi haja ya idadi ya wananchi kwa hadhi ya Mji wa Bunda. Serikali tayari imeshaelekeza, kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Halmashauri ya Mji wa Bunda kuleta andiko la kimkakati la kuomba fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo kile cha mabasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia mara kadhaa, lakini pili, namwagiza Mkurugenzi wa Mji wa Bunda kuleta andiko Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili lifanyiwe tathmini na kuona uwezekano wa kupata fedha. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa, changamoto kubwa ya Kituo cha Mbezi ni sehemu ya kuingilia magari yanayotoka mikoani, pamechimbika na wala hapafai. Je, Serikali ina mpango gani wa muda mfupi kuhakikisha wanarekebisha eneo hilo la lango la kuingilia magari yanayotoka mikoani ili magari yaweze kuingia vizuri zaidi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la eneo la kuingilia magari kuharibika ni suala linalohitaji matengenezo ya haraka. Kwa hiyo, natumia nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kumwelekeza Mkurugenzi wa Manispaa ya Ubungo kufanya tathmini kwa haraka, kutenga fedha mapato ya ndani na kufanya marekebisho ili mabasi yaweze kupita vizuri kuingia kwenye kituo hicho cha mabasi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea. Swali linalofuata namwita Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrissa Juma, Mbunge wa Jimbo la Mtoni, sasa aulize swali lake.

Na. 52

**Ujenzi wa Kituo cha Daladala na Soko, Kijichi**

**MHE. USSI SALUM PONDEZA K.n.y. MHE. ABDUL-HAFAR IDRISSA JUMA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza kutumia kwa ukamilifu Kituo cha Daladala na Soko, Kijichi katika Jimbo la Temeke?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Daladala na Soko la Kijichi vilijengwa kupitia Mradi wa Uboreshaji wa Miundombinu katika Jiji la Dar es Salaam *(DMDP)*. Mradi huu ulizinduliwa Septemba, 2019 ukihusisha uwepo wa miundombinu mbalimbali likiwemo jengo la ghorofa ambalo lilikusudiwa kutumiwa kama ofisi na huduma mbalimbali zinazoenda sambamba na maendeleo ya soko hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Halmashauri ya Manispaa ya Temeke ilifanya juhudi mbalimbali za kuhakikisha mradi huo unaanza kufanya kazi, kama ilivyokusudiwa, ikiwemo kuwapanga wafanyabiashara wadogo katika eneo hilo, kuelekeza mabasi yanayoelekea mikoa ya kusini kutumia kituo hicho. Kwa kuwa, bado kituo hicho na soko havitumiki kwa ufanisi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Halmashauri ya Manispaa ya Temeke inakamilisha uchambuzi wa mradi huo ili ubadilishiwe matumizi ikiwemo kumtafuta mwekezaji katika mradi huo ili awekeze na majengo hayo yaweze kutumika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pondeza kwa niaba ya Mheshimiwa Idrissa Juma, swali la nyongeza.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huu muda umekuwa mrefu sasa, kila siku majibu yamekuwa "Serikali inafanya upembuzi ya yakinifu" bila watu kuelekea kule katika kituo kipya. Je, Serikali ipo tayari kutupa *commitment* ni lini sasa itakuwa mwisho wa upembuzi yakinifu na tuweze kutumia kituo kile kwa sababu ya pesa nyingi za Serikali ambazo zimeweza kutumika? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba baada ya jitihada za kuwapeleka

wafanyabiashara wadogo pale kutokuwa na matunda ambayo yalitarajiwa, tayari Manispaa ya Temeke imeshaleta andiko na mapendekezo Ofisi ya Rais, TAMISEMI na tayari wataalamu wetu wanalipitia andiko lile ambalo linapendekeza kubadili matumizi ya kituo kile. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ndani ya miezi miwili tutakuwa tumeshapata majibu ya nini kinakwenda kufanyika na baada ya hapo tutatangaza fursa hizo kwa ajili ya wawekezaji wengine kutumia majengo yale kwa faida ya Wanatemeke na nchi yetu kwa ujumla, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ipo tayari au itakuwa tayari kuiwezesha Halmashauri ya Moshi Vijijini kuboresha Kituo cha Mabasi pale Njia Panda? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali siku zote ipo tayari ilimradi kama kituo hicho ni kipaumbele cha Halmshauri ya Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu kwamba Halmashauri ya Moshi Vijijini ifanye tathmini ya uhitaji wa soko hilo ione uwezo wa mapato yao ya ndani lakini kama hayatoshi, basi walete andiko Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili Serikali ione namna ya kuchangia kujenga kituo hicho cha mabasi, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea Wizara ya Nishati, sasa nimwite Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Njelu Kasaka.

Na. 53

**Kushusha Bei ya *Unit* za Umeme**

**MHE. MASACHE N. KASAKA K.n.y. MHE. SUMA I. FYANDOMO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itashusha bei ya *unit* za umeme?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya *unit* ya umeme inapatikana kulingana na gharama za uzalishaji, usafirishaji na usambazaji umeme. Bei ya sasa siyo halisia, ni bei ambayo ina ruzuku za Serikali ndani yake ambapo kwa sasa wastani wa bei ya *unit* moja ya umeme yenye ruzuku ni shilingi 100 (matumizi ya kawaida chini ya *unit* 75 kwa mwezi) na bila ruzuku ni shilingi 292.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa mwananchi anayetumia zaidi ya *unit* 75 kwa mwezi, analipa kiasi cha shilingi 292 kwa *unit* moja ya umeme ambapo kuna ruzuku ndani yake badala ya shilingi 320 bila ruzuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la kupunguza bei ya *unit* moja ya umeme, tutandelea kufanya tathmini ya gharama za utoaji wa huduma za *TANESCO* mara kwa mara na kuendelea kurekebisha bei kulingana na gharama za uzalishaji, usafirishaji na usambazaji zitakavyokuwa, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kasaka.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Kwa kuwa Bwawa la Mwalimu Nyerere sasa hivi limeanza uzalishaji na tuna umeme wa kutosha na ziada tunayo. Sasa hatuoni haja kwamba Serikali ipitie upya ukokotoaji wa hizi bei za *unit* na baadaye tuweze kushusha hizi bei ili kuweza kuleta nafuu kwa Mtanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, maeneo ya uchimbaji kuna mradi wa kupeleka umeme kwenye maeneo hayo hasa Wilaya yangu ya Chunya maeneo mengi umeme unaenda kwa kusuasua kwenye huu mradi na sasa mradi huu unaelekea ukingoni. Je, nini mkakati wa Serikali wa haraka kupeleka umeme maeneo haya ya uchimbaji ili wananchi wetu hawa wa maeneo ya uchimbaji waweze kunufaika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge. La kwanza kuhusiana na kuona umuhimu wa kushusha gharama kutokana na umeme wa ziada ambao unapatikana kwa kuanza kufanya kazi kwa Bwawa la Julius Nyerere, kwenye jibu langu la msingi nimesema gharama za umeme siyo gharama za uzalishaji peke yake, zinahusisha pia gharama za usafirishaji, usambazaji na uwekezaji na kwa sasa hata *unit* ya umeme ambayo wananchi wanatumia imewekewa ruzuku ya Serikali ili iweze kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nikasema kwa kadiri ambavyo tunaendelea kufanya tathmini tutaangalia namna ambavyo tunaendelea kuchakata bei hizi lakini hata kwa sasa wananchi wanapata bei hii wanayopata kwa sababu Serikali imeweka ruzuku. Hata ukilinganisha na nchi nyingine zote za Afrika Mashariki Tanzania ndiyo ina bei ndogo za umeme kuliko nchi zote. Kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge suala la kumuuzia mwananchi umeme tutaendelea kulichakata na tutaendeleza hizi ruzuku ili wananchi waweze kupata umeme kwa bei ambayo ni himilivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la pili la miradi kwenye uchimbaji, mradi huu ni mradi ambao unatekelezwa kwa zile fedha za UVIKO-19, nimwelekeze Mkurugenzi wa *REA* fedha hizi ni fedha ambazo ziliwekwa kwenye miradi ili kuleta unafuu kwenye maeneo ya uchimbaji na kufikisha huduma ili kuweza kuongeza tija kwenye masuala ya kiuchumi ya wananchi. Wahakikishe mkandarasi aliyekuwa *site* anatekeleza mradi huu kwa haraka na unakamilika kulingana na mkataba, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Genzabuke.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ya *Kasulu DC,* Shule ya Sekondari Nyenge iliyopo Kata ya Kurugongo ni shule mpya, lakini shule hiyo haina umeme. Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika shule hiyo mpya? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaenda kufanya tathmini na kuweza kuona namna gani shule hiyo inapata umeme. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na swali linalofuata, bado tupo Wizara ya Nishati. Namwita Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 54

**Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme Kata ya Mogitu - Hanang**

**MHE. ASIA A. HALAMGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Kupoza Umeme Kata ya Mogitu - Hanang?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Hanang unatarajiwa kufanyika wakati wa utekelezaji wa Mradi wa Gridi Imara Awamu ya Pili. Aidha, kwa sasa Serikali ipo kwenye hatua ya utekelezaji wa Mradi wa Gridi Imara kwa Awamu ya Kwanza ambapo miradi 27 inatekelezwa. Awamu ya pili ya Mradi wa Gridi Imara unatarajiwa kuanza kutekelezwa

mara baada ya kukamilika kwa miradi ya awamu ya kwanza, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halamga.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nitauliza swali moja dogo la nyongeza. Kwanza, nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa jitihada kubwa za kuendelea kutatua changamoto ya umeme katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Wilaya ya Hanang tumekuwa na changamoto ya muda mrefu ya kutumia *line* ya Babati ambapo umeme ukikatika Wilaya Babati, Jimbo zima la Wilaya ya Hanang umeme unakatika kwa kata zote 33. Je, nini kauli ya Serikali? Wakati sisi tukisubiri kuwekwa kwenye awamu ya pili ambayo tunaishukuru sana Serikali, nini sasa kitafanyika hapa ili tuweze kuondokana na changamoto hii? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Judith Kapinga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Mbunge. Ni kweli changamoto hii ipo kwa sababu *line* ile ni ndefu sana. Nimwelekeze Meneja wa Manyara ahakikishe wanaweka vikata umeme na kufunga kifaa cha mfumo wa kuongeza *voltage* ili kuhakikisha patakapotokea changamoto, basi kipande kidogo cha *line* tu ndiyo kiathirike, labda kukiwa na changamoto kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka kuboresha huduma kwa wateja na umeme, ukikatika, ikitokea hitilafu kipande tu kile mahususi ndicho ambacho kikose umeme na *line* nzima iweze kuwa na umeme. Kwa hiyo, wafanye tathmini hiyo ya kuweka vikata umeme na kama umeme ni mdogo waweke kifaa cha kuongeza *voltage* ili wananchi wa Hanang waweze kupata umeme wa uhakika, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Kupozea Umeme cha Mahumbika Mkoani Lindi kipo umbali wa zaidi ya kilometa 300 kutoka Liwale Mjini. Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kujenga kituo cha kupozea umeme Wilayani Liwale ili kupunguza shida ya kukatikakatika kwa umeme mara kwa mara?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachukua suala hili la Mheshimiwa Mbunge, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa sasa tunatekeleza mradi mkubwa wa kupeleka umeme wa gridi katika mikoa ya Mtwara na Lindi. Pamoja na kwamba suala hili ni la muhimu la kujenga Kituo cha Kupoza Umeme, tunaamini tukikamilisha mradi, maeneo yote ya Mkoa wa Lindi yataendelea kupata umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa azma yetu ni kuhakikisha wananchi wanaendelea kupata umeme wa uhakika na kadiri tunavyoendelea tutaendelea kuboresha miradi na kupeleka miradi kwa ajili ya kuhakikisha wananchi wanaendelea kupata umeme wa uhakika, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Kassinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kisiwa cha Songosongo katika Wilaya ya Kilwa ni moja ya sehemu ambazo zinazalisha umeme unaotokana na gesi asili lakini bado kuna changamoto kubwa ya upatikanaji wa umeme katika kisiwa hiki. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba Kisiwa cha Songosongo kinapata umeme wa uhakika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwa kweli kuna changamoto ya umeme na kwenye maeneo ambayo kuna miradi hii mikubwa kwa kweli siyo suala la kiungwana wananchi washindwe kunufaika na miradi ambayo

ipo katika maeneo yao. Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, alishatolea maelekezo juu ya kufanya taratibu ili kuhakikisha wananchi hawa sio tu wanapata umeme wa uhakika na kwa sababu miradi hii inatekelezeka, basi na huduma nyingine za kijamii ziweze kuimairishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa tayari tunalifanyia kazi, tutahakikisha wananchi hawa wa maeneo ya Songosongo wanapata umeme wa uhakika na huduma nyingine za kijamii ambazo zinaendana na miradi ambayo ipo katika maeneo yao, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, bado kuna maswali mengi kwenye Wizara hii. Tunaendelea, nampa swali moja tu Mheshimiwa Amar alikuwa amesimama mapema.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kwa sababu nimeshawasilisha kwako changamoto ya *transformer* ambazo zimezidiwa (idadi ni *transformer* tisa), je, ni lini sasa utekelezaji wa kupeleka *transformer* kubwa utafanyika? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Mheshimiwa Mbunge, alisema *transformer* zimezidiwa, nilituma timu ya wataalamu, jana walifanya tathmini na kugundua *transformer* tisa zinahitaji kubadilishwa, kwa sababu tumetambua hilo tunalifanyia kazi ili *transformer* hizo ziweze kubadilishwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea. Namwita sasa Mheshimiwa Dkt. Angeline Sylvester Mabula, Mbunge wa Ilemela, sasa aulize swali lake.

Na. 55

**Mahitaji ya Umeme Visiwa vya Ilemela**

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itawapatia umeme wa uhakika wananchi wanaoishi katika Kisiwa cha Bezi na Tefu Manispaa ya Ilemela?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* ilishaanza kushirikiana na Kampuni Binafsi ya *Powerhut Renewables Limited* katika Kisiwa cha Bezi kwa kutoa ruzuku kupitia mradi wa *Result-Based Financing* Awamu ya kwanza. Serikali kupitia *REA* inatarajia kuendelea kushirikiana na kampuni hiyo kwa kutoa ruzuku kupitia Mradi huu wa "*Result-Based Financing*" ili kumwezesha mwekezaji kuongeza miundombinu ya uzalishaji na pia kuimarisha miundombinu ya usambazaji na uunganishaji umeme wa wateja wengi hasa wale ambao walikuwa bado hawajaunganishiwa kupitia mradi huu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, huduma ya umeme wa *solar* unaopatikana katika Kisiwa cha Bezi una gharama kubwa kiasi kwamba mwananchi analipa shilingi 1,000 kwa *unit* na *unit* hiyo wala haitumiki kwa siku nzima. Je, hawaoni kwamba ni wakati mwafaka sasa wa kupeleka umeme wa gridi ili na wao waweze kufaidika na ruzuku inayotolewa Serikalini kama wengine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, pamoja na umeme huo wa *solar* ambao hauna uhakika hasa kipindi cha mvua

wanatozwa 1,000 lakini umeme wa gridi unatozwa shilingi 356. 24 hii ikiwa ni pamoja na tozo nyingine za *REA, EWURA* pamoja na *VAT,* je, ni lini Serikali itapitia upya bei anazotoza yule mwekezaji kule ili walau hawa waweze kupata nafuu ya ulipaji wa gharama ya umeme ukilinganisha na umeme wa gridi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nashukuru kwa maswali mawili ya Mheshimiwa Dkt. Angelina Mabula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, kuhusiana na kupeleka umeme wa gridi, visiwa hivi Tanzania nzima vipo 120 na tumeshaanza kufanya tathmini ya namna ya kufikisha umeme wa gridi, lakini tunaposubiria ndipo ambapo tumekuja na mradi huu wa kupeleka hizi *solar panel* na kuziuza kwa bei nafuu kulingana na ukubwa kati ya 55% mpaka 65% kwa kuweka ruzuku hiyo ili mwananchi aweze kupata umeme wa uhakika kwa muda wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshafanya tathmini ya kupeleka *underground cable* katika Kisiwa hiki cha Bezi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tunaendelea na tathmini na kutafuta fedha ili mwisho wa siku tuweze kufikisha umeme huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala hili la bei, ninachukua hilo Mheshimiwa Mbunge na kupitia *EWURA* tutapitia upya gharama hizi ili kuhakikisha mwananchi anauziwa umeme kwa thamani ya kile anachotumia, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sijaona mtu amesimama. Tunaendelea na swali linalofuta, bado tupo katika Wizara hii.

Sasa namwita Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, Mbunge wa Ushetu, aulize swali lake. Kwa niaba yake litaulizwa na Mheshimiwa Lucy Mayenga.

Na. 56

**Ruzuku Mitungi ya Gesi**

**MHE. LUCY T. MAYENGA K.n.y. MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI** aliuliza:-

Je, upi mkakati wa kuweka ruzuku kwenye mitungi ya gesi ili kuwawezesha wananchi kumudu gharama na kupunguza uharibifu wa mazingira?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwezesha wananchi kumudu gharama ya mitungi ya gesi, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* inaendelea kutoa ruzuku kwa wasambazaji wa mitungi ya gesi ili waweze kuuza mitungi hiyo kwa wananchi kwa bei ya punguzo ambapo kwa mwaka wa fedha 2023/2024, ruzuku iliwekwa kwenye mitungi ya gesi 104,000. Aidha, kwa mwaka huu wa fedha (2024/2025), Serikali kupitia *REA* imejipanga kutoa ruzuku kwenye mitungi 450,000, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucy Mayenga.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Licha ya kazi nzuri ambayo imekuwa ikifanywa na Wizara hii hasa Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini Wizara hii itahakikisha shauku ya akina mama ya kutumia mitungi ambayo ina mita inafanikiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, Wizara hii ni lini itakamilisha agizo la Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba wanakuja na teknolojia ili akina mama hasa wale wa Kishapu, Shinyanga na nchi nzima waweze kuwa na uwezo wa kununua gesi katika kiwango kidogo kidogo? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, naomba niyajibu kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Rais alitoa agizo la kuweza kuhakikisha tunarahisisha matumizi, lakini vilevile tunaweka teknolojia ambazo vitafanya mwananchi ananunue gesi kidogo kidogo kwa bei nafuu kuliko kununua kwa bei ya mkupuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kushirikiana na sekta binafsi, tayari tumeshanza kufanyia kazi na zipo kampuni ambazo zimeanza kuweka mita ambazo zinaonesha matumizi, lakini vilevile mita ambayo inamfanya mwananchi aweze kutumia kidogo kidogo. Tunaendelea kushirikiana na sekta binafsi ili kuhakikisha agizo hili la Mheshimiwa Rais linatekelezeka kwa haraka, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Janeth Mahawanga.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia mafanikio makubwa ya Serikali kwenye kutoa elimu ya matumizi ya nishati safi ya kupikia na sasa tumeona wananchi wameendelea kuwa wanahamasika. Sasa ni upi mpango wa Serikali kuhakikisha mawakala wa kutosha wanapatikana hususan kwenye maeneo ya vijijini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, alishafanya vikao na hizi kampuni ambazo zinahusika na *LPG* na kwa kweli tumeshahamasishana kuhakikisha wanaenda maeneo ya vijijini na wanaweka mawakala. Kwa kweli baadhi ya kampuni zinafanya hivyo kwamba ukitaka kufungua sehemu fulani, basi utatumia gharama ya kiasi fulani ili kuhamasisha wananchi waweze kupata uwakala katika maeneo ya vijijini. Kwa hiyo, tunaendelea kulifanyika kazi kwa nguvu sana ili kuhakikisha huduma hii ya gesi pia inafika maeneo ya vijijini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Boniphace Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Zaidi ya familia zaidi ya 1,500 zimekuwa zikitumia nishati hii ya gesi katika Wilaya ya Kishapu, changamoto kubwa ni namna ya kupata mawakala wanaotosheleza katika maeneo yote ya vijijini katika maeneo ya Wilaya ya Kishapu. Nini tamko la Serikali kuhakikisha kwamba inaongeza mawakala ili mradi huduma hii iweze kuwa endelevu katika maeneo hayo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitafanya tathmini ndogo na kuona kampuni ambazo zipo kishapu na nitazungumza nao ili kuweka mkakati mahususi kwa ajili ya kuongeza mawakala ili wananchi hawa ambao wanatumia nishati ya gesi Kishapu waweze kupata gesi hii kwa urahisi zaidi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Kapinga, kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea Wizara ya Ujenzi, namwita sasa Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, sasa aulize swali lake.

Na. 57

**Ujenzi wa Barabara ya Kahama – Nyang'hwale – Busisi – Sengerema**

**MHE. HUSSEIN N. AMAR** aliuliza:-

Je, lini upembuzi yakinifu utakamilika na kuanza ujenzi wa Barabara ya Kahama - Nyang'hwale – Busisi - Sengerema kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Kasekenya.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Barabara ya *Nyang'hwale Junction* eneo la Busisi kwenda *Wing 3* - Nyang'hwale – Nyang'holongo – Nyambula (Kahama) yenye urefu wa Kilometa 204.13 inaendelea kwa sehemu ya Busisi Ngoma – *Wing 3* yenye urefu wa Kilometa 55. Kwa sehemu ya Nyang'hwale – Nyang'holongo hadi Nyambula (Kahama) mkataba wa kuanza kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina utasainiwa Mwezi Septemba, 2024, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza Serikali kwa hatua hii ambayo inaenda kufikiwa ya kwenda kusaini mkataba huo kwa ajili ya upembuzi yakinifu mwezi Septemba. Pia naipongeza Serikali kwa kuendelea kukamilisha ujenzi wa kilomita moja Makao Makuu pale Karumwa.

Je, ni lini taa za barabara hiyo kilomita moja zitaanza kufungwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Nassor kwa kufuatilia sana hii Barabara. Nakumbuka katika majibu yetu tulimuahidi kwamba katika hiyo kilomita moja ambayo tuliahidi kuikamilisha ya lami na tumeikamilisha tutamwekea taa. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, hivi tunavyoongea, Mkandarasi ameshapatikana, yupo *site* na taa za kufunga hiyo kilomita moja zipo tayari Mjini Geita kwa ajili ya kufunga hiyo kilomita moja katika Mji wa Karumwa, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saashisha swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Moshi - Arusha pamoja na daraja la Kikafu tuliambiwa Mkandarasi ameshafika. Wananchi waliopisha lile

daraja la Kikafu wamesubiri muda mrefu kulipwa fidia. Je, tunaomba maelezo ya Serikali, nini kinaendelea kwa wananchi wale wanaosubiri fidia ya kupisha barabara ya Moshi - Arusha? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hii barabara tunajenga kwa kusaidiana na wenzetu wa *JICA* na tunavyoongea wanapitia ule usanifu. Hivi tunavyoongea wapo uwandani. Kwa hiyo, ni kwamba tutaanza haraka sana baada ya kukamilisha kupitia ule usanifu ikiwa ni pamoja na kulipa fidia kwa wananchi wote watakaopisha ujenzi huo wa barabara pamoja na eneo hilo la Daraja la Kikafu, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kungu.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taa za barabarani zinaleta ulinzi na usalama nyakati za usiku.

Je, ni lini Serikali itatufungia taa za barabarani Wilayani Tunduru?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea na kazi hiyo na tuliahidi kwamba maeneo yote ya mijini na hasa ambapo barabara za *TANROADS* zinapita kwenye miji, tutaendelea kufunga ikiwa ni pamoja na Mji wa Tunduru pia watapata taa, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Bado tupo Wizara ya Ujenzi. Namwita sasa Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali aulize swali lake. Kwa niaba yake swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Ali Juma Mohamed.

Na. 58

**Maboresho ya Alama za Barabarani**

**MHE. ALI JUMA MOHAMED K.n.y. MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI** aliuliza: -

Je, Serikali imejipangaje kufanya maboresho ya alama za barabarani?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Ujenzi kupitia *TANROADS*, imetenga fedha kiasi cha shilingi za Kitanzania bilioni 2.55 kwa ajili ya uwekaji wa alama na michoro ya usalama barabarani kwenye barabara kuu na zile za Mikoa ikiwemo uwekaji wa alama za watu wenye mahitaji maalum katika Mikoa yote 26, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ali Mohamed nimekuona.

**MHE. ALI JUMA MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nilikuwa na swali moja la nyongeza. Kwa vile bado kuna wimbi la ajali nyingi za barabarani hususan katika maeneo yale ya vivukio kwa maana ya *zebra cross,* Serikali haioni haja sasa ya kuweza kuweka miundombinu ya kisasa ili kuweza kudhibiti ajali hizi zisiweze kutokea mara kwa mara? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli lakini niseme tu, kumekuwa na changamoto kubwa ya watumiaji wa barabara kutozingatia alama za barabarani, alama zote za barabarani tunazozitumia Tanzania kwa sasa zinafikia 183 na sasa zimeenda mpaka 180 kwa ajili ya hawa watu wenye mahitaji maalumu.

Mheshimiwa Mwenyeiti, hizi alama tunazozitumia ndiyo zinazotumika kwenye *East Africa* na *SADC*. Kwa hiyo, ndiyo alama

ambazo zinatambuliwa labda kama Mheshimiwa Mbunge kuna alama ambazo tutahitaji kuziweka mpya, basi maana yake lazima tukubaliane kwenye hizi Afrika Mashariki na wenzetu wa *SADC* kwa sababu wote ndiyo tunaozitumia hizo alama, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea na Wizara ya Afya. Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge. Tunakwenda Wizara ya Afya, namwita sasa Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli Mbunge wa Segerea, sasa aulize swali lake. Haonekani na hamna *volunteer*? Mheshimiwa Anatropia kwa niaba.

Na. 59

**Wanufaika wa Toto Afya Kadi Kuendelea Kuhudumiwa**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST K.n.y. MHE. BONNAH L. KAMOLI** aliuliza:-

Je, kwa nini wanufaika wa Toto Afya Kadi wasiendelee kuhudumiwa huku taratibu za Bima ya Afya kwa wote zikisubiri kukamilika?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanufaika wa Toto Afya Kadi wanaendelea kunufaika isipokuwa mfumo wa kulipia bima za watoto kupitia Toto Afya Kadi umebadilika. Kwa sasa usajili wa Toto Afya Kadi unafanyika kupitia utaratibu wa shule na vifurushi vya Bima ya Afya vya Najali, Wekeza na Timiza ambapo wanajiunga kupitia wazazi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanza utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote utawezesha makundi mbalimbali ya wananchi wakiwemo watoto kupata huduma za afya kwa urahisi pasipokuwa na vikwazo vyovyote, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri juu ya *Toto Afya Card,* kumekuwepo na taharuki juu ya matumizi ya Bima ya Afya nchini na hasa Bima ya *NHIF*. Kumekuwepo na maelezo au na taarifa mbalimbali kutoka hospitali moja maarufu hapa nchini Agha Khan ikieleza kusitisha huduma zake za Bima ya *NHIF*. Tungetaka kupata kauli ya Serikali au waeleze Watanzania nini hatma ya matumizi ya Bima ya *NHIF,* kwa kuwa wengi wamekuwa wakipata huduma katika hizi hospitali za Agha Khan na zipo maeneo mengi nchi nzima, nini kauli ya Serikali? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla kwamba, Serikali inatambua umuhimu wa Bima ya Afya kwa Watanzania wote na ndiyo maana imeendelea kutoa huduma ya bima ya afya kupitia *NHIF* lakini tunatambua pia umuhimu wa kuwa na uendelevu wa Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pamoja na huduma ambazo zinaendelea kutolewa, Serikali inaendelea kufanya tathmini na kuweka mipango thabiti kuhakikisha kwamba mfuko wenyewe unakuwa endelevu lakini pia na huduma zinaendelea kutolewa kwa wananchi. Kama tutakumbuka tumeshatunga Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, kwa hiyo, tutaendelea kuhakikisha tunaboresha pamoja na hospitali ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja, maongezi na mazungumzo yanaendelea kwa Serikali na Mfuko wa Serikali wa Bima ya Afya ya Taifa kuona namna nzuri ya kuendelea kutoa huduma. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea, nimwite sasa Mheshimiwa Tamima Haji Abass, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 60

**Mafanikio ya Tiba Mtandao**

**MHE. TAMIMA HAJI ABASS** aliuliza:-

Je, huduma ya tiba mtandao imeleta mafanikio gani tangu imeanzishwa nchini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya tiba mtandao imeanza kutolewa kuanzia Novemba 2023 hadi sasa huduma hii imeunganishwa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa 17, Hospitali za Kanda Nne, Hospitali Maalum Tatu pamoja na Hospitali ya Taifa Muhimbili. Huduma hii imeleta mafanikio makubwa kama ifuatavyo: -

(i) Jumla ya wagonjwa 676 wamepata huduma ya Tiba Mtandao katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, Kanda na Taifa kuanzia Novemba, 2023 hadi Julai 2024.

(ii) Kiasi cha shilingi milioni 270 ambacho kingetumika kuwezesha rufaa za wagonjwa kimeokolewa na kutumika kwa shughuli nyingine katika vituo vya huduma.

(iii) Wataalamu 275 wamewezeshwa kupata mafunzo ya kutumia mfumo huu, hivyo kuwaongezea ujuzi.

(iv) Wananchi kupata huduma za kibingwa na bobezi bila kujali umbali au eneo waliko. Kwa mfano, mgonjwa yuko Katavi anaweza kubaki pale Katavi na akapata huduma za Kibingwa zisizopatikana Katavi kupitia tiba mtandao kutokea hospitali ya mbalimbali.

(v) Huduma hii imesaidia kupunguza gharama kubwa ya kutafuta matibabu ya kibingwa na bobezi kwa

wananchi kwa kuzileta karibu kupitia huduma hizi za tiba mtandao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tamima swali la nyongeza.

**MHE. TAMIMA HAJI ABASS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa huduma hii ni muhimu je, mnao mpango gani wa kuiunganisha na hospitali zilizopo Zanzibar ikiwemo Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja pamoja na hospitali kuu iliyopo Pemba kwa Zanzibar? *(Makofi)*

Swali namba mbili, je, ni magonjwa ya aina gani ambayo yanatibiwa kwa kupitia huduma hii ya tiba mtandao? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo anafuatilia juu ya huduma hizi za tiba mtandao, lakini nimhakikishie tu kwamba nchi yetu ni moja, Wizara ya Afya Tanzania Bara pamoja na Wizara ya Afya Zanzibar tutafanya mazungumzo na kuona uwezekano wa kuunganisha mtandao huu wa tiba mtandao kwa nchi nzima kwa maana ya Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara ili wananchi wa pande zote waendelee kupata huduma bora za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, magonjwa ambayo yanatibiwa kwa utaratibu huu wa tiba mtandao ni magonjwa karibu yote hususan magonjwa yanayohusisha masuala ya *CT-Scan, MRI, X-Rays* ambapo mgonjwa kutoka sehemu ambayo haina Madaktari Bingwa wa huduma hiyo wanaweza wakatuma picha kimtandao kwenda kwenye hospitali kwa mfano, Muhimbili na Madaktari Bingwa wakasoma na kutoa majibu na ushauri wa matibabu wakati huo huo na mgonjwa akanufaika pale alipo. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea Wizara ya Mifugo na Uvuvi, namwita sasa Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Makete, sasa aulize swali lake.

Na. 61

**Mkakati wa Kubinafsisha Shamba la Kitulo**

**MHE. FESTO R. SANGA** aliuliza:-

Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kubinafsisha Shamba la Mifugo Kitulo?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shamba la Kuzalisha Mifugo Kitulo lipo katika Wilaya ya Makete, Mkoani wa Njombe linamilikiwa na Serikali likiwa ni eneo lenye jumla ya hekta 4,875. Madhumuni ya kuanzisha shamba ilikuwa kuzalisha mitamba na ng'ombe bora wa maziwa na kuuza kwa wafugaji. Shamba hili lilianzishwa mwaka 1975 likiwa na ng'ombe wa maziwa 1,049 aina ya *Friesian* ambapo mwaka 1995 hadi 2001 shamba lilikuwa chini ya Kampuni ya Serikali ya Ng'ombe wa Maziwa - *DAFCO*.

Shamba hilo liliwekwa kwenye mpango wa kubinafsishwa baada ya *DAFCO* kukosa uwezo wa kuliendesha kwa ufanisi ambapo mwaka 1998 shamba liliwekwa chini ya Shirika la Kurekebisha na Kubinafsisha Mashirika ya Umma - *PSRC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, shamba hilo halikubinafsishwa, na mnamo mwaka 2003 Shamba lilirejeshwa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo ambapo kwa sasa ni Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Aidha, toka shamba hilo lirejeshwe Wizara haijawahi kuwa na mpango wa kulibinafsisha ila Serikali inaendelea na mikakati ya kuboresha shamba hili mwaka hadi mwaka kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka 2022/2023 Serikali ililiboresha shamba hili kwa kuliongezea ng'ombe wazazi 160 na kununua trekta moja kwa ajili ya shughuli za shambani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo Richard Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa majibu waliyonijibu na naomba niulize swali moja tu la nyongeza. Mheshimiwa Waziri kwanza atakubaliana nami kwamba uhitaji wa maziwa nchini ni mkubwa. Pili, atakubaliana nami kwamba uboreshaji na uwekezaji kwenye Shamba la Kitulo upo chini, na tatu, atakubaliana nami kwamba kuna uhitaji wa lile shamba kuongezewa mifugo. Sasa kwa muktadha wa kuwekeza kwa *level* ya ubia kati ya Serikali aidha na sekta binafsi, je, Serikali haioni mkakati wa wazi na wa makusudi kuwekeza kwenye shamba hili ambalo lipo katika eneo zuri sana kwenye kuzalisha maziwa na kuzalisha mitamba lakini uzalishaji wake upo chini?

Je, Serikali kwa makusudi kabisa haioni umuhimu wa kutafuta angalau nusu ya shamba ikagawa ikampa mwekezaji akawekeza na Serikali ikapata manufaa na wananchi wakapata manufaa ya shamba hilo?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakubaliana na hoja zote tatu za Mheshimiwa Sanga, na kwa kweli nitumie nafasi hii kumpongeza sana kwa sababu amekuwa mfuatiliaji mkubwa sana wa shamba hili na namna ambavyo amekuwa akitoa ushauri katika kuleta tija kwa wafugaji wetu wanaozunguka katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhitaji wa maziwa ni mkubwa, hilo linafahamika. Nami niungane naye kwamba uwekezaji unahitajika kufanyika kwenye shamba letu, lakini pia kuongeza mifugo katika shamba hili. Yote haya tunakubaliana naye na tayari Serikali tumeshapokea mawazo yake ya maandishi kuona ni namna gani tutafanya katika kuwekeza kwenye shamba hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri kwamba tumechukua mawazo yake, tutakwenda kuyafanyia kazi na kisha tutamletea majibu kwa maandishi tuone namna ambavyo shamba hili linaweza likaboreshwa katika kipindi hiki, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea na swali linalofuata. Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa Mheshimiwa Mbunge. Tunaelekea Wizara ya Madini, nimwite sasa Mheshimiwa Aloyce John Kamamba Mbunge wa Buyungu, sasa aliulize swali lake.

Na. 62

**Mapato ya Madini Kakonko**

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA** aliuliza:-

Je, fedha kiasi gani zimepatikana kutokana na madini katika Wilaya ya Kakonko kuanzia mwaka 2019 hadi 2023?

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kakonko ni miongoni mwa Wilaya zilizojaliwa kuwa na madini ya dhahabu nchini. Madini mengine yanayopatikana katika Wilaya hiyo ni madini ujenzi ambayo kwa sehemu kubwa yamechangia katika ujenzi wa barabara zinazounganisha Wilaya hiyo na maeneo mengine nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2019 hadi 2023 jumla ya shilingi 924,685,884.00 zilikusanywa kutokana na madini yaliyozalishwa katika Wilaya ya Kakonko, ambapo kati ya fedha hizo shilingi 725,171,133.52 zilizotokana na mrabaha na shilingi 199,514,750.46 zilizotokana na ada ya ukaguzi wa madini yaliyozalishwa kwa kipindi kinachorejewa. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aloyce Kamamba swali la nyongeza

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kwanza nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri katika majibu yake ametaja fedha nyingi tu, sasa nahitaji kujua, katika fedha hizo ni kiasi gani ambacho Wilaya yetu ya Kakonko imepata na fedha hizo zimeelekezwa katika maeneo yapi?

Swali la pili, changamoto ambayo inawakabili wachimbaji wadogo wadogo wa dhahabu na madini mengine katika Wilaya ya Kakonko ni mtaji mdogo. Sasa ni upi mkakati wa haraka wa Serikali kuwawezesha wachimbaji wadogo wadogo hasa katika vijiji vya Nyamwilonge, Luhuru, Kasuga na Kabingo ambao wanaendelea na uchimbaji sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mbunge wa Kakonko, Mheshimiwa Kamamba kwa maswali yake mazuri na nimjulishe tu kwamba, kwa mujibu wa Sheria ya Madini na kanuni zake, tunapotoza fedha za mrabaha na ukaguzi pia kuna tozo ya 0.3% ambayo hutonzwa kwa ajili ya *service levy* au ushuru wa huduma ambazo fedha hizo huenda moja kwa moja ndani ya Halmashauri husika na kuingizwa kwenye matumizi ya mapato ya ndani ambayo hupangiliwa matumizi yake na miradi itakayoendelezwa na Baraza la Madiwani. Kwa hiyo, kwa kipindi rejewa zaidi ya shilingi 60,891,000.00 zilitengwa kupitia hizo tozo za *service levy.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali lake la pili, kwamba kuna changamoto za wachimbaji wadogo hasa kwenye suala la kimitaji, Serikali kupitia Wizara ya Madini na taasisi zake, ina mpango mahususi wa kupita katika mikoa yote ya kimadini nchini kutoa elimu juu ya sheria, kanuni, taratibu na miongozo ambayo wachimbaji wadogo wanatakiwa waifahamu ili waweze kupata mikopo ambayo hutolewa kwa riba nafuu na benki ambazo

tayari Wizara kupitia taasisi yake ya *STAMICO* wana mikataba nao ili waweze kutoa mikopo, lakini ni lazima kwanza waelimishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumwelekeza Afisa Madini wa Mkoa wa Kigoma, aandae semina kwa ajili ya wachimbaji wadogo wa Kakonko wapate uelewa huo ili waweze kujua fursa zilizopo za kupata mikopo ya kuendeleza uchimbaji wao. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nimekuona Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Eneo la Kijiji la Mdundualo na Mgazini kuna madini ya makaa ya mawe na baadhi ya wachimbaji wameanza kuondoka. Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka wataalamu wakaangalie ubora wa haya makaa ya mawe ili wachimbaji hao wasiondoke kwenye hiyo sehemu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ndiyo napata hizi taarifa kwamba kule Mgazini wachimbaji wa makaa ya mawe wanataka kuondoka, basi natumia fursa hii kuielekeza taasisi yetu ya *STAMICO* inayohusika, wafike eneo hilo na kukutana na hao wananchi na kuangalia ubora wa hayo madini ya makaa ya mawe ili wachimbaji hao waweze kuendelea na shughuli zao.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tunaendelea. Mheshimiwa Naibu Waziri, nakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Namwita Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, aulize swali lake.

Na. 63

**Kukarabati Skimu ya Umwagiliaji Mariwanda - Bunda**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka fedha kukarabati Skimu ya Umwagiliaji ya Mariwanda – Bunda? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, kwa niaba yake Mheshimiwa Geophrey Pinda.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Skimu ya Mariwanda iliyopo Wilaya ya Bunda ina ukubwa wa hekta 400. Kati ya hekta hizo, hekta 180 zilijengewa miundombinu ya umwagiliaji kwa kutumia fedha za Mradi wa Kuendeleza Skimu Ndogo za Umwagiliaji *(Small Scale Irrigation Development Project)* awamu ya tatu mwaka 2018/2019 hadi 2020/2021. Pamoja na mradi huu wenye hekta 180 kuendelea kutumika, unahitaji ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ya Kilimo kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imepanga kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji katika eneo lililotajwa la hekta 180 pamoja na usanifu wa miundombinu ya umwagiliaji katika eneo lenye ukubwa wa hekta 220 ili kufanya eneo litakalomwagiliwa kufikia hekta 400. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza, nawashukuru Wizara ya Kilimo kwa kufanya kazi ya Skimu ya Mariwanda, kwa sababu Wizara imetoa trekta kwa ajili ya Wanachama wa Mariwanda. Tatizo kubwa ambalo swali hili limeuliza ilikuwa kuja kukarabati Lambo la Mariwanda ambalo linatumika kwenye skimu na Viongozi wa Mariwanda na Wanachama walishakuja kwa Mheshimiwa Waziri, wakakaa na

viongozi wote na idara zote za umwagiliaji. Swali sasa, ni lini wataenda kukarabati lambo ambalo maji yake yanataka kutoka yote? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, nakuomba Mheshimiwa Naibu Waziri kama inawezekana, mwende mkatembelee Lambo la Mariwanda ili mweze kujionea hali halisi ilivyo. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kama tulivyojibu kwenye swali la msingi, tayari ile Tume ya Umwagiliaji imeelekezwa kwenda kule kwa ajili ya kufanya tathmini, lakini namwomba Katibu Mkuu wa Wizara hii ya Kilimo aweze kutuma timu maalum kwa ajili ya kwenda kukomboa lile bwawa lisije likaharibika. Tathmini nyingine zinaweza zikaendelea, lakini huku kuepusha uharibifu kufanyike kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili la kutembelea lambo. Mheshimiwa Mbunge tukimaliza kujibu swali hili, tutakaa na kukubaliana namna ya kwenda kutembelea lambo hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Jimbo la Kalenga lina skimu zaidi ya 19 ambazo ni chakavu sana. Nini mpango na mkakati wa Serikali kuhakikisha Skimu hizo zinakarabatiwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, sasa hivi Wizara ya Kilimo ina mkakati wa kubainisha malambo yote na ile miradi yote ambayo ni chakavu na kuifanyia matengenezo upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama utakumbuka Wizara ya Kilimo tumepewa fedha nyingi mwaka huu kwa ajili ya kazi maalum ya kuinua hii Sekta ya Kilimo. Kwa hiyo, naomba usiwe na wasiwasi, wataalamu watakwenda kwenye maeneo haya na kwenda kujiridhisha juu ya uharibifu wake, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Samweli Hhayma.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kinipa nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Serikali ilikuwa imepata mkandarasi kwa ajili ya upanuzi na ukarabati wa Skimu ya Endagaw. Mkandarasi huyo aliposhindwa kazi, mwingine bado hajapatikana. Je, ni lini mkandarasi mwingine atapatikana na pia kuwashirikisha wananchi wa eneo hilo ili kuhakikisha kwamba wale waliopisha skimu wanapata au wanahusishwa kwenye upanuzi huu mpya ambao utafanyika? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taratibu za kawaida ni kwamba mkandarasi mmoja anapoondoka kunaanza mchakato wa mkandarasi wa pili. Mheshimiwa Mbunge, mchakato huu unaendelea na baada ya muda tutamleta mkandarasi mwingine kuendelea na zoezi hilo. Vilevile ushirikiano na wananchi utakuwa ni mkubwa sana ili waweze kunufaika kwa sababu tunaowawekea miundombinu ni wananchi wenyewe, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, nakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na swali linalofuata ambalo liko Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Namwita sasa Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni, aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 64

**Utaratibu wa Kufuata kwa Wananchi Waliobambikwa Kesi na Polisi**

**MHE. USSI SALUM PONDEZA** aliuliza:-

Je, utaratibu gani wananchi wanapaswa kuufuata ili kufikisha malalamiko yao pindi wanapobambikiwa kesi na polisi nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi linaongozwa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu katika kutekeleza majukumu yake nchini. Utaratibu wa kuwasilisha malalamiko pindi mwananchi anapotendewa kitendo chochote ambacho ni kinyume na maadili ya Jeshi la Polisi, anaweza kuwasilisha malalamiko yake kwa *OCS* yaani ngazi ya Kituo, *OCD* kwa ngazi ya Wilaya, kwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa, yaani *RPC* na kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, upo mfumo wa kiserikali (*e* – Mrejesho) wa kutuma, kupokea na kushughulikia malalamiko. Endapo mwananchi hatashughulikiwa malalamiko yake anaweza kuwasilisha Wizarani kwenye Kitengo Maalum cha Malalamiko ambacho kinahusika na malalamiko yote kwa vyombo vya usalama vilivyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na pindi askari huyo akibainika kufanya kosa hilo, hatua kali za kisheria huchukuliwa dhidi yake ikiwa ni pamoja na kushtakiwa kijeshi, kufukuzwa kazi na kufikishwa Mahakamani. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pondeza.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa jibu lake ambalo amesema unapopeleka malalamiko ya kubambikiwa

kesi, apelekewe *OCS, OCD, RPC* au Mkuu wa Jeshi la Polisi. Pia, wameanzisha mfumo wa e-Mrejesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, e–Mrejesho ni mfumo ambao unapatikana kidijiti, wananchi wengi au wote siyo wenye simu za kidijiti. Atafikishaje kwa kutumia e–Mrejesho (dijitali) hizi taarifa zake za ubambikiwaji wa kesi... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, swali.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Jeshi la Polisi halioni kama umefika wakati sasa wa kutoa elimu kwa wananchi wenye simu za *Android* na zisizo-*android* ili wafahamu jinsi ya kuwasilisha malalamiko yao kwa sababu wanaowasilisha malalamiko au wanaoonewa sana kutekwa na kupotea ni wananchi wengi zaidi wale ambao hawana uwezo wa kutumia simu hizi? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri. Sasa kutokana na hii hali kuwa imekuwa ipo muda mrefu na ipo kwa wingi sana na malalamiko yamekuwa yakipelekwa sana kwenye Jeshi la Polisi. Je, Serikali na Wizara ya Mambo ya Ndani haioni sasa inafaa kumwamrisha Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, atenge angalau siku moja katika mwezi ya kusikiliza malalamiko ya wananchi ambao wanabambikiwa kesi; wale ambao watakuwa hawana uwezo wa kufikisha malalamiko yao kwa e–Mrejesho lakini wanaweza wakaenda? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu. Mheshimiwa umeeleweka. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Ussi kwa kuhakikisha kwamba anataka wananchi waweze kufahamu

mfumo huu na kwa namna ambavyo wanaweza kufikisha malalamiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo njia ambazo kwanza nataka niseme kwamba kuna mifumo mingi sana katika Jeshi la Polisi na vyombo vingine ambavyo hutumika katika kutoa huduma kwa Polisi wenyewe ama Majeshi wenyewe pamoja na wananchi. Kwa upande wa mfumo huu wa *e*–Mrejesho, kama ambavyo nimesema ni mfumo ulioanzishwa kwa ajili ya kutuma, kupeleka na kupokea malalamiko ya wananchi yanayosababishwa na mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, tumekuwa tukitumia vyombo vya habari kama televisheni, redio, magazeti na mitandao ya kijamii katika kueleza na kuufahamisha mfumo huu. Pia, ziara za viongozi mbalimbali wa Jeshi la Polisi, *RPC's, OCD's, OCS* na Kamshina wa Polisi Zanzibar na *IGP's* wanapofanya ziara huko kwenye vijiji, kata na shehia, huwa wanausema na kuutolea maelezo mfumo huu na hata kwa kupitia dhana yetu ya ulinzi shirikishi huwa tunaueleza mfumo huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni mfumo rahisi na ni mfumo ambao tutaendelea kuendelea kuwapa elimu wananchi ili sasa wale ambao hawana namna ya kuwafikia viongozi waweze kutuma malalamiko yao huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine nataka niseme tu, niwaambie Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwamba, Ofisi ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi iko wazi saa 24. Muda wowote wananchi wanaweza wakaenda ikiwa kama wataandika barua, ikiwa kama watamwona Mheshimiwa Waziri na ikiwa kama watampigia simu, taarifa zitafika na malalamiko yatapokelewa na kufanyiwa kazi. Pia... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, malizia kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kubwa nataka nitoe tu ushauri kwa Waheshimiwa Wabunge, yeyote ambaye anahisi ana

changamoto ya malalamiko, aidha ya kubambikiziwa au mengine, basi aione Ofisi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi au hapa hapa Bungeni ili tuone namna ya kuweza kumsaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hatua kali ambazo Mheshimiwa Waziri ameziainisha hapa, lakini ukweli ni kwamba, kumekuwa na mwendelezo wa raia kubambikiwa kesi na Askari Polisi. Sasa nataka kujua, kuna askari wowote ambao wameshachukuliwa hizi hatua kali baada ya kugundulika wamebambikia kesi wananchi ili iwe fundisho kwa wengine na kukomesha tabia hizi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Matiko kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Mheshimiwa Mbunge afahamu kwamba Jeshi la Polisi linafanya kazi zake kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa. Katika jibu langu la msingi nimesema, askari yeyote atakayeshiriki kwenye vitendo vya kubambikiza kesi au vya kinyume na utaratibu, hatua za kisheria na kinidhamu zitachukuliwa zikiwemo za kiaskari na nyingine za Mahakamani na kufukuzwa kazi. Kwa hiyo, nimwambie tu kwamba, kama atakuwa ana ushahidi na askari amefanya hilo, aje ili tujue namna ya kushughulika na hilo jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea; bado tuko Wizara ya Mambo ya Ndani. Sasa namwita Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Moshi Mjini, aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 65

**Kuboresha Makazi ya Polisi Nchini**

**MHE. PRISCUS J. TARIMO** aliuliza:-

Je, upi mpango wa Serikali wa kuboresha makazi ya askari wa Jeshi la Polisi nchini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Hamza Khamis, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na mpango wake wa kuboresha makazi ya Askari Polisi kwa kujenga nyumba bora na kuzifanyia ukarabati nyumba zilizopo ambazo nyingi ni za zamani na zimechakaa. Katika bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2024/2025 zimetengwa fedha kiasi cha shilingi 224,000,000.00 na kwenye Mfuko wa Tuzo na Tozo kwa mwaka 2024/2025 zimetengwa fedha kiasi cha shilingi bilioni 15.6 kwa ajili ya ukarabati na ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali itaendelea kutenga fedha toka kwenye Bajeti ya Serikali na kwenye mfumo ama Mfuko wa Tuzo na Tozo kila mwaka kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za makazi, ofisi na Vituo vya Polisi pamoja na kufanya ukarabati ili kuboresha makazi ya Askari Polisi nchini. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Priscus Tarimo, swali la nyongeza.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali; na kwa kuwa uhitaji ni mkubwa kuliko *resources* tulizonazo; je, hawaoni sasa umuhimu wa kushirikisha Taasisi za Serikali kama *TBA* na *NHC* ili kuharakisha na kufikia nyumba nyingi zaidi kwa wakati mmoja, kukarabati pamoja na kujenga? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, pamoja na ukarabati sasa wa nyumba, liko suala la miundombinu. Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha miundombinu hiyo inarekebishwa? Kwa mfano, Chuo cha Polisi Moshi ambacho sasa kesho kutwa tunaenda kufanya miaka 105 ya kuanzishwa kwa Jeshi la Polisi, barabara zake zile za lami zimekwisha kabisa. Nini mpango wa Serikali kuzitengeneza barabara hizo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tarimo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, Jeshi la Polisi huwa tunatumia taasisi mbalimbali zikiwemo fedha zetu za ndani wenyewe kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunaimarisha majengo, makazi na ofisi. Sasa namwambia tu Mheshimiwa kwamba, hili naomba tulichukue twende tukakae na wenzetu *TBA* na hawa *NHC* ili tuone namna ambavyo tunaweza tukashirikiana na tukaingia makubaliano ya kuweza kujenga na kuzifanyia ukarabati hizi nyumba ili ziweze kutumika kwa Askari Polisi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa barabara nimwambie pia atupe muda tulichukue twende tukakae na wenzetu wa *TARURA* kwa sababu kuna barabara zilizoingia katika maeneo ya vituo, maeneo ya makazi na maeneo mengine. Ziko zile *periodic maintenance* na ziko zile *spot maintenance*. Sasa tufanye utafiti kwanza tujue zipi zinahitaji *periodic* na zipi zinahitaji *spot maintenance* ili tuone namna ambavyo tunaweza tukatatua changamoto hii, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Catherine Magige, swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, wananchi wa Wilaya ya Longido Kata ya Kamwanga kwa nguvu zao wenyewe walishirikiana wakajenga

Kituo cha Polisi lakini wamebakiza hatua chache mno. Mheshimiwa Naibu Waziri aliyepita Mheshimiwa Sagini alienda wakafanya tathmini, wakasema kuwa wanahitaji shilingi milioni 22. Serikali iliahidi kupeleka lakini hadi sasa haijatekeleza ahadi yake. Je, ni lini sasa Serikali itatekeleza ahadi hii kwa wananchi wa Kata ya Kamwanga? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Magige kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwambie Mheshimiwa Mbunge, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote, ahadi zote zilizoahidiwa na Serikali zinakwenda kutekelezwa. Namwambia tu Mheshimiwa Mbunge kwamba awe na subira, fedha zinatafutwa ili tukamalize hicho Kituo cha Polisi huko alikosema. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mussa Sima.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kumekuwa na uchakavu wa miundombinu ya majengo ya Vituo vyetu vya Polisi hususan vituo hivi vya mikoa pamoja na uchakavu wa samani zake. Serikali imeweka mkakati gani wa kuboresha vituo hivi na kuweka samani mpya zinazoendana na wakati? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najibu swali la Mheshimiwa Sima, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika jibu letu la msingi kwamba, tunatafuta fedha ingawa nyingine tumeshazipata na tunataka tukaanze ukarabati lakini bado

tunaendelea kutafuta fedha ili kuona namna ambavyo tunakwenda kukarabati na ikiwezekana kujenga kabisa hivyo vituo na kuzirekebisha hizo samani. Namwomba tu Mheshimiwa awe na Subira. Serikali iko mbioni kuona namna ambavyo tunarekebisha haya mambo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Munde.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii ili niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Tabora Manispaa ni mji mkubwa na wa siku nyingi lakini mpaka leo hii nyumba zake za Polisi hazijakarabatiwa. Je, ni lini Serikali inajipanga kwenda kukarabati nyumba hizo za Polisi Tabora Manispaa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Munde kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema katika jibu la msingi kwamba, kuna fedha zimetoka kwenye Tuzo na Tozo takribani shilingi bilioni 15 ambazo hizi lengo lake, tunakwenda kufanya ukarabati wa nyumba za makazi kwa ajili ya Jeshi la Polisi. Namwambia Mheshimiwa, katika fedha hizi tutahakikisha zinafika katika Mkoa huo wa Tabora na tunarekebisha hizo nyumba. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Maganga, swali la nyongeza.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Mheshimiwa Waziri, naomba nijue Askari Polisi wa Mbogwe hawana nyumba za kuishi, wanaishi mitaani. Nini mpango wa Serikali kutoa pesa ili kuwajengea askari wale? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA) K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maganga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli na kama tulivyosema katika jibu letu la msingi kwamba bado tuna changamoto ya makazi zaidi ya yale ambayo yameshakaa kwa muda mrefu na mengine bado askari wanakaa kwenye nyumba nyingine, nimwambie tu Mheshimiwa Maganga kwamba Serikali ya Mheshimiwa Mama Samia itajenga, kwa maana ya kwamba tunaendelea kutafuta fedha, na zitakapopatikana tutahakikisha kwamba askari wa Mbogwe wanakaa kwenye makazi mazuri ya kisasa ambayo wanaweza wakakaa kama askari. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Naibu Waziri nakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge. Tunakwenda Wizara ya Fedha, namwita sasa Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake. Kwa niaba yake, endelea Mheshimiwa Minza.

Na. 66

**Kulipa Wazabuni na Wakandarasi Rukwa**

**MHE. MINZA S. MJIKA K.n.y. MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itawalipa fedha wazabuni na wakandarasi waliotoa huduma mbalimbali katika Mkoa wa Rukwa ambao hawajalipwa miaka mitano sasa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya kulipa madeni ya wazabuni na wakandarasi yaliyohakikiwa na kukubaliwa na Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali. Kwa mwaka 2023/2024 jumla ya shilingi bilioni 600 zilitengwa kwa ajili kulipa madeni ya wazabuni, wakandarasi, watumishi na watoa huduma. Hadi Juni, 2024 jumla ya shilingi bilioni 491.25 zilitolewa kwa ajili ya kulipa madeni ya wazabuni na wakandarasi. Aidha, Serikali itaendelea kulipa madeni ya wazabuni na wakandarasi mara yanapohakikiwa ili kuendelea kukuza na kuchochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Minza Mjika.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, na ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Wakandarasi wengi na Wazabuni hufanya kazi hizi kwa kukopa fedha zao benki, lakini Serikali haiwalipi kwa wakati, na hivyo wengi wamefilisiwa mali zao, nyumba na magari vimeuzwa: -

Je, Serikali ina kauli gani kuhusu wazabuni hao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Wazabuni wengi madeni yao yameshahakikiwa na yana kama miezi sita na kuendelea, lakini bado hawajalipwa, na haya madeni tukumbuke ni ya muda mrefu kuanzia miaka miwili mpaka mitano. Mheshimiwa Waziri naomba aniambie kauli ya Serikali juu ya wakandarasi: -

Je, Serikali ina kauli gani juu ya wazabuni na wakandarasi hao, kwa sababu Serikali hailipi kwa wakati na wengi sasa wameshafilisiwa?

**MWENYEKITI:** Umeeleweka. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. kwanza...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri samahani, Mheshimiwa Waziri amesimama.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii, na nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa, vilevile nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia sana masuala ya wakandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili la wakandarasi siyo kwamba Serikali imeacha kulipa ama Serikali imekuwa hailipi. Kinachojitokeza ni kwamba kumekuwepo na malimbikizo ya madeni ya muda mrefu; na kama alivyosema, kwamba mengine ni ya miaka mitano. Mimi nimwambie tu kwamba siyo ya miaka mitano. Tena tuipongeze sana Serikali ya Awamu ya Sita kwa sababu imejitahidi sana kuyalipa madeni haya. Mengine yalikuwa na zaidi ya miaka hata saba, kuna madeni ambayo yamelipwa ya tangu mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, huwezi ukayapangia bajeti ya mwaka mmoja kwa sababu yataathiri shughuli nyingine za Serikali. Kinachotokea ni kwamba tumeendelea kuiongeza bajeti ya kulipa madeni hayo ya watoa huduma, wazabuni na wakandarasi. Utaweza kuona, mwaka juzi ilikuwa takribani shilingi bilioni 200, mwaka jana ilikuwa takribani bilioni 400, mwaka huu ilishafika takribani shilingi bilioni 600. Kwa sababu kulikuwa na malimbikizo, hiyo ndiyo iliyosababisha hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msisitizo wa Serikali ambao umetoka kabisa kwenye kauli ya Mheshimiwa Rais ni kuendelea kuongeza bajeti ya kulipa wazabuni hawa na wakandarasi na watoa huduma ili kutokuathiri shughuli za kiuchumi pamoja na mitaji yao, ambayo ni jambo la msingi sana katika uchumi wetu. Kwa hiyo, hilo limewekewa msisitizo, na bajeti inayofuata tutaendelea kuongeza ili kuweza kuhakikisha tunalipa sehemu kubwa na ikiwezekana tuyamalize yote.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa na majina mengi sana ya swali hili. Sasa kwa majibu tuliyoyapata hapa nitaruhusu maswali machache tu. Mheshimiwa Cecilia Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tupate majibu ya uhakika, kwamba kama wakandarasi wa nje wakipewa kazi kutoka nje ya nchi wakicheleweshewa malipo wanalipwa na riba, lakini wakandarasi wa ndani wakicheleweshewa malipo hawapewi riba hizo:-

Je, Serikali ina kauli gani kuhusiana na jambo hili?

**MWENYEKITI:** Naona Mheshimiwa Waziri amesimama tena. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna aina mbili za mikataba kuanzia mwanzo mikataba inapoingiwa. Kuna mikataba ya ndani na kuna mikataba ya nje. Mikataba ya nje wakandarasi wengi wa nje wanatumia *international standards* za mikataba na wakandarasi wa ndani wanatumia mikataba ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ndani ya mikataba ya sasa ambayo tunashawishi iliyo mingi, hata ya nje, ni kutokuwa na riba zinazohusiana na masuala ya kimikataba. Hivyo ndivyo tulivyoingia mikataba ya Wizara ya Kilimo ya masuala ya umwagiliaji kwa ajili ya kuepuka gharama zinazotokana na *mismatch* ya mapato na matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba hatutengenezi malimbikizo hayo ili kuhakikisha kwamba shughuli za wakandarasi haziathiriwi na malipo yanayotoka Serikalini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri nakushukuru. Kuna moja tu Mheshimiwa Mbunge alisimama tangu mwanzo, Mheshimiwa Esther Malleko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, tatizo la wakandarasi hawa kutokulipwa

limekuwa ni changamoto kubwa sana ambayo inasababisha mgogoro au inaichonganisha Serikali pamoja na wakandarasi. Je, Serikali haioni kuwa umuhimu wa kulifanya jambo hili kumalizika haraka kwa sababu wakandarasi wengi wa nchini wanafilisika kutokana na kutokulipwa madeni yao kwa wakati?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyojibu katika swali letu la msingi, kwamba madeni yote ambayo yamehakikiwa yatalipwa, na yote yaliyochelewa na yaliyowahi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutalipa deni hilo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata; Mheshimiwa Costantine John Kanyasu Mbunge wa Geita Mjini aulize swali lake.

Na. 67

**Posho za Nyumba na Majukumu kwa Wafanyakazi wa Chuo Kikuu Huria**

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU** aliuliza:-

Je, lini Serikali italipa posho za nyumba na majukumu kwa watumishi wa Chuo Kikuu Huria ambao hawajalipwa tangu mwaka 2020?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri unaendelea mwenyewe.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wizara ya Fedha imepokea na kuhakiki madeni ya watumishi wa Chuo Kikuu Huria Tanzania yenye thamani ya shilingi 5,430,613,831.00. Taratibu za

kushughulikia malipo ya madeni husika zinaendelea na yatalipwa katika hatua za utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka 2024/2025, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kanyasu swali la nyongeza.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba tufanye marekebisho. Ni kwamba hawajalipwa tangu mwaka 2012 na siyo mwaka 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadai wa madeni haya ni watumishi ambao tangu mwaka 2012 hawajalipwa, wengine wamestaafu, wengine wamefariki na wengine walishaacha kazi. Serikali kwa kutambua kwamba hawa ni watumishi wa umma, ukiacha kuwafanya wasiwe na *morale* ya kufanya kazi, haioni kwamba haiwatendei haki kwa miaka 14 kusubiri haki zao za msingi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Uhakiki kwa mujibu wa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri umefanyika mpaka 2022, leo ni 2024, utaratibu ule ule wa malimbikizo unaendelea. Ni kwamba Serikali haina mpango au haina utaratibu rasmi wa kuwalipa watumishi hawa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kanyasu, lakini kabla ya kujibu kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Kanyasu, siku zote anakuwa akifuatilia suala hili. Naomba maswali yake yote mawili nijibu kwa jibu moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mwaka huu wa fedha, 2024, madeni hayo ya watumishi wetu hao yatalipwa na bila kucheleweshwa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mhata.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna zoezi lingine la uhakiki ambalo linafanywa na benki yetu ya

NMB kwa wateja wao; zoezi ambalo limekuwa ghali na lina usumbufu mkubwa kwa wakulima wetu?

Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba kuna kila sababu ya benki hiyo ya *NMB* kuwafuata wakulima huko waliko badala ya zoezi ambalo sasa hivi wanafanya, kwamba wakulima wanatoka vijijini kwenda katika matawi yao na kusababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mhata kwamba, tumepokea ushauri wake na tunaenda kuufanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, naona Mheshimiwa Bulaya umesimama; unauliza swali? Maana ulishauliza swali la nyongeza moja. Sasa mtu mmoja maswali mawili kwa siku moja nadhani haitakuwa vizuri, umeshauliza.

Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea, tunakwenda Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, namwita Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu Mbunge wa Singida Mashariki sasa aulize swali lake.

Na. 68

**Malipo kwa Askari Waliopigana Vita ya Kagera**

**MHE. MIRAJI J. MTATURU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itawalipa Askari waliopigana Vita ya Kagera mwaka 1978?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa niaba yake Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Geophrey Pinda, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mtaturu kwa kweli kwa ufuatiliaji wake juu ya maisha ya wapiganaji hawa ambao walipigana Vita vya Kagera na kuendelea kufuatilia haki zao za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Ulinzi wa Taifa Na. 24 ya mwaka 1966 kifungu cha 20(1) na (2) kinampa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu mamlaka ya kuyaingiza Majeshi ya Ulinzi vitani; na kifungu cha 20(3) kinampa mamlaka ya kuyatoa vitani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo, Maafisa na Askari kutoka vyombo mbalimbali vya ulinzi na usalama walioshiriki Vita ya Kagera, walishiriki kwa mujibu wa sheria tajwa hapo juu wakiwa chini ya utawala wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Wanajeshi wote wastaafu waliopigana vita vya Kagera na waliostahili malipo ya viinua mgongo na pensheni wameendelea kulipwa kwa mujibu wa Sheria ya Pensheni na Viinua Mgongo ya Mwaka 1966, yakiwemo malipo ya ulemavu ya kila mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kundi ambalo lilishiriki vita na halikuwa limeajiriwa na vyombo vya ulinzi na usalama, baada ya vita kundi hilo lilipewa nafasi ya kujiunga katika vyombo vya ulinzi na usalama kwa kufuata taratibu. Kwa wale walioamua kutojiunga na wale waliokosa sifa katika kundi hilo walilipwa kifuta jasho na kurejeshwa makwao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtaturu, swali la nyongeza.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu ya maswali aliyonijibu, pamoja na hayo nina maswali mwili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunajua kwamba kazi waliyoifanya wapiganaji wa Vita ya Kagera ni kubwa na imetupa heshima kama Taifa. Swali la kwanza, je, Serikali ina mpango gani

katika kufanya sensa ya askari hawa ili kuwatambua na kuona namna ya kuwasaidia, ikiwemo kupitia pensheni kwa ajili ya kuboresha maisha yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili Serikali ina mpango gani ukizingatia kuna baadhi ya askari, kama aliyosema Mheshimiwa Waziri, kwamba walipata ulemavu wa kudumu na wengine maisha yao ni mabaya kwa sababu ya uwezo na wengine wamepata ulemavu wa kudumu? Je, Serikali ina mpango wa kuwakatia bima ya afya ili kuwawezesha kupata matibabu ya uhakika ili kuendelea kuishi vizuri?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, ni kwamba suala la uhakiki ni jambo endelevu kwetu kwa sababu wale wanajeshi pale baada ya vita vile wengine walitawanyika maeneo mbalimbali. Itakumbukwa kuwa hivi karibuni tulitoa tangazo kwamba wale wote ambao wana uhakika hawakuguswa na lile zoezi la kwanza kwenda kuripoti kwenye ofisi za washauri wa mgambo wa mikoa na wilaya zote hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wapo watu wa aina hiyo ili waweze kutambuliwa na haki zao kufanyiwa kazi, basi tunashauri waende wakaripoti huko kwa sababu ndiyo maeneo ambayo wanaweza wakahakikiwa na yapo karibu na maeneo wanayotoka badala ya kwenda mpaka Makao Makuu ya Jeshi, kwa sababu wanaosimamia wote ni washauri wa mgambo ambao wanatoka Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa chini ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la bima ya afya, kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi, watu hawa wameendelea kutibiwa chini ya Wizara hii ya Ulinzi. Hata hivyo wazo hili ulilolitoa ni jema sana, tunalichukua, litakwenda kuangaliwa na vyombo huko juu ya utaratibu. Nirudie tena kusema namshukuru sana kwa jinsi ambavyo amekuwa mfuatiliaji

wa maisha ya wapiganaji hawa waliojitoa mhanga wakati wa vita vya Kagera.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Benaya, swali la nyongeza.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Baadhi ya wapiganaji hawa ambao sio wengi wamekuwa wananung'unika siyo kwa kutolipwa kiinua mgongo, bali wanasema kwamba baada ya vita waliitwa na Mheshimiwa Baba wa Taifa katika uwanja wa vita na kuambiwa ahsante ya mdomo. Naungana na mwuliza swali. Je, hamna utaratibu mwingine wa kuhakiki askari hawa kama kuna uwezekano ili kuondoa manung'uniko hayo mengine kuwapa kitu chochote?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu jibu la msingi, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwanza ilitambua mchango wa hawa wapiganaji. Kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi, wale ambao hawakuwa kwenye mfumo wa jeshi walipata kifutajasho na wale ambao walikuwa kwenye muundo wa kijeshi wengi wameendelea kwanza kuhudumiwa mpaka leo. Majeruhi na wale walemavu waliolemaa kwa ajili ya vita hii, wameendelea kuhudumiwa na walipata kiinua mgongo pamoja na hiyo ahsante ya Baba wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiongozi yule aliposimama kusema ahsante, alikuwa anamaanisha kutoa shukrani kwa wanajeshi wale kujitoa muhanga kwa ajili ya kuipambania nchi yao. Huku nyuma watendaji ndio waliokwenda kusimamia sasa maslahi ya wale wapiganaji kwa maana niliyoitaja hapo juu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deogratius Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nami niulize swali dogo la nyongeza. Askari hawa waliopigana vita wamewekewa utaratibu wakipata changamoto za afya kwenda kutibiwa kwenye hospitali za kijeshi tu ilhali wengine wapo pembezoni, hawapo karibu na hospitali za jeshi. Je, Serikali

imeweka utaratibu gani sasa hivi ili kuwawezesha wanajeshi hao waliopigana vita kuweza kupata huduma za afya mahali walipo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri kama unaweza kulijibu lijibu, maana anaongelea bima ya afya kwa hao askari.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la nyongeza la Mheshimiwa mwuliza swali alizungumzia suala la bima ya afya, na Wizara tumelichukua kwenda kulichakata. Ni kweli kabisa wengi wapo mbali na maeneo ambayo hospitali za jeshi zinatoa huduma, tunalijua na wengi uwezo wao ni mdogo. Kwa hiyo, tumelichukua hili kwa thamani kubwa tutakwenda kuliangalia namna ya kulifanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mathayo Manyinyi.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kilio cha hawa askari waliopigana vita vya Idd Amin ni kikubwa sana, takribani nchi nzima, ni kwa nini Serikali isiunde Kamati ipite kila mkoa ionane nao, izungumze nao, ione namna ya kulimaliza tatizo hili kuliko kuwaacha wakaendelea kupiga kelele kwa namna wanavyoendelea kulia?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vyombo hivi vya ulinzi vina utaratibu wake unaofanana na hicho Mheshimiwa Mbunge alichokisema. Zipo Kamati za Jeshi ambazo zimeundwa zinatembea kila mkoa kwa kushirikiana na wale washauri wa mgambo wa mkoa kubainisha waathirika hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie kwamba chombo hiki kipo, na kipo kwenye muundo wetu wa Jeshi na hivyo basi, katika hali ya kawaida hakuna hata sababu ya

kuzalisha makundi mengine ya watu kwenda kule. Kama nilivyoeleza kwenye jibu langu kwamba ofisi zote za mikoa na wilaya ambako tuna washauri wa mgambo, tunawashauri sana hawa wapiganaji ambao kumbukumbu zao hazijatufikia waende pale ili kumbukumbu zao ziweze kuingia kwenye mfumo wetu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa kipindi cha maswali na nilete kwenu majina ya wageni ambao wametembelea ukumbi wetu wa Bunge leo.

Kwanza kabisa ni wageni Jukwaa la Spika, wageni 15 wa Mheshimiwa Spika, kutoka *Clouds Media Group* wakiongozwa na Ndugu Sheba Kussaga, Mkurugenzi wa Biashara na Uwekezaji, Ndugu Reuben Ndege, Mkuu wa Mikakati na Ubunifu, Ndugu Dotto Bahemu, Mkuu wa Vipindi *Clouds TV,* wengine ni Lilian Masuka, Zayrose Meja, Alex Kussaga, Mercyline Mwita, Phillios Lemi, Esha Kangele, Fidelis Hoza, Mariam Juma, Sakina Lyoka, Kerrwin Swai, Clara Manyinyi. Tunawakaribisha sana *Clouds Media* na tunatambua sana mchango wenu kwenye nchi hii. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kundi la pili ni wageni watatu wa Mheshimiwa Jerry Silaa, Mbunge, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Hawa ni wafanyabiashara na viongozi kutoka Jimbo la Ukonga Jijini Dar es Salaam; Ndugu Hamis Gea ambaye ni Mwenyekiti wa Mtaa wa Nyeburu, Kata ya Buyuni Jimbo la Ukonga, Ndugu Khamis Kombo Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa Mvuleni Kata ya Msongola – Ilala, Ndugu Emmanuel Sabuni, Katibu *Chanika Veteran Football Club* Jimbo la Ukonga, Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Kundi la pili ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Tunao wageni 20 wa Mheshimiwa Dkt. Dorothy Onesphoro Gwajima, Mbunge na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na

Makundi Maalum. Hawa ni wadau wa mashirika yasiyo ya kiserikali wa Sheria za Ulinzi wa Watoto, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni 40 wa Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge, hawa ni Madiwani. Kwanza msafara wao unaongozwa na Mkuu wa Wilaya, Mheshimiwa Onesmo Buswelu akiwa na Yasini Kibiriti ambaye ni Mwenyekiti wa Chama CCM Wilaya ya Tanganyika; vilevile yupo Mwenyekiti wa Halmashauri Mheshimiwa Mapengo, ameongozana na Madiwani wote kutoka Jimbo hili, karibuni sana katika Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kundi lingine ni mgeni wa Mheshimiwa Asha Abdullah Juma. Huyu ni mjukuu wake kutoka Zanzibar, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wageni nane wa Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga. Hiki ni kikundi cha *Clever Momies* kutoka Mkoa wa Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni watatu wa Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, wapiga kura wake kutoka Kalenga Mkoa wa Iringa, karibuni sana. Tuna mgeni wa Mheshimiwa Michael Constantine Mwakamo, kiongozi wa wafugaji na mpiga kura wake kutoka Jimbo la Kibaha Vijijini Mkoa wa Pwani. *(Makofi)*

Tuna kundi la wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wanafunzi 80 na walimu saba wa Shule ya Msingi Elisabetta Sanna, kutoka Mkoa wa Morogoro, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 31 na walimu watatu wa Shule ya Msingi Mwembesongo kutoka Mkoa wa Morogoro, karibuni sana Bungeni. Tuna Ndugu Paulina Dotto na Ndugu Modester Dotto Lubambi, hawa ni wakulima kutoka Jijini Mwanza, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo majina yaliyofika kwenye kiti kwa ajili ya kutambulishwa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mwongozo wa Spika.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Spika ataendelea na kikao na agenda inayofuata. *(Makofi)*

*Hapa Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nimesimama kwa Kanuni ya 76 kuomba mwongozo wako kwa jambo ambalo limetokea mapema leo.

Mheshimiwa Spika, wakati Waziri wa Fedha akijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecilia Paresso kwa kurejea swali namba 66 ambalo liliulizwa na Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata akitaka kujua ni kwa nini wakandarasi wa nje wanapocheleweshewa kulipwa fedha wanakuwa wanapewa riba, lakini wakandarasi wa ndani wanakuwa wanacheleweshewa lakini hawalipwi kwa riba. Sasa nimesimama kwa sababu majibu ya Waziri wa Fedha kwa kweli siyo tu kwamba yanasikitisha, lakini yanakatisha tamaa kwa wakandarasi wazawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Fedha anasema wanafanya wanayoyafanya ni kwa sababu wakandarasi wa nje wanapoingia mikataba ya kufanya kazi wanafuata *standard* za kimataifa, lakini wakandarasi wa ndani kwa taratibu zilizopo ndizo zinazowataka hata wakicheleweshewa wasilipwe na riba.

Mheshimiwa Spika, nafikiri kote tulipo tumekuwa tukipokea malalamiko mengi sana, wakandarasi wa ndani ambapo wanashindwa kulipwa kwa muda na wakati mwingine kama ilivyoelezwa kwa swali la msingi, inapita zaidi ya miaka mitano hata saba. Kuendelea na hao wakandarasi wa ndani, wanakuta wamekopa fedha na wakati mwingine wanatelekeza hata kazi au wanafanya kazi zao kwa kiwango cha chini sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nimesimama kuomba mwongozo wako, wakandarasi wetu wazawa lazima tuwatie moyo. Tumewasomesha na *the more* wanavyo-*practice* kama wanapewa kazi na wanalipwa kwa muda ina maana wanapata ujuzi zaidi. Kuna nchi tu za Afrika, kwa mfano *Egypt* kazi zao nyingi wanawapa wakandarasi wa ndani, sasa hawa wa kwetu tukiwa tunawa-*supress* hivyo hatutaweza kuwapata? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimesimama kuomba mwongozo wako kama itakupendeza uweze kuielekeza Serikali kama kuna *gap* ambalo linasababisha wakandarasi wa nje wawe *favoured* kufuata *standard* za nje, na wa ndani kama ni sheria au miongozo inasababisha wanakuwa *suppressed,* basi waweze kuleta yafanyike mabadiliko ili wakandarasi wa ndani na wenyewe waweze kupata hiyo fedha ama la wakandarasi wa ndani wawe wanalipwa kwa muda, yaani wakianza kazi basi wamaliziwe *hundred percent* ya malipo yao wafanye wamalize kuliko hivi wanavyopata *suppression. (Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naona anataka kutoa ufafanuzi.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, Serikali hatupingani na hoja aliyoileta Mbunge, kama utaona hivi juzi tu Bunge lililopita Serikali tulileta marekebisho ya sheria ili kuweza kuwabeba wakandarasi wazawa, na haya yalikuwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais kuweza kuhakikisha tunajenga uchumi wetu kwa kuwawezesha wakandarasi wazawa. Kwa hiyo, hicho alichokisema Mheshimiwa Mbunge na ambacho Bunge linataka ndicho na sisi Serikali tunachosisitiza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, rai yangu kwa wakandarasi Watanzania wenyewe wajiamini. Kwa mfano, tuna mikataba ambayo ni ya mkandarasi na Serikali na tuna mikataba ambayo ni ya mkandarasi mzawa na mkandarasi wa nje. Kinachotokea, moja ya wakandarasi wazawa wanaingia ile mikataba na wakandarasi wa nje ambayo haiweki ukomo huo.

Pili, sisi tunawalipa wakandarasi wa nje kwa wakati, lakini hawaweki ukomo wa wakandarasi wanapoingia hizo *subcontract*. Sisi tunawalipa wakandarasi wa nje kwa dola halafu wao wanapokwenda kulipwa, kwanza wanakuwa wamecheleweshewa, lakini la pili wanalipwa kwa *gap* ambalo ni kubwa sana ukilinganisha na kile tulichokilipa. Kwa hiyo, kwenye hili tumeweka kwenye sheria ambalo linahusisha mkandarasi wa nje pamoja na *subcontractor*. Sasa kwenye hili ambalo ni la ndani, hatukusema kwamba Serikali inawataka walipwe hivyo, tulisema ni zile *negotiation* za mikataba ambazo zinafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, sasa sisi ambacho tumekiweka tumeelekeza hata wale wa nje, tumeelekeza kuepuka kuweka vile vifungu ambavyo vinaweza vikaepukika kama ambavyo wamefanya wenzetu wa Wizara ya Kilimo kwenye miradi ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, lakini hii hoja ambayo ameitoa Mheshimiwa Mbunge tutaweka hiyo *fair treatment* kwa mikataba yote, na hata tumefanya kikao na Wizara ya Ujenzi, tumefanya kikao pia na Wizara ya Maji na wakandarasi wahusika, kwa sababu kwa kweli hili jambo linahitaji *capacity building* kwa sababu ya watu wetu pia wanapokwenda kwenye hizo *negotiation* zinazohusiana na kusaini mikataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumepokea hoja hiyo na tutakachofanya ni *capacity building* ya kuongea na wakandarasi wetu lakini kwa yale ambayo yanayohusisha wakandarasi wazawa na wakandarasi wa nje tumeweka kwenye sheria. Kwa sasa hivi mkandarasi mzawa anaruhusiwa kuchukua mradi wa aina yoyote ile na yeye ndio atafute wale atakaofanya nao kazi ili kuweza kuepusha hili ambalo lilikuwa linajitokeza.

Mheshimiwa Spika, tumeipokea hoja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko akiomba Mwongozo wa Spika kuhusu majibu ambayo yametolewa kwenye swali lililokuwa limeulizwa na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso kuhusu tofauti na yeye aliuliza kuhusu malipo lakini mwongozo ulivyoombwa hapa ni kwamba ule utofauti uliojibiwa kwamba wale wa nje mikataba yao ni ya Kimataifa, kwa hiyo, inawekewa riba malipo yakichelewa wakati wakandarasi wa ndani mikataba yao ni ya ndani haina masharti ya kudai riba malipo yakichelewa.

Sasa ameuliza kama hilo jambo linaruhusiwa ama haliruhusiwi? Kwa maana ya swali lililokuwa limeulizwa na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, majibu aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri ndiyo yanaruhusiwa, lakini hoja ya mwongozo wake sasa inaondoka kwenye kuomba Mwongozo wa Spika kwa sababu ni hoja ambayo haihusu jambo kama lililotokea kwamba linaruhusiwa ama haliruhusiwi, kwa sababu ukisimama kwenye mwongozo maana yake nitoe mwongozo kwamba hili jambo linaruhusiwa ama haliruhusiwi.

Waheshimiwa Wabunge, sasa hoja inayokuja ni kwamba katika yale majibu kumwonesha kwamba kuna hiyo tofauti ya malipo, haimaanishi kwamba yale majibu hayako sawasawa kwenye swali. Kwa hiyo, hapo tunaondoka kwamba kwa mwongozo ulioombwa hilo jambo linaruhusiwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hoja ya ziada aliyoisema Mheshimiwa Mbunge ni kwamba wale wakandarasi wa nje mikataba yao inaweka kifungu kinachohusu riba, wale wakandarasi wa ndani mikataba yao haiwekwi kifungu kinachohusu riba na huenda hilo ndilo linalosababisha wakandarasi wa ndani kucheleweshewa malipo kwa sababu wao hawana riba wakicheleweshewa.

Sasa ameeleza kwamba wakandarasi wa ndani pia wanakuwa wamekopa kama watu wengine na wanadaiwa na mambo kama hayo na pia mzunguko tu ule wa fedha kwa

sababu wao wasipolipwa inakuwa na changamoto kubwa. *(Makofi)*

Sasa kwenye ufafanuzi alioutoa Waziri ameutoa kwa upana mwingine tena, ameongeza na mambo mengine yale ambayo yanatokea kati ya wakandarasi wetu na wakandarasi wa nje wakiingia huko. Sasa tukiyaondoa haya, tukaenda kwenye hoja aliyoisema mwomba mwongozo ni kwamba Mheshimiwa Waziri amesema wameichukua.

Sasa ni kazi yetu kama Bunge kuendelea kuifuatilia. Sijajua vizuri kwa sababu ile sheria siko nayo hapa; kama ni sheria ndiyo inayosema wale wanaruhusiwa kuweka riba halafu hawa wa ndani hawaruhusiwi kuweka riba au ni utaratibu ambao Serikali imeuweka, lakini kwa maelezo aliyoyatoa Waziri ni kwamba Serikali inao utayari wa kubadili utaratibu huo ambao umewekwa.

Waheshimiwa Wabunge, sasa sijajua kama umewekwa kisheria ama vipi na sitaki kumwuliza mtu hapa kwa sababu hakuna mtu ambaye ameshika hiyo sheria, nami mwenyewe sijaishika hapa. Kama ni utaratibu wa Serikali, Mheshimiwa Waziri alivyosema, wao wanao utayari wa kubadili huo utaratibu, basi wataenda wabadilishe upande mwingine kama ni sheria imesema, hivyo basi ni kazi yetu kama Bunge kuibadili hiyo sheria ili kuweka mazingira ambayo wakandarasi wa ndani pia watafaidika kutokana na yale ambayo yanafanyika hapa nchini kama ambavyo yule wa nje anapata faida. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, Serikali iwatazame hawa ili wawe wanafanana ili yale aliyoyasema Mheshimiwa ya kuwapa uwezo yataweza kufanyika vizuri zaidi kwa maana ya kwamba ili wawe na uwezo, ni lazima wawe na fedha. Kama hawana fedha, wanalipwa hawa wengine, wao wanacheleweshewa, kunakuwa na changamoto kubwa hapo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, nadhani mmeshaelewa, Mheshimiwa Waziri amesema wanao utayari wa kubadili hilo. Kama ni wa kisheria, basi sheria tuibadili na Serikali italeta Muswada, na kama ni utaratibu ambao wameweka ndani ya Serikali, basi wataenda kubadili huo utaratibu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Ulinzi wa Mtoto wa Mwaka 2024 *[The Child Protection Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024]***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nilikuwa namwangalia hapo Mheshimiwa Waziri, mbona leo hamjavaa sare! Ama... *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, namwita Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima aje awasilishe hoja yake.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kabla ya kutoa maelezo kuhusu Muswada huu nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha sote kuwepo hapa kushiriki katika Mkutano huu wa Kumi na Sita wa Bunge la Kumi na Mbili; na kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Bungeni Muswada wa Marekebisho ya Sheria zinazohusu Ulinzi wa Mtoto wa mwaka 2024 *(The Child Protection Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024)*.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kuungana na Bunge lako Tukufu katika kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuiongoza nchi kwa umahiri na mafanikio makubwa katika nyanja zote, ikiwemo kuboresha Sekta ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii. Mengi yamefanyika chini ya uongozi wake na sote ni mashahidi wa jitihada anazochukua katika kuiongoza na kuitangaza nchi kimataifa kwa maendeleo ya Taifa na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa pongezi na shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Philip Isdory Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa *Dkt*. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Mbunge, Naibu Waziri Mkuu wa Tanzania na Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe mwenyewe, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zinazoliongoza Bunge hili. Nawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Spika, aidha, nawapongeza, Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, Mbunge, kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu); Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Mbunge, kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi - Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu); Mheshimiwa Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, Mbunge, kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria; Mheshimiwa Jenista Joackim Mhagama, Mbunge, kwa kuendelea kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Waziri wa Afya; Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana, Mbunge, kwa kuendelea kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii; Mheshimiwa Jerry William Silaa, Mbunge, kwa kuendelea kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Mheshimiwa Balozi Mahmoud Thabit Kombo, Mbunge, kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, Mbunge, kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na

Waheshimiwa Naibu Mawaziri wote walioaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais katika Wizara mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Hamza Said Johari kwa kuteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Vilevile, pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Mbunge, kwa kushinda uchaguzi wa Kiti cha Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Duniani, Kanda ya Afrika. Hongera sana Mheshimiwa.

Mheshimiwa Spika, kipekee naishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii inayoongozwa na Mwenyekiti Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge, na Makamu wake, Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mbunge, pamoja na Wajumbe wa Kamati hii kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia na kuchambua Muswada huu mbele ya kamati hiyo. Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri sana ya kuchambua Muswada huu kwa makini na kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu. Serikali imezingatia ushauri wa Kamati na imeleta Jedwali la Marekebisho kwa kuzingatia ipasavyo ushauri huo muhimu.

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwa Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mahakama ya Tanzania, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania na Wadau wa Maendeleo. Nayashukuru Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa ushirikiano waliotupatia katika mchakato mzima wa mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria zinazohusu ulinzi wa mtoto.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini kuwa Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Namhakikishia kuwa nitaendelea kutekeleza majukumu yangu kwa weledi, uaminifu na ufanisi mkubwa ili kuliletea Taifa letu maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria Zinazohusu Ulinzi wa Mtoto *(The Child Protection Laws (Miscellaneous Amendments)*

*Bill, 2024)* ambao uko mbele ya Bunge lako Tukufu, unapendekeza kufanya marekebisho ya sheria tatu ambazo ni:-

(1) Sheria ya Makosa ya Kimtandao, Sura ya 443;

(2) Sheria ya Mtoto, Sura ya 13; na

(3) Sheria ya Msaada wa Kisheria, Sura ya 21.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya Muswada huu yanalenga kuondoa upungufu uliojitokeza wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti ya Sheria hizo, ili kuimarisha ulinzi na maslahi bora ya mtoto. Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Nne, ambapo Sehemu ya Kwanza inahusu Masharti ya Utangulizi yanayojumuisha Jina la Muswada na namna ambavyo Sheria mbalimbali zinapendekezwa kurekebishwa katika sehemu zake.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Makosa ya Kimtandao, Sura ya 443 ambapo Kifungu cha Tatu kinapendeza kurekebishwa kwa kufuta na kuboresha baadhi ya tafsiri za misamiati kwenye Sheria na kuongeza misamiati mipya. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha tafsiri za misamiati iliyopo na kutoa ufafanuzi wa misamiati mipya ambayo itatumika katika Sheria husika.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 13 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuweka masharti yanayohusiana na makosa ya unyanyasaji na utumikishaji wa kingono kwa watoto kwa kutumia nyenzo za TEHAMA. Lengo la marekebisho haya ni kuwalinda watoto kutokana na kuwepo kwa ongezeko la matukio ya uhalifu wa kingono dhidi ya watoto kupitia nyenzo za TEHAMA zinazotumika kuwashawishi, kuwatishia au kuwaonesha watoto ponografia kwa lengo la kuwashawishi kushiriki katika matendo ya kingono.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 19 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza tafsiri ya msamiati "uhalifu dhidi ya binadamu" ambao umetumika katika Sheria, lakini haukuwa umetafsiriwa. Lengo la marekebisho haya ni kutoa ufafanuzi wa

msamiati kwa kurejea tafsiri ya msamiati huo kama ilivyoainishwa katika Mkataba wa Roma wa Mahakama ya Kimataifa ya Jinai na kurahisisha utekelezaji wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, kifungu kipya cha 19(A) kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti yanayozuia mtu au mfumo wa kompyuta kutekeleza kitendo cha kigaidi na kuweka adhabu kwa mtu anayekiuka masharti hayo. Lengo la marekebisho haya ni kudhibiti na kuzuia vitendo vya kigaidi vinavyoweza kutendeka kwa njia ya kompyuta au mifumo ya kompyuta.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 49 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuweka masharti yanayohusu adhabu kwenye makosa yanayotendwa na kampuni au taasisi. Lengo la marekebisho haya ni kuainisha namna ya kushughulikia uhalifu unaotendwa na kampuni au taasisi na kuhakikisha kuwa, Wakurugenzi wa Kampuni wanawajibika kwa uhalifu wa kimtandao unaofanywa na kampuni au taasisi wanazozisimamia.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 50 kinapendekezwa kurekebishwa ili mamlaka ya kufifilisha makosa yasihusishe makosa ya udhalilishaji wa kingono kwa watoto. Marekebisho haya yanalenga kufanya adhabu kwa makosa ya udhalilishaji wa kingono dhidi ya watoto, itolewe na mahakama pekee kutokana na uzito wa makosa hayo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Mtoto, Sura ya 13, ambapo kifungu cha 3 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta baadhi ya misamiati na kuindika upya, kurekebisha na kuongeza baadhi ya tafsiri za misamiati. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha tafsiri za misamiati inayotumika katika Sheria hiyo ili kuendana na muktadha uliokusudiwa na kutoa ufafanuzi wa misamiati ambayo haikuwa imetafsiriwa ili kuwezesha utekelezaji wa Sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, aidha, kifungu cha 14 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuainisha ukomo wa chini wa adhabu. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kwamba adhabu inayotolewa inaendana na ukubwa wa kosa husika.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 22 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa dhana ya Shule za Maadilisho na badala yake kuweka dhana iliyokusudiwa katika kifungu hicho ambayo ni Makao ya Malezi ya Watoto waliotoroka kutoka sehemu waliyowekwa kwa amri ya Mahakama ya uangalizi baada ya kuondolewa kwenye familia zao kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo uhanga wa ukatili, mazingira hatarishi.

Mheshimiwa Spika, vifungu vya 32 na 53 vinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kurekebisha makosa ya kiuandishi na kuondoa masharti yanayojirudia katika Sheria kwa kuwa, Mamlaka ya kutengeneza Kanuni kuhusu malezi ya kambo tayari yameainishwa katika kifungu cha 157. Marekebisho mengine katika kifungu cha 53, yanalenga kurahisisha utaratibu wa uwasilishaji wa maombi ya malezi ya kambo kwa kuondoa mlolongo mrefu uliopo sasa.

Mheshimiwa Spika, aidha, kifungu cha 36 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza sharti la ulazima kwa Mahakama kuzingatia taarifa ya uchunguzi wa kitaalamu kutoka kwa Afisa Ustawi wa Jamii wakati wa kutoa amri ya kugharamia vipimo vya vinasaba. Lengo la marekebisho haya ni kuiwezesha Mahakama kufikia uamuzi wa haki na unaotekelezeka.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 45 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka masharti yanayomtaka Afisa Ustawi wa Jamii kuandaa Taarifa ya Uchunguzi kwa ajili ya kutumika Mahakamani wakati wa mashauri yanayohusu malezi, matunzo, uangalizi na haki ya kumwona mtoto. Lengo la marekebisho haya ni kuisaidia Mahakama kupata taarifa ambazo zitaiwezesha kutoa uamuzi wa haki na unaozingatia maslahi bora ya mtoto.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 54 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kubainisha Mamlaka za Mahakama katika kushughulikia mashauri ya kuasili watoto. Aidha, Mahakama ya watoto inaongezwa miongoni mwa Mahakama zitakazoshughulikia mashauri hayo ili kuongeza ufanisi na kupunguza mlundikano wa mashauri katika Mahakama nyingine. Kifungu cha 55 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuondoa masharti yaliyojirudia katika kifungu kingine.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo yaliyokuwa yanapendekezwa kwenye kifungu cha 56 yanapendekezwa kuondolewa kupitia Jedwali la Marekebisho la Serikali ili marekebisho katika Kifungu hicho yafanyiwe kazi zaidi kwa lengo la kuboreshwa na Serikali kabla ya kuwasilishwa tena Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 60 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuiondolea Mahakama mamlaka ya kuruhusu mtoto kusafirishwa nje ya nchi wakati wa utoaji wa amri ya mpito kabla ya kukamilika kwa mchakato wa kuasili mtoto. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha ulinzi kwa mtoto anayekusudiwa kuasiliwa kabla ya Mahakama kutoa amri ya kuasili.

Mheshimiwa Spika, kifungu kipya cha 71(A) kinapendekezwa kuongezwa kwa lengo la kuipa Mahakama mamlaka ya kufuta amri ya kuasili kwa manufaa ya mtoto baada ya kupokea maombi kutoka kwa mzazi, mlezi au ndugu wa mtoto aliyeasiliwa au mtu mwingine yeyote mwenye maslahi.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo katika kifungu cha 74 kilichokuwa na lengo la kupunguza muda unaotakiwa kwa mwombaji wa kuasili mtoto asiye Mtanzania kukaa nchini kutoka miaka mitatu hadi miaka miwili mfululizo, yanapendekezwa kuondolewa kupitia Jedwali la Marekebisho ya Serikali baada ya majadiliano na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kwa lengo la kuimarisha ulinzi na ustawi wa Watoto wa Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, aidha, marekebisho mengine katika kifungu hicho yanayopendekeza kuongeza muda wa kumlea mtoto kabla ya kumwasili kutoka miezi mitatu hadi miezi sita, yanapendekezwa kubaki katika Muswada na kupitishwa na Bunge lako Tukufu. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha na kurahisisha taratibu za kuasili na kulinda maslahi bora ya mtoto.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 94 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kufuata takwa linaloelekeza kwamba, Halmashauri pale inaposhindwa kumpata mzazi au ndugu wa mtoto aliyepotea au kutelekezwa iwasilishe suala hilo kwa Afisa Ustawi wa Jamii. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa

mkanganyiko, kwani Mtendaji wa Masuala ya Watoto katika Halmashauri ni Afisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri husika. Kifungu cha 96 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kurekebisha makosa ya kiuandishi katika masharti ya kifungu hicho kwa lengo la kupata mantiki iliyokusudiwa katika kifungu husika.

Mheshimiwa Spika, kifungu kipya cha 96(A) kinapendekezwa kuongezwa kwa ajili ya kuanzisha na kurasimisha Mabaraza ya Watoto katika ngazi ya Kijiji, Kata, Wilaya, Mkoa na ngazi ya Taifa. Lengo la marekebisho haya ni kuwa na majukwaa yanayowafikia watoto na kujua changamoto zinazowakabili ili kuweza kuwalinda na matukio ya unyanyasaji na uhalifu katika jamii.

Mheshimiwa Spika, Kichwa cha Habari cha Sehemu ya Tisa kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuakisi maudhui ya masharti yaliyomo chini ya sehemu hiyo. Kifungu cha 97 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuanzisha na kutambua Mahakama za Watoto katika kila Wilaya.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho haya ni kuwezesha utoaji haki kwa watoto kwa wakati na kuboresha ustawi na maslahi ya watoto. Vilevile, marekebisho haya yanalenga kuzingatia mikataba ya Kimataifa kuhusu haki za watoto inayoelekeza nchi wanachama kuwa na Mahakama za Watoto, kwa ajili ya kusikiliza mashauri ya watoto.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 99 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuondoa maneno "*next of kin*" katika masharti ya kifungu hicho ambayo kwa sasa hayatumiki na badala yake kuweka maneno "*next friend*" ambayo ndiyo yanatumika. Kifungu cha 100 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha masharti ya kifungu hicho ili kuendana na marekebisho yanayopendekezwa katika Muswada huu. Pia, kifungu hicho kinapendekeza marekebisho endapo Mahakama itabaini kuwa mhusika katika shauri sio mtoto, basi badala ya kuendelea na shauri kama ilivyo sasa, zitapaswa kuwasilisha shauri husika katika Mahakama yenye mamlaka.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 102 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kumlinda mtoto dhidi ya uhalifu kwa

kutoruhusu mtoto kuchangamana na wahalifu ambao ni watu wazima hata kama ni ndugu. Kifungu cha 103 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka masharti kwa Mahakama kuhusu kuahirisha kesi zinazowahusu watoto wanaotuhumiwa kutenda makosa ya mauaji. Lengo la marekebisho haya ni kuharakisha usikilizwaji wa mashauri ya watoto na kuwalinda watoto hao dhidi ya kujifunza tabia za uhalifu gerezani.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya marekebisho katika kifungu cha 107 ambayo kupitia Jedwali la Marekebisho ya Serikali yanapendekezwa kuhamishiwa katika Kifungu Kipya cha 101(A) yanalenga kuhakikisha kwamba mtoto anarekebishwa nje ya Mfumo wa Mahakama kwa makosa madogo ili kumsaidia kubadilika kitabia kupitia mifumo ya jamii iliyopo zikiwemo Ofisi za Ustawi wa Jamii na vilevile kupunguza muda na gharama za uendeshaji wa kesi za watoto.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 115 kinapendekezwa kurekebisha kwa lengo la kumlinda mtoto ambaye amekinzana na Sheria kwa kuhakikisha uwepo wa Afisa Ustawi wa Jamii katika shauri linalohusisha mtoto. Kwa sasa, masharti haya yapo kwa Mahakama za Watoto pekee na siyo katika Mahakama za kawaida. Aidha, marekebisho haya pia, yanampa Jaji Mkuu mamlaka ya kutengeneza Kanuni zitakazoainisha utaratibu wa kuwadodosa watoto Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, Kichwa cha Habari cha Sehemu Ndogo ya (c) ya Sehemu ya Tisa kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuakisi maudhui yaliyo chini ya Sehemu hiyo. Kifungu cha 130 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuweka utaratibu sahihi wa uwasilishaji wa rufaa kutoka Mahakama ya Mtoto kwenda Mahakama Kuu na kuondoa utata katika masharti hayo.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 151 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuweka mpangilio mzuri wa vifungu ndani ya Sheria kwa kuondoa masharti yanayohusiana na makao ya watoto ambayo tayari yameainishwa na kubakiza masuala ya vituo vya kulea watoto wadogo na watoto wachanga katika kifungu hiki. Kifungu cha 155 kinapendekezwa kurekebishwa kwa

lengo la kuondoa kasoro za kiuchapaji na kuwezesha utekelezaji wa masharti ya kifungu hicho kwa kuwa, kifungu hicho kinatoa cheti cha usajili na siyo leseni.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 157 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuongeza maeneo ambayo Waziri anaweza kutengeneza Kanuni. Lengo la marekebisho hayo ni kuwezesha utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hiyo. Kifungu cha 158 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kupanua wigo wa makosa ya ukatili wa kingono dhidi ya watoto. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ulinzi kwa watoto dhidi ya uhalifu wa kingono ambao kwa sasa unaongezeka kwa kasi, hasa kutokana na kukua kwa teknolojia na utandawazi. Kifungu cha 158(A) kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kukifanya kifungu hiki kuwa na nguvu dhidi ya masharti ya sheria nyingine kuhusu makosa ya ukeketaji wa watoto na kutoa fidia kwa wahanga wa makosa hayo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika ya Sheria ya Msaada wa Kisheria, Sura ya 21, ambapo Kifungu cha 33 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumpa Hakimu Mfawidhi mamlaka ya kumwelekeza Wakili kumwakilisha mtoto ambaye ni mshtakiwa inapothibitika kuwa mshtakiwa anapaswa kupata msaada wa Kisheria. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha mtoto ambaye ni mshtakiwa anapata uwakilishi wa Kisheria.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya na kwa mara nyingine tena, naomba Bunge lako Tukufu liujadili Muswada wa Sheria Zinazohusu Ulinzi wa Mtoto wa Mwaka huu 2024 na kuupitisha katika hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Pili na ya Tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe Sehemu ya Sheria za Nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(maofi)*

**MAELEZO YA MHESHIMIWA DKT. DOROTHY GWAJIMA (MB), WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM AKIWASILISHA MUSWADA WA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI ZINAZOHUSU ULINZI WA MTOTO *(THE CHILD PROTECTION LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) BILL, 2024)* KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**Mheshimiwa Spika**, Awali ya yote, naomba kabla ya kutoa maelezo kuhusu Muswada huu nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai na afya njema; na kutuwezesha sote kuwepo hapa kushiriki katika Mkutano huu wa Kumi na Sita wa Bunge la Kumi na Mbili, na kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha Bungeni Muswada wa Marekebisho ya Sheria Zinazohusu Ulinzi wa Mtoto wa Mwaka 2024 *(The Child Protection Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024)*.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kutumia fursa hii kuungana na Bunge lako Tukufu katika kumpongeza kwa dhati **Mhe. *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kuendelea kuiongoza Nchi kwa umahiri na mafanikio makubwa katika nyanja zote, ikiwemo kuboresha Sekta ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii. Mengi yamefanyika chini ya uongozi wake na sote ni mashahidi wa jitihada anazochukua katika kuiongoza na kuitangaza Nchi kimataifa kwa maendeleo ya Taifa na wananchi kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Napenda pia kutoa pongezi na shukrani za dhati kwa Mheshimiwa *Dkt.* Philip Isdory Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mhe. *Dkt.* Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. *Dkt.* Doto Mashaka Biteko (Mb), Naibu Waziri Mkuu wa Tanzania na Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe mwenyewe, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zinazoliongoza Bunge hili. Ninawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuisimamia Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, niwapongeze, Mhe. William Vangimembe Lukuvi (Mb) kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb) kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi - Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu), Mhe. Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb) kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Jenista Joackim Mhagama (Mb) kwa kuendelea kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Waziri wa Afya, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana (Mb) kwa kuendelea kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Jerry William Silaa (Mb), kwa kuendelea kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Balozi Mahmoud Thabit Kombo (Mb) kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mhe.Deogratius John Ndejembi (Mb) kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Waziri wa Ardhi,Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Waheshimiwa Manaibu Waziri wote walioaminiwa na kuteuliwa na Mhe. Rais katika Wizara mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** Nampongeza Mhe. Hamza Said Johari kwa kuteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali vilevile pongezi nyingi kwa Mhe. Dkt. Faustine Ndugulile (Mb.) kwa kushinda uchaguzi wa kiti cha Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Duniani – Kanda ya Afrika, hongera sana Mheshimiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kipekee niishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii inayoongozwa na Mwenyekiti **Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq (Mb)** na Makamu wake, **Mheshimiwa Riziki Said Lulida (Mb)** pamoja na Wajumbe wa Kamati hii kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa

kupitia na kuchambua Muswada huu mbele ya Kamati hiyo. Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri sana ya kuchambua Muswada huu kwa makini na kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu. Serikali imezingatia ushauri wa Kamati na imeleta Jedwali la Marekebisho kwa kuzingatia ipasavyo ushauri huo muhimu.

**Mheshimiwa Spika,** Ninatoa shukrani zangu za dhati kwa Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mahakama ya Tanzania, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Wadau wa Maendeleo na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa ushirikiano waliotupatia katika mchakato mzima wa mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria zinazohusu ulinzi wa mtoto.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa heshima na taadhima, ninaomba nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini kuwa Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Ninamhakikishia kuwa, nitaendelea kutekeleza majukumu yangu kwa weledi, uaminifu na ufanisi mkubwa ili kuliletea Taifa letu maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Muswada wa Sheria zinazohusu Ulinzi wa Mtoto (The Child Protection Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024) ambao uko mbele ya Bunge lako Tukufu, unapendekeza kufanya marekebisho ya sheria tatu ambazo ni-

1. Sheria ya Makosa ya Kimtandao Sura ya 443;
2. Sheria ya Mtoto, Sura ya 13; na
3. Sheria ya Msaada wa Kisheria, Sura ya 21.

**Mheshimiwa Spika,** Madhumuni ya Muswada huu yanalenga kuondoa upungufu uliojitokeza wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti ya sheria hizo ili kuimarisha ulinzi na maslahi bora ya mtoto.

**Mheshimiwa Spika,** Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Nne, ambapo Sehemu ya Kwanza inahusu Masharti ya Utangulizi yanayojumuisha Jina la Muswada na namna ambavyo Sheria mbalimbali zinapendekezwa kurekebishwa katika Sehemu zake.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Makosa ya Kimtandao, Sura ya 443 ambapo kifungu cha 3 kinapendeza kurekebishwa kwa kufuta na kuboresha baadhi ya tafsiri za misamiati kwenye Sheria na kuongeza misamiati mipya. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha tafsiri za misamiati iliyopo, na kutoa ufafanuzi wa misamiati mipya ambayo itatumika katika Sheria husika.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 13 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuweka masharti yanayohusiana na makosa ya unyanyasaji na utumikishaji wa kingono kwa watoto kwa kutumia nyenzo za TEHAMA. Lengo la marekebisho haya ni kuwalinda watoto kutokana na kuwepo kwa ongezeko la matukio ya uhalifu wa kingono dhidi ya watoto kupitia nyenzo za TEHAMA zinazotumika kuwashawishi, kuwatishia au kuwaonesha watoto ponografia kwa lengo la kuwashawishi kushiriki katika matendo ya kingono.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 19 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza tafsiri ya msamiati "uhalifu dhidi ya binadamu" ambao umetumika katika Sheria lakini haukuwa umetafsiriwa. Lengo la marekebisho haya ni kutoa ufafanuzi wa msamiati kwa kurejea tafsiri ya msamiati huo kama ilivyoainishwa katika Mkataba wa Roma wa Mahakama ya Kimataifa ya Jinai na kurahisisha utekelezaji wa Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu kipya cha 19A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti yanayozuia mtu au mfumo wa kompyuta kutekeleza kitendo cha kigaidi na kuweka adhabu kwa mtu anayekiuka masharti hayo. Lengo la marekebisho haya ni kudhibiti na kuzuia vitendo vya kigaidi vinavyoweza kutendeka kwa njia ya kompyuta au mifumo ya kompyuta.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 49 kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuweka masharti yanayohusu adhabu kwenye makosa yanayotendwa na kampuni au taasisi. Lengo la marekebisho haya ni kuainisha namna ya kushughulikia uhalifu unaotendwa na kampuni au taasisi na kuhakikisha kuwa

wakurugenzi wa kampuni wanawajibika kwa uhalifu wa kimtandao unaofanywa na kampuni au taasisi wanazozisimamia.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 50 kinapendekezwa kurekebishwa ili mamlaka ya kufifilisha makosa yasihusishe makosa ya udhalilishaji wa kingono kwa watoto. Marekebisho haya yanalenga kufanya adhabu kwa makosa ya udhalilishaji wa kingono dhidi ya watoto itolewe na mahakama pekee kutokana na uzito wa makosa hayo.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Mtoto, Sura ya 13, ambapo kifungu cha 3 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta baadhi ya misamiati na kuindika upya, kurekebisha na kuongeza baadhi ya tafsiri za misamiati. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha tafsiri za misamiati inayotumika katika sheria hiyo ili kuendana na muktadha uliokusudiwa na kutoa ufafanuzi wa misamiati ambayo haikuwa imetafsiriwa ili kuwezesha utekelezaji wa Sheria hiyo. Aidha, Kifungu cha 14 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuainisha ukomo wa chini wa adhabu. Lengo la marekebisho hayo ni kuhakikisha kwamba adhabu inayotolewa inaendana na ukubwa wa kosa husika.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 22 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuondoa dhana ya Shule za Maadilisho na badala yake kuweka dhana iliyokusudiwa katika kifungu hicho ambayo ni Makao ya Malezi ya Watoto waliotoroka kutoka sehemu waliyowekwa kwa amri ya mahakama ya uangalizi baada ya kuondolewa kwenye familia zao kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo uhanga wa ukatili, mazingira hatarishi.

**Mheshimiwa Spika,** Vifungu vya 32 na 53 vinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kurekebisha makosa ya kiuandishi na kuondoa masharti yanayojirudia katika Sheria kwa kuwa mamlaka ya kutengeneza kanuni kuhusu malezi ya kambo tayari yameainishwa katika kifungu cha 157. Marekebisho mengine katika kifungu cha 53 yanalenga kurahisisha utaratibu wa uwasilishaji wa maombi ya malezi ya kambo kwa kuondoa mlolongo mrefu uliopo sasa.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha, kifungu cha 36 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza sharti la ulazima kwa mahakama kuzingatia taarifa ya uchunguzi wa kitaalamu kutoka kwa afisa ustawi wa jamii wakati wa kutoa amri ya kugharamia vipimo vya vinasaba. Lengo la marekebisho haya ni kuiwezesha mahakama kufikia uamuzi wa haki na unaotekelezeka.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 45 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka masharti yanayomtaka afisa ustawi wa jamii kuandaa taarifa ya uchunguzi kwa ajili ya kutumika mahakamani wakati wa mashauri yanayohusu malezi, matunzo, uangalizi na haki ya kumuona mtoto. Lengo la marekebisho haya ni kuisaidia mahakama kupata taarifa ambazo zitaiwezesha kutoa uamuzi wa haki na unaozingatia maslahi bora ya mtoto. Kifungu cha 54 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kubainisha mamlaka za mahakama katika kushughulikia mashauri ya kuasili watoto. Aidha, mahakama ya watoto inaongezwa miongoni mwa mahakama zitakazoshughulikia mashauri hayo ili kuongeza ufanisi na kupunguza mlundikano wa mashauri katika mahakama nyingine. Kifungu cha 55 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuondoa masharti yaliyojirudia katika kifungu kingine.

**Mheshimiwa Spika**, Mapendekezo yaliyokuwa yanapendekezwa kwenye kifungu cha 56 yanapendekezwa kuondolewa kupitia Jedwali la Marekebisho la Serikali ili marekebisho katika kifungu hicho yafanyiwe kazi zaidi kwa lengo la kuboreshwa na Serikali kabla ya kuwasilishwa tena Bungeni. Kifungu cha 60 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuiondolea mahakama mamlaka ya kuruhusu mtoto kusafirishwa nje ya nchi wakati wa utoaji wa amri ya mpito kabla ya kukamilika kwa mchakato wa kuasili mtoto. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha ulinzi kwa mtoto anayekusudiwa kuasiliwa kabla ya mahakama kutoa amri ya kuasili.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu kipya cha 71A kinapendekezwa kuongezwa kwa lengo la kuipa mahakama mamlaka ya kufuta amri ya kuasili kwa manufaa ya mtoto baada ya kupokea maombi kutoka kwa mzazi, mlezi au ndugu wa mtoto aliyeasiliwa au mtu mwingine yeyote mwenye maslahi.

**Mheshimiwa Spika,** mapendekezo katika kifungu cha 74 kilichokuwa na lengo la kupunguza muda unaotakiwa kwa mwombaji wa kuasili mtoto asiye mtanzania kukaa nchini kutoka miaka mitatu hadi miaka miwili mfululizo yanapendekezwa kuondolewa kupitia Jedwali la Marekebisho ya Serikali baada ya majadiliano na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kwa lengo la kuimarisha ulinzi na ustawi wa watoto wa kitanzania. Aidha, marekebisho mengine katika kifungu hicho yanayopendekeza kuongeza muda wa kumlea mtoto kabla ya kumuasili kutoka miezi mitatu hadi miezi sita yanapendekezwa kubaki katika Muswada na kupitishwa na Bunge lako Tukufu. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha na kurahisisha taratibu za kuasili na kulinda maslahi bora ya mtoto.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 94 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta takwa linaloelekeza kwamba halmashauri pale inaposhindwa kumpata mzazi au ndugu wa mtoto aliyepotea au kutelekezwa iwasilishe suala hilo kwa afisa ustawi wa jamii. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa mkanganyiko kwani mtendaji wa masuala ya watoto katika halmashauri ni afisa ustawi wa jamii wa halmashauri husika. Kifungu cha 96 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kurekebisha makosa ya kiuandishi katika masharti ya kifungu hicho kwa lengo la kupata mantiki iliyokusudiwa katika kifungu husika.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu kipya cha 96A kinapendekezwa kuongezwa kwa ajili ya kuanzisha na kurasimisha mabaraza ya watoto katika ngazi ya Kijiji, Kata, Wilaya, Mkoa na ngazi ya Taifa. Lengo la marekebisho haya ni kuwa na majukwaa yanayowafikia watoto na kujua changamoto zinazowakabili ili kuweza kuwalinda na matukio ya unyanyasaji na uhalifu katika jamii.

**Mheshimiwa Spika,** Kichwa cha habari cha Sehemu ya TISA kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuakisi maudhui ya masharti yaliyomo chini ya Sehemu hiyo. Kifungu cha 97 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuanzisha na kutambua Mahakama za Watoto katika kila wilaya. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha utoaji haki kwa watoto kwa wakati na kuboresha ustawi na maslahi ya watoto. Vilevile, marekebisho haya yanalenga kuzingatia mikataba ya kimataifa kuhusu haki za

watoto inayoelekeza nchi wanachama kuwa na Mahakama za Watoto kwa ajili ya kusikiliza mashauri ya watoto.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 99 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuondoa maneno "next of kin" katika masharti ya kifungu hicho ambayo kwa sasa hayatumiki na badala yake kuweka maneno "next friend" ambayo ndiyo yanatumika. Kifungu cha 100 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha masharti ya kifungu hicho ili kuendana na marekebisho yanayopendekezwa katika Muswada huu. Na pia kifungu hicho kinapendekeza marekebisho endapo mahakama itabaini kuwa muhusika katika shauri si mtoto, basi badala ya kuendelea na shauri kama ilivyo sasa, zitapaswa kuwasilisha shauri husika katika mahakama yenye mamlaka.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 102 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kumlinda mtoto dhidi ya uhalifu kwa kutoruhusu mtoto kuchangamana na wahalifu ambao ni watu wazima hata kama ni ndugu. Kifungu cha 103 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka masharti kwa mahakama kuhusu kuahirisha kesi zinazowahusu watoto wanaotuhumiwa kutenda makosa ya mauaji. Lengo la marekebisho haya ni kuharakisha usikilizwaji wa mashauri ya watoto na kuwalinda watoto hao dhidi ya kujifunza tabia za uhalifu gerezani.

**Mheshimiwa Spika**, Mapendekezo ya marekebisho katika kifungu cha 107 ambayo kupitia Jedwali la Marekebisho ya Serikali yanapendekezwa kuhamishiwa katika kifungu kipya cha 101A yanalenga kuhakikisha kwamba mtoto anarekebishwa nje ya mfumo wa mahakama kwa makosa madogo ili kumsaidia kubadilika kitabia kupitia mifumo ya jamii iliyopo zikiwemo ofisi za ustawi wa jamii na vilevile kupunguza muda na gharama za uendeshaji wa kesi za watoto.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 115 kinapendekezwa kurekebisha kwa lengo la kumlinda mtoto ambaye amekinzana na sheria kwa kuhakikisha uwepo wa afisa ustawi wa jamii katika shauri linalohusisha mtoto. Kwa sasa masharti haya yapo kwa mahakama za watoto pekee na si katika mahakama za kawaida. Aidha, marekebisho haya pia yanampa Jaji Mkuu mamlaka ya

kutengeneza kanuni zitakazoainisha utaratibu wa kuwadodosa watoto mahakamani.

**Mheshimiwa Spika**, Kichwa cha habari cha Sehemu Ndogo ya (c) ya Sehemu ya Tisa kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuakisi maudhui yaliyo chini ya Sehemu hiyo. Kifungu cha 130 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuweka utaratibu sahihi wa uwasilishaji wa rufaa kutoka mahakama ya mtoto kwenda mahakama kuu na kuondoa utata katika masharti hayo.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 151 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuweka mpangilio mzuri wa vifungu ndani ya Sheria kwa kuondoa masharti yanayohusiana na makao ya watoto ambayo tayari yameainishwa na kubakiza masuala ya vituo vya kulea watoto wadogo na watoto wachanga katika kifungu hiki. Kifungu cha 155 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuondoa kasoro za kiuchapaji na kuwezesha utekelezaji wa masharti ya kifungu hicho kwa kuwa kifungu hicho kinatoa cheti cha usajili na siyo leseni.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 157 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuongeza maeneo ambayo Waziri anaweza kutengeneza kanuni. Lengo la marekebisho hayo ni kuwezesha utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hiyo. Kifungu cha 158 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kupanua wigo wa makosa ya ukatili wa kingono dhidi ya watoto. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ulinzi kwa watoto dhidi ya uhalifu wa kingono ambao kwa sasa unaongezeka kwa kasi hasa kutokana na kukua kwa teknolojia na utandawazi. Kifungu cha 158A kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kukifanya kifungu hiki kuwa na nguvu dhidi ya masharti ya sheria nyingine kuhusu makosa ya ukeketaji wa watoto na kutoa fidia kwa wahanga wa makosa hayo.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika ya Sheria ya Msaada wa Kisheria, Sura ya 21, ambapo kifungu cha 33 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumpa hakimu mfawidhi mamlaka ya kumuelekeza Wakili kumwakilisha mtoto ambaye ni mshtakiwa inapothibitika kuwa mshtakiwa anapaswa kupata msaada wa

kisheria. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha mtoto ambaye ni mshtakiwa anapata uwakilishi wa kisheria.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo haya na kwa mara nyingine tena, ninaomba Bunge lako tukufu liujadili Muswada wa Sheria Zinazohusu Ulinzi wa Mtoto (The Child Protection Laws (Miscellaneous Amendments) Bill,2024) na kuupitisha katika hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Pili na ya Tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya Sheria za Nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, NAOMBA KUTOA HOJA.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha hoja hii.

Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ili aje awasilishe hoja ya Kamati. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Mbunge wa Tarime Mjini, Mheshimiwa Michael Kembaki.

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niwasilishe Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii. Naomba taarifa hii yote ya kamati iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, leo 30 Agosti, 2024 naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Ulinzi wa Mtoto wa Mwaka 2024 *(the Child Protection Laws (Miscellenaous Amendments Bill, 2024)* kwa

mujibu wa Kanuni ya 99 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Ulinzi wa Mtoto wa Mwaka 2024, ulisomwa Bungeni kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Kanuni wa 15 katika Kikao cha 56 kwenye Bunge la 12, tarehe 28 Juni, 2024 kwa mujibu wa Kanuni ya 93 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136 (14) na Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nne ya Kanuni za Kudumu za Bunge, uliuelekeza Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa kwa kina. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati imeuchambua na kuujadili Muswada huu kwa kuzingatia, Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati imeuchambua na kuujadili Muswada huu kwa kuzingatia Katiba na Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, namna uchambuzi wa Muswada ulivyofanyika. Hatua za kuufanya Muswada huu zilianza kwa maandalizi mbalimbali ya kiutendaji yaliyofanywa na Sekretarieti kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji bora wa shughuli za Kamati. Maelezo ya uchambuzi wa Muswada ulifanywa na kuwasilishwa kwenye Kamati na Sekretarieti ya Bunge kwa mujibu wa Kanuni 24(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Hatua hii ilijenga msingi wa utekelezaji wa kazi za Kamati kuhusiana na Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana na Serikali tarehe 14 Agosti, 2024 ili kupokea maelezo ya Mheshimiwa Dorothy Onesphoro Gwajima, Mbunge na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu kuhusu madhumuni na sababu za Muswada huu. Baada ya Kamati kupatiwa maelezo ya Serikali, Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali na kupata maelezo ya ufafanuzi katika ibara mbalimbali za Muswada.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilifanya Mkutano wa kusikiliza maoni ya wadau *(Public Hearing*) tarehe 15 na 16 Agosti, 2024 ili kupokea maoni yao kuhusu Muswada huu. Aidha, Kamati ilipokea maoni kwa njia ya mtandao kutoka kwa watu na makundi mbalimbali ya wadau ambao hawakuweza kufika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao.

Mheshimiwa Spika, Napenda kuwashukuru wadau wote waliotoa maoni yao ili kuuboresha Muswada huu na nichukue fursa hii kuwatambua kama ifuatavyo: -

(i) Mashirika 24 yasiyo ya Kiserikali yanayojishughulisha na afua za watoto ambao ni: *Genesis for Children Organization*, *Support for the Future Foundation, Tanzania Girls Guides Association, Tanzania Child Rights Forum, UNICEF, Lecri Consult, Investing in Children and Strengthening their Community,* Mtoto wa Tanzania *Foundation,* Msichana *Initiative, Save the Children, TAWLA, Children Dignity Forum,* HEKIMA, *Women Global Network For Reproductive Rights Africa, Boys Initiative, The Inclusive Forum on People with Disabilities Voice and Agenda, WEADO,* Fikra Mpya, *Legal Human Rights Center, YWL,* Jamii Kwanza, Macho kwa Jamii na Malezi *Foundation;*

(ii) Mtandao wa Wanawake Haki za Uzazi;

(iii) Akili *Platform* Tanzania;

(iv) *Children Education Society;*

(v) *Institute of Social Work;*

(vi) Tume ya Haki za Binadamu; na

(vii) Wadau binafsi kutoka maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo, Wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya Muswada kwa

kuzingatia hoja zilizotokana na maelezo, uchambuzi, maoni pamoja na nyaraka mbalimbali kuhusiana na Muswada huu. Mnamo tarehe 20 Agosti, 2024 Kamati ilikutana tena na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu ili kujadiliana kuhusu hoja zilizobainika kwa kila ibara ya Muswada na kumshauri Waziri kufanya marekebisho katika ibara zilizoonekana kuhitaji marekebisho kwa mujibu wa Kanuni ya 97(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo, nilizingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kukujulisha rasmi kwamba Kamati imekamilisha uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bungeni.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Muswada; Kamati ilichambua Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali za Ulinzi wa Mtoto wa Mwaka 2024 *[The Child Protection Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024]* ukiwa umegawanyika katika sehemu nne na unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria tatu kwa madhumuni ya kuondoa upungufu au dosari au kutatua changamoto ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wa sheria hizo kama zilivyoelezwa na mtoa hoja mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni zifuatazo: -

(a) Sheria ya Makosa ya Kimtandao, Sura ya 443 (*The Cyber Crimes Act, Cap. 443*);

(b) Sheria ya Mtoto, Sura ya 13 (*The Law of the Child Act, Cap.13*); na

(c) Sheria ya Msaada wa Kisheria, Sura ya 21(*The Legal Aid Act. 21*).

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kwanza ya Muswada inahusu masharti ya utangulizi, inajumuisha Ibara ya kwanza inayohusu jina fupi na Ibara ya pili inayoeleza marekebisho yanayofanyika katika sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, sheria zinazofanyiwa marekebisho na maudhui yake; Kamati imefanya uchambuzi wa maudhui ya marekebisho ya Muswada kwa kuzingatia changamoto ambazo mtoa hoja alieleza Kamati kuwa Muswada huu umelenga kuzitatua pamoja na masuala mengine ambayo Kamati iliona yanafaa kuzingatiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, Kamati imefanya uchambuzi wa mapendekezo yote ya marekebisho kwa kila Ibara ya Muswada kama inavyofafanuliwa hapo chini.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Makosa ya Kimtandao, Sura ya 443. Marekebisho hayo yanafafanuliwa katika Ibara ya 3 hadi 10 ya Muswada. Marekebisho katika sehemu hii yanalenga kufanya tafsiri ya misamiati mahususi katika Sheria ya Mtoto, kuongeza masharti mapya yanayohusu makosa ya unyanyasaji na utumikishaji wa kingono kwa mtoto kwa kutumia mifumo ya TEHAMA.

Mheshimiwa Spika, vilevile marekebisho katika sheria hii yanakusudia kukataza uchapishaji wa Makala zinazochochea mauwaji ya halaiki na ukatili dhidi ya binadamu ikiwa pamoja na watoto kwa kuongeza maneno ‘makosa dhidi ya binadamu’ ili kuwa na maana iliyotolewa chini ya Mkataba wa Roma wa Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu ya 1998.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo mengine ni kuweka masharti yanayozuia mtu au mfumo wa kompyuta kutekeleza kitendo cha ugaidi pamoja na kuweka adhabu kwa mtu anayekiuka masharti hayo. Vilevile yameweka utaratibu wa kumjumuisha Mkurugenzi au Afisa wa Kampuni au Taasisi kuwajibika kwa makosa ya kimtandao yanayofanywa na kampuni au taasisi na kuweka masharti kuwa Kifungu cha 50 hakitatumika katika Kifungu cha 13 kinachohusu makosa ya udhalilishaji wa kingono kwa watoto ili adhabu za makosa ya udhalilishaji wa kingono kwa watoto zitolewe na Mahakama pekee.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Mtoto, Sura ya 13. Sehemu hii inahusu Ibara ya 11 hadi 42 ya Muswada. Kamati ilielezwa kuwa marekebisho katika Sheria hii yanajumuisha mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuipa uwezo Mahakama wa kuzingatia taarifa ya uchunguzi wa kitaalamu kutoka kwa Afisa Ustawi wa Jamii wakati wa kuzingatia amri ya kugharamia vipimo vya vinasaba, kubainisha mamlaka ya Mahakama katika kushughulikia mashauri ya kuasili watoto ambapo Mahakama kuu itashughulikia mashauri ya kuasili kwa asiye ndugu na kwa ndugu ni katika Mahakama ya Hakimu Mkazi, Mahakama ya Wilaya na Mahakama za Watoto.

Mheshimiwa Spika, kifungu hiki kimeongeza Mahakama ya Watoto katika kushughulikia masuala haya ili kuongeza ufanisi na kupunguza mlundikano wa mashauri katika Mahakama zingine.

Mheshimiwa Spika, aidha, sheria inapendekeza kuipa mamlaka Mahakama ya kubatilisha amri ya kuasili mtoto baada ya kupokea maombi kutoka kwa mzazi, mlezi, ndugu wa mtoto aliyeasiliwa au mtu mwingine yeyote mwenye maslahi endapo itaonekana maslahi ya mtoto hayajazingatiwa na vilevile kinaeleza kuwa maombi ya kubatilisha amri ya kuasili mtoto yatafanywa kabla mtoto aliyeasiliwa hajafikisha miaka 24.

Mheshimiwa Spika, marekebisho mengine ni kupunguza muda wa mwombaji wa kuasili mtoto asiye Mtanzania kukaa nchini kutoka miaka mitatu hadi miaka miwili. Vilevile marekebisho haya yanalenga kuanzisha mabaraza ya watoto katika kila kijiji, kata, wilaya, mkoa, na katika ngazi ya Taifa ikiwa na lengo la kuanzisha majukwaa yatakayoweza kujua changamoto zinazowakabili watoto na kuwalinda dhidi ya unyanyasaji unaofanywa katika jamii.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika, marekebisho haya yemepanua wigo wa makosa ya ukatili wa kingono dhidi ya watoto ambapo pamoja na makosa yaliyopo kwenye kifungu hiki yameongezeka makosa mengine sita ili kuongeza ulinzi wa watoto dhidi ya uhalifu wa kingono ambao umeongezeka kwa kasi kutokana na kukua kwa teknolojia.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Msaada wa Kisheria, Sura ya 21. Sehemu hii inahusu Ibara ya 43 na 44. Marekebisho katika sehemu hii yanalenga kumpa hakimu mamlaka ya kumwelekeza wakili kumwakilisha mtoto ambaye ni mshtakiwa inapothibitika kuwa mshatikwa anapaswa kupata msaada wa kisheria. Lengo ni kuhakikisha mtoto ambaye ni mshatakiwa anapata uwakilishi wa kisheria.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati, kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum isipokuwa kwa baadhi ya maeneo ambayo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni, mapendekezo na kufanya marekebisho ya msingi ili kuuboresha Muswada huu kama inavyofafanuliwa katika aya zifuatazo.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Sheria ya Makosa ya Kimtandao, Sura ya 443 Ibara ya 4 inatoa tafsiri ya misamiati mbalimbali ilipendekeza tafsri ya neno "*Child sexual abuse material or child sexual exploitation material*" ambapo maneno "*Other activities that are not sexual*" yalionekana kutokuwa na maana kutokana na tafsiri iliyopo katika maneno hayo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilishauri maneno hayo yafutwe, Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati kwa kuwa kuondolewa na kufanya maboresho kwenye Muswada kulingana na ushauri wa Kamati kwani kuondolewa kwake hakuathiri dhamira iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya tano ya Muswada inarekebisha Kifungu cha 13 kinachohusu matumizi ya nyenzo za kumyanyasa mtoto na kutoa adhabu ya faini na kifungo kwa mtu atayethibika kutenda kosa hilo, aidha kifungu hiki kinaipa Mahakama mamlaka ya kuamuru mkosaji kulipa fidia kwa mwathirika.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Kamati ilishauri kuwa Kifungu hiki kirekebishwe ili Mahakama imlazimishe mkosaji kumlipa fidia mtoto aliyeathirika na kitendo cha ukatili kwa kutumia neno "*shall*" na siyo "*may*" kama ilivyotumika kwenye Muswada. Serikali

ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati na kufanya maboresha kwa kufuta neno "*may*" na kuweka neno "*shall*".

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Sheria ya Mtoto, Sura ya 13. Ibara ya 23 inaongeza Kifungu kipya cha 71(A)(2) kinachohusu sababu ambazo Mahakama itazingatia katika kufikia uamuzi wa kutengua amri ya kuasili mtoto. Moja ya sababu zilizoorodheshwa ni kushindwa kutekeleza mahitaji tarajiwa ya mtoto *(child expected needs)*. Kamati ilishauri maneno hayo yabadilishwe na badala yake yatumike maneno "kushindwa kutimiza mahitaji ya msingi ya mtoto" *(child basic need)*. Serikali ilikubaliana na Kamati na kufanya maboresho kulingana na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, aidha, Ibara ya 71(A) (3) imeeleza kuwa maombi ya kubatilisha amri ya kuasili yafanywe kabla ya mtoto aliyeasiliwa hajafikisha umri wa miaka 24. Kamati ilishauri kuwa umri wa miaka 24 uondolewe na badala yake iwe kabla hajafikisha miaka 18 kwakuwa mawanda ya sheria hii yanamtambua mtoto kuwa ni mwenye umri chini ya miaka 18. Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati na kufanya maboresho.

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 24 Kamati ilipendekeza kufuta pendekezo la kupunguza muda unaotakiwa kwa mwombaji asiye Mtanzania kukaa nchini kutoka miaka mitatu hadi miwili mfululizo na badala yake kuacha miaka mitatu kama ilivyo kwenye sheria. Pendekezo hili la Kamati linalenga kuhakikisha kuwa mamlaka husika zinapata muda wa kutosha wa kujiridhisha na mtu anayetaka kuasili mtoto. Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati na wamefanya mabadiliko kwa kuweka miaka mitatu badala ya miwili.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 27 inaongeza Kifungu cha 95(A) kinachohusu uanzishaji wa Mabaraza ya Watoto. Mapendekezo ya Kamati katika Kifungu hiki ni kuongeza aya mpya itakayompa Waziri mwenye dhamana mamlaka ya kutengeneza kanuni za uendeshaji wa mabaraza hayo. Mapendekezo ya Kamati yanalenga kuwepo kwa Kanuni zitakazofafanua uendeshaji wa mabaraza haya.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati ilishauri kuwa Kanuni ambazo zitatengenezwa na Waziri zizingatie uanzishwaji wa Mabaraza ya Watoto kwa kuzingatia ujumuishwaji wa makundi yote ya watoto katika mabaraza hayo hasa wale wenye mahitaji maalumu na wale wanaotokea katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati ilishauri kuwa neno "*Junior Councils*" liondolewe na badala yake litumike neno "*Children Council*" ili kushabihiana na tafsiri ya Kiswahili ya Mabaraza ya Watoto. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, tunaipongeza Serikali kwa kukubaliana na ushauri wa Kamati na wamefanya mabadiliko kwa kuzingatia ushauri wa Kamati kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa jumla, pamoja na mapendekezo ambayo Kamati imeyatoa katika kila Ibara ya Muswada, Kamati ina maoni na ushauri wa jumla ambao ni vema Serikali ikauzingatia na kuufanyia kazi kwa kuwa ni masuala yanayohusiana na watoto kama ifuatavyo:-

(a) Sheria zote zinazohusiana na masuala ya watoto zipitiwe upya kwa lengo la kuhusianisha na kusomana kulingana na mazingira ya sasa;

(b) Serikali ione umuhimu wa kutenga bajeti kwa ajili ya kuendesha Mabaraza ya Watoto yaliyoanzishwa kwenye Sheria hii; na

(c) Kutokana na Majukumu aliyoongezewa Afisa Ustawi wa Jamii katika Sheria hii, Serikali ione umuhimu wa kuajiri Maafisa Ustawi wa Jamii ambapo kwa sasa kuna upungufu wa 95.3% ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu

wa mchango wao katika kushughulikia Muswada huu, naomba majina yao yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Dorothy Onesphoro Gwajima, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na Naibu Waziri Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis, Mbunge; Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali Ndugu Onorius Njole, pamoja na watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati katika kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* na kwa upekee Sekretarieti ya Kamati kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, msimamo wa Kamati kuhusu hoja; baada ya kusema hayo, Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho kama lilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI ZA ULINZI WA MTOTO WA MWAKA 2024 *[THE CHILD PROTECTION LAWS (MISCELLENAOUS AMENDMENTS) BILL, 2024]* -KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali za Ulinzi wa Mtoto wa Mwaka 2024 *[the Child Protection Laws*

*(Miscellenaous Amendments) Bill, 2024]* kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

**Mheshimiwa Spika**, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali za Ulinzi wa Mtoto wa Mwaka 2024 ulisomwa Bungeni kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Kumi na Tano, Kikao cha Hamsini na Sita kwenye Bunge la Kumi na Mbili, tarehe 28 Juni, 2024 kwa mujibu wa Kanuni ya 93 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136 (14) na Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, uliuelekeza Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa kwa kina. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba, Kamati imeuchambua na kuujadili Muswada huu kwa kuzingatia, Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

### 1.2 Namna Uchambuzi wa Muswada ulivyofanyika.

**Mheshimiwa Spika**, hatua za kuufanya muswada huu zilianza kwa maandalizi mbalimbali ya kiutendaji yaliyofanywa na Sekretarieti kwaajili ya kuwezesha utekelezaji bora wa shughuli za Kamati. Maelezo ya uchambuzi wa muswada ulifanywa na kuwasilishwa kwenye Kamati na Sekretarieti ya Bunge kwa mujibu wa Kanuni 24(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Hatua hii ilijenga msingi wa utekelezaji wa kazi za Kamati kuhusiana na Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana na Serikali tarehe 14 Agosti, 2024 ili kupokea maelezo ya Mhe. Doroth Onesphoro Gwajima, (Mb) Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu kuhusu madhumuni na sababu za Muswada huu. Baada ya Kamati kupatiwa maelezo ya Serikali, Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali, na kupata maelezo ya ufafanuzi katika ibara mbalimbali za Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Kamati ilifanya Mkutano wa kusikiliza maoni ya wadau *(Public Hearing*) tarehe 15 na 16 Agosti, 2024 ili kupokea

maoni yao kuhusu Muswada huu. Aidha, Kamati ilipokea maoni kwa njia ya mtandao kutoka kwa watu na makundi mbalimbali ya wadau ambao hawakuweza kufika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao.

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuwashukuru wadau wote waliotoa maoni yao ili kuuboresha Muswada huu na nichukue fursa hii kuwatambua kama ifuatavyo: -

1. Mashirika 24 yasiyo ya kiserikali yanayojishughulisha na afua za watoto ambao ni Genesis for Children Oranization, Support for the Future Foundation, Tanzania Girls Guides Association, Tanzania Child Rights Forum, UNICEF, Lecri Consult, investing in Children and Strengthening their Community, Mtoto wa Tanzania Foundation, Msichana Initiative, Save the Children, TAWLA, Children Dignity Forum, HEKIMA, Women Global Network For Reproductive Rights Africa, Boys Initiative, The Inclusive Forum on People with Disabilities voice and Agenda, WEADO, Fikra Mpya, Legal Human Rights Center, YWL, Jamii Kwanza, Macho kwa Jamii, Malezi Foundation.

2. Mtandao wa Wanawake Haki za uzazi

3. Akili Platform Tanzania

4. Children Education Society

5. Institute of Social Work

6. Tume ya Haki za Binadamu

7. Wadau binafsi kutoka maeneo mbalimbali nchini.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, Wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia hoja zilizotokana na maelezo, uchambuzi, maoni pamoja na nyaraka mbalimbali kuhusiana na muswada huu. Mnamo tarehe 20 Agosti, 2024 Kamati ilikutana tena na Waziri wa

Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu ili kujadiliana kuhusu hoja zilizobainika kwa kila ibara ya Muswada na kumshauri Waziri kufanya marekebisho katika Ibara zilizoonekana kuhitaji marekebisho kwa mujibu wa Kanuni ya 97(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, nilizingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kukujulisha rasmi kwamba Kamati imekamilisha uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bungeni.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

### 2.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kamati ilichambua Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali za Ulinzi wa Mtoto wa Mwaka 2024 *[the Child Protection Laws (Miscellenaous Amendments) Bill, 2024]* ukiwa umegawanyika katika sehemu Nne (4) na unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria tatu (3) kwa madhumuni ya kuondoa mapungufu au dosari au kutatua changamoto ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wa Sheria hizo kama zilivyoelezwa na mtoa hoja mbele ya Kamati. Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni zifuatazo: -

(a) Sheria ya Makosa ya Kimtandao, Sura ya 443 (*The Cyber Crimes Act, Cap. 443*)

(b) Sheria ya Mtoto, Sura ya 13; (*The Law of the Child Act, Cap.13*)

(c) Sheria ya Msaada wa Kisheria, Sura ya 21; (*The Legal Aid Act. 21*)

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Kwanza ya Muswada inayohusu masharti ya utangulizi, inajumuisha **Ibara ya 1** inyohusu jina fupi na **Ibara ya 2** inayoeleza marekebisho yanayofanyika katika sheria mbalimbali.

## 2.2 Sheria Zinazofanyiwa Marekebisho na Maudhui yake

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi wa maudhui ya marekebisho ya Muswada kwa kuzingatia changamoto ambazo mtoa hoja alieleza Kamati kuwa Muswada huu umelenga kuzitatua pamoja na masuala mengine ambayo Kamati iliona yanafaa kuzingatiwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa msingi huo, Kamati imefanya uchambuzi wa mapendekezo yote ya marekebisho kwa kila Ibara ya Muswada kama kama inayofafanuliwa hapo chini.

**2.2.1 Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya **Sheria ya Makosa ya Kimtandao, Sura ya 443 (*The Cyber Crimes Act, Cap. 443*)** Marekebisho hayo yanafafanuliwa katika ibara ya 3 hadi 10 ya muswada. Marekebisho katika sehemu hii yanalenga kufanya tafsiri ya misamiati mahususi katika sheria ya mtoto, kuongeza masharti mapya yanayohusu makosa ya unyanyasaji na utumikishaji wa kingono kwa mtoto kwa kutumia mifumo ya TEHAMA.

**Mheshimiwa Spika,** Vilevile marekebisho katika sheria hii yanakusudia kukataza uchapishaji wa Makala zinazochochea mauwaji ya halaiki na ukatili dhidi ya binadamu ikiwa pamoja na watoto kwa kuongeza maneno makosa dhidi ya binadamu ili kuwa na maana iliyotolewa chini ya Mkataba wa Roma wa Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu ya 1998".

Mapendekezo mengine ni kuweka masharti yanayozuia mtu au mfumo wa kompyuta kutekeleza kitendo cha ugaidi pamoja na kuweka adhabu kwa mtu anayekiuka masharti hayo. Na vilevile yameweka utaratibu wa kumjumuisha Mkurugenzi au Afisa wa kampuni au Taasisi kuwajibika kwa makosa ya kimtandao yanapofanywa na Kampuni au Taasisi na kuweka masharti kuwa Kifungu cha 50 hakitatumika katika Kifungu cha 13 kinachohusu makosa ya udhalilishaji wa kingono kwa watoto ili adhabu za makosa ya udhalilishaji wa kingono kwa watoto zitolewe na Mahakama pekee.

**2.2.2 Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya **Sheria ya Mtoto, Sura ya 13 (*The Law of the Child Act, Cap. 13***. Sehemu hii inahusu ibara ya 11 hadi 42 ya muswada. Kamati ilielezwa kuwa marekebisho katika Sheria hii yanajumuisha mambo mbalimbali ilkiwa ni pamoja na kuipa uwezo Mahakama wa kuzingatia taarifa ya uchunguzi wa kitaalamu kutoka kwa Afisa Ustawi wa Jamii wakati wa kuzingatia amri ya kugharamia vipimo vya vinasaba, kubainisha mamlaka ya Mahakama katika kushughulikia mashauri ya kuasili watoto ambapo Mahakama kuu itashughulikia mashauri ya kuasili kwa asiye ndugu na kwa ndugu ni katika Mhakama ya Hakimu Mkazi, Mahakama ya Wilaya na Mahakama za Watoto. Kifungu hiki kimeongeza Mahakama ya Watoto katika kushughulikia masuala haya ili kuongeza ufanisi na kupunguza mlundikano wa mashauri katika Mahakama zingine.

Aidha Sheria inapendekeza kuipa mamlaka Mahakama ya kubatilisha amri ya kuasili mtoto baada ya kupokea maombi kutoka kwa mzazi, mlezi, ndugu wa mtoto aliyeasiliwa au mtu mwingine yeyote mwenye maslahi endapo itaonekana maslahi ya mtoto hayajazingatiwa na vilevile kinaeleza kuwa maombi ya kubatilisha amri ya kuasili mtoto yatafanywa kabla Mtoto aliyeasiliwa hajafikisha miaka 24**.**

**Mheshimiwa Spika,** marekebisho mengine ni kupunguza muda wa mwombaji wa kuasili mtoto asiye mtanzania kukaa nchini kutoka miaka mitatu hadi miaka miwili. Vilevile marekebisho haya yanalenga kuanzisha mabaraza ya watoto katika kila Kijiji, Kata, Wilaya, Mkoa, na katika ngazi ya Taifa ikiwa na lengo la kuanzisha majukwaa yatakayoweza kujua changamoto zinazowakabili watoto na kuwalinda dhidi ya unyanyasaji unaofanywa katika jamii. Halikadhalika marekebisho haya yemepanua wigo wa makosa ya ukatili wa kingono dhidi ya watoto ambapo pamoja na makosa yaliyopo kwenye kifungu hiki yameongezeka makosa mengine sita ili kuongeza ulinzi wa watoto dhidi ya uhalifu wa kingono ambao umeongezeka kwa kasi kutokana na kukua kwa teknolojia.

**2.2.3 Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya **Sheria ya Msaada wa**

**Kisheria, Sura ya 21 (*The Lega Aid Act, Cap. 21)***. Sehemu hii inahusu Ibara ya 43 na 44. Marekebisho katika sehemu hii yanalenga kumpa Hakimu mamlaka ya kumuelekeza Wakili kumwakilisha mtoto ambaye ni mshtakiwa inapothibitika kuwa mshatikwa anapaswa kupata msaada wa kisheria. Lengo ni kuhakikisha mtoto ambaye ni mshatakiwa anapata uwakilishi wa Kisheria.

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Maelezo ya Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu isipokuwa kwa baadhi ya maeneo ambayo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni, mapendekezo na kufanya marekebisho ya msingi ili kuuboresha Muswada huu kama inavyofafanuliwa katika aya zinazofuata.

### 3.2 Marekebisho ya Sheria ya Makosa ya Kimtandao, Sura ya 443 (*The Cyber Crimes Act, Cap. 443)*

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 4 inatoa tafsiri ya misamiati mbalimbali ilipendekeza tafsri ya neno "Child Sexual abuse Material or Child sexual exploitation material ambapo maneno "other activities that are not sexual" yalionekana kutokuwa na maana kutokana na tafsri iliyopo katika maneno hayo. Kamati ilishauri maneno hayo yafutwe. Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati kwa kuwa kuondolewa na kufanya maboresho kwenye muswada kulingana na ushauri wa Kamati kwani kuondolewa kwake hakuathiri dhamira iliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 5 ya Muswada inarekebisha Kifungu cha 13 kinachohusu matumizi ya nyenzo za kumyanyasa mtoto na kutoa adhabu ya faini na kifungo kwa mtu atayethibika kutenda kosa hilo, aidha kifungu hiki kinaipa Mahakama mamlaka ya kuamuru mkosaji kulipa fidia kwa muathirika. Hata hivyo Kamati ilishauri kuwa Kifungu hiki kirekebishwe ili Mahakama imlazimishe mkosaji kumlipa fidia mtoto aliyeathirika na kitendo cha ukatili

kwa kutumia neno “shall” na siyo “may” kama ilivyotumika kwenye muswada. Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati na kufanya maboresha kwa kufuta neno “May” na kuweka neno “Shall”

### 3.3 Marekebisho ya Sheria ya Mtoto, Sura ya 13 (*The Law of the Child Act, Cap. 13*

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 23 inaongeza Kifungu kipya cha 71A (2) kinachohusu sababu ambazo mahakama itazingatia katika kufikia uamuzi wa kutengua amri ya kuasili mtoto, moja ya sababu zilizoorodheshwa ni kushindwa kutekeleza mahitaji tarajiwa ya mtoto (Child expected needs). Kamati ilishauri maneno hayo yabadilishwe na badala yake yatumike maneno “kushindwa kutimiza mahitaji ya msingi ya mtoto” (Child basic need). Serikali ilikubaliana na Kamati na kufanya maboresho kulingana na mapendekezo ya Kamati.

Aidha Ibara ya 71A (3), imeeleza kuwa maombi ya kubatilisha amri ya kuasili yafanywe kabla ya mtoto aliyeasiliwa hajafikisha umri wa miaka 24. Kamati ilishauri kuwa umri wa miaka 24 uondolewe na badala yake iwe kabla hajafikisha miaka 18 kwakuwa mawanda ya sheria hii yanamtambua mtoto kuwa ni mwenye umri chini ya miaka 18. Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati na kufanya maboresho.

**Mheshimiwa Spika** Katika Ibara ya 24 Kamati ilipendekeza kufuta pendekezo la kupunguza muda unaotakiwa kwa mwombaji asiye Mtanzania kukaa nchini kutoka miaka mitatu hadi miwili mfulul ilzo na badala yake kuacha miaka mitatu kama ilivyo kwenye sheria, pendekezo hili la Kamati linalenga kuhakikisha kuwa mamlaka husika zinapata muda wa kutosha wa kujiridhisha na mtu anayetaka kuasili mtoto. Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati na wamefanya mabadiliko Kwa kuweka miaka mitatu badala ya miwili.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 27 inaongeza Kifungu cha 95A kinachohusu uanzishaji wa Mabaraza ya Watoto. Mapendekezo ya Kamati katika Kifungu hiki ni kuongeza aya mpya itakayompa Waziri mwenye dhamana mamlaka ya kutengeneza Kanuni za

uendeshaji wa Mabaraza hayo. Mapendekezo ya Kamati yanalenga kuwepo kwa Kanuni zitakazofafanua undeshaji wa mabaraza haya. Aidha Kamati ilishauri kuwa Kanuni ambazo zitatengenezwa na Waziri zizingatie uanzishwaji wa Mabaraza ya Watoto kwa kuzingatia ujumuishwaji wa makundi yote ya watoto katika mabaraza hayo hasa wale wenye mahitaji maalumu na wale wanaotokea katika mazingira magumu.

Vilevile Kamati ilishauri kuwa neno "Junior Councils" liondolewe na badala yake litumike neno "Children Council" ili kushabihiana na tafsiri ya Kiswahili ya Mabaraza ya Watoto. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Tunaipongeza Serikali kwa kukubaliana na ushauri wa Kamati na wamefanya mabadiliko kwa kuzingatia ushauri wa Kamati kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali.

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA JUMLA

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mapendekezo ambayo Kamati imeyatoa katika kila Ibara a Muswada, Kamati ina maoni na ushauri wa jumla ambao ni vema Serikali ikauzingatia na kuufanyia kazi kwa kuwa ni masuala yanayohusiana na Watoto kama ifuatavyo;

a) Sheria zote zinazohusiana na masuala ya watoto zipitiwe upya kwa lengo la kuhusianisha na kusomana kulingana na mazingira ya sasa.

b) Serikali ione umuhimu wa kutenga Bajeti kwaajili ya kuendesha Mabaraza ya Watoto yaliyoanzishwa kwenye Sheria hii.

c) Kutokana na Majukumu aliyoongezewa Afisa Ustawi wa Jamii katika Sheria hii, Serikali ione umuhimu wa kuajiri Maafisa Ustawi wa Jamii ambapo kwasasa kuna upungufu wa **asilimia 95.3** ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

## 5.0 HITIMISHO

### 5.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia muswada huu, naomba niwatambue kama ifuatavyo: -

1. Mhe.Fatma Hassan Toufiq, Mb. – **Mwenyekiti**
2. Mhe.Riziki Said Lulida, Mb. – **Makamu Mwenyekiti**
3. Mhe. Tamima Haji Abass, Mb.
4. Mhe.Neema Gerald Mwandabila, Mb.
5. Mhe.Tecla Mohammed Ungele, Mb.
6. Mhe.Kabula Enock Shitobela, Mb.
7. Mhe.Mohamed Abdulrahman Mwinyi, Mb.
8. Mhe.Katani Ahmadi Katani, Mb.
9. Mhe. Ahmed Ally Salum, Mb.
10. Mhe. Furaha Ntengo Matondo, Mb.
11. Mhe. Mariam Nassoro Kisangi, Mb.
12. Mhe. Athuman Almas Maige, Mb.
13. Mhe. Alli Hassan Omar King, Mb.
14. Mhe. Boniphace Mwita Getere, Mb.
15. Mhe. Sanya Juma Jafar, Mb.
16. Mhe. Shanif Mansoor Jamal, Mb.
17. Mhe. Michael Mwita Kembaki, Mb.
18. Mhe. Neema Kachiki Lugangira, Mb.
19. Mhe. Khamis Yussuf Mussa, Mb
20. Mhe. January Yussuf Makamba, Mb
21. Mhe. Khadija Shaban Taya, Mb

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Dkt. Doroth Onesphoro Gwajima Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na Naibu Waziri Mhe. Mwanaidi Ali Khamis, Mb, Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali Ndg. Onorius Njole, pamoja na watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati katika kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* na kwa upekee Sekretarieti ya Kamati kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**5.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, Kamati inalishauri Bunge lako tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho kama lilivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Mhe. Fatma Hassan Toufiq (Mb)

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII**
30 Agosti, 2024

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge ninayo majina hapa ya Wabunge ambao wameomba kuchangia hoja hii. Tutaanza na Mheshimiwa Athuman Almas Maige, atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mheshimiwa Tecla Mohamedi Ungele ajiandae.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na mimi kuniruhusu niwe mtu wa kwanza kuchangia Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Ulinzi wa Mtoto wa Mwaka 2024 *[The Child Protection Law (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024]*.

Mheshimiwa Spika, Muswada unapendekeza marekebisho katika sheria zifuatazo na sheria hizi ni muhimu kwa ajili ya ulinzi wa mtoto: Sheria ya Makosa ya Kimtandao Sura Namba 443 *(The Cyber Crime Act Cap 443)*; Sheria ya Mtoto Sura ya 13 (*The Law of the Child Act Cap 13);* na Sheria ya Msaada wa Kisheria Sura ya 21*(The Legal Aid Act Cap 21)*.

Mheshimiwa Spika, katika Sheria ya Makosa ya Kimtandao Sura ya 444 Muswada huu unapendekeza marekebisho Katika tafsiri ya misamiati mahususi katika Sheria ya Mtoto kwa ajili ya kumlinda mtoto. Vilevile kuongeza masharti mapya yanayohusu makosa ya unyanyasaji na utumikishaji wa kingono kwa mtoto kwa kutumia vifaa vya TEHAMA. Marekebisho yanayopendekezwa yanaweka katazo la uchapishaji kwa mfano ya makala zinazochochea mauaji lakini pia yale mauaji ya halaiki na ukatili dhidi ya binadamu na watoto.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Mtoto Sura ya 13 Ibara ya 11 hadi ya 42 zinazohusu kuasiliwa au kuasili taratibu za kuasili mtoto. Muswada unapendekeza kuipa Mahakama mamlaka mahususi ya kubatilisha amri ya kuasili mtoto baada ya kupokea malalamiko au maombi kutoka kwa mzazi, mlezi au ndugu wa mtoto aliyeasiliwa.

Mheshimiwa Spika, endapo itathibitika au itaonekana maslahi ya mtoto aliyeasiliwa hayajazingatiwa kama ilivyokubalika huko mwanzoni. Maombi ya kubatilisha amri ya mtoto kuasiliwa yatafanywa kabla ya mtoto hajatimiza miaka 18. Ni muhimu katika mapendekezo ya awali Serikali ilileta kwamba maombi yatafanywa chini ya miaka 24, lakini Kamati ilipendekeza kwamba miaka 24 ni mtu mzima, siyo mtoto tena. Kwa hiyo, tumekubaliana kwamba sheria hii irekebishwe na sasa maombi haya ya kubatilisha uasili wa mtoto chini ya miaka 18.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya tano ya Muswada inarekebisha Kifungu cha 13 cha sheria kinachohusu matumizi ya nyenzo ya kumnyanyasa mtoto, pia kimekuja na adhabu ya faini ya kifungo kwa mtu ambaye atathibitika ametenda kosa hilo. Pia, Kifungu kinaipa Mahakama mamlaka maalum ya kuamuru mkosaji kumlipa mwathirika fidia.

Mheshimiwa Spika, marekebisho yanayopendekeza shuruti ya kulipa fidia kuwa ya lazima kwa kubadili Kifungu kile cha shuruti ya "*may*" na kufanya shuriti ya "*shall*" kwa malipo ya fidia.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 27 inaongeza Kifungu cha 95(a) kinachoanzisha mabaraza ya watoto, Kamati imeshauri mabaraza yaitwe *Child Council* kutokana na neno 'mtoto.' Waziri anashauriwa kutunga kanuni ambazo zitazingatia kuyahusisha makundi yote ya watoto wenye mahitaji maalum na wenye mazingira magumu kutoka kwenye maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, masharti ya sheria zote zinazohusu watoto, naomba niliweke wazi hilo. Nashauri mimi sheria zote zilizopo sasa hivi zinazowahusu watoto zirekebishwe na Bunge lako ili ziendane na mazingira ya sasa, kwa sababu sheria hizi mwaka huu na miaka michache iliyopita kumekuwa na matukio mengi yanayohusu watoto. Kwa hiyo, tunapendekeza na kushauri sheria zote zinazohusu watoto zipitiwe upya, ziendane mazingira ya sasa.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali iweke bajeti ya mabaraza haya ya watoto yanayopendekezwa ili yawe na ufanisi, lakini yaweze kukamilika na kukutana mikutano bila kuwa na ukwasi au matatizo ya fedha.

Mheshimiwa Spika, Serikali izibe pengo la watumishi, sasa hivi Serikali inajua kwamba upungufu wa watumishi wanaotakiwa ambao ni Maafisa Ustawi wa Jamii, upungufu huo kwa sasa ni 95.3%, yaani ufanisi waliopo sasa hivi ni asilimia nne nukta saba tu na hawatoshi kufanya kazi kwa ajili ya utendaji unaotakiwa wa kuhudumia watoto. Nashauri Serikali ifanye juhudi kubwa sana za kuweza kuwapata hawa Maafisa Ustawi wa Jamii ili waweze kufanya kazi zao za kulinda watoto.

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana na ninaunga mkono hoja, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi siku ya leo, nami niweze kuchangia kwenye Muswada huu muhimu wa Marekebisho ya Sheria zinazohusu Ulinzi wa Mtoto. Tuipongeze sana Serikali yetu na nampongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, nampongeza Mheshimiwa Waziri wetu,

Naibu Waziri, Makatibu Wakuu wa Wizara hii na wote kwa pamoja kwa kuona umuhimu sasa wa kuleta marekebisho ya Sheria hii ya Ulinzi wa Mtoto.

Mheshimiwa Spika, tumeona katika nchi yetu kadri ya siku zilivyokuwa zinaendelea kumekuwa na changamoto kubwa sana ya matatizo ya Watoto, Ukatili wa kijinsia kwa watoto. Tatizo linaloendelea ni kubwa, hivyo basi, naipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Muswada huu nitachangia katika Kifungu cha 23, Kifungu cha 12, Kifungu cha 19(A), Kifungu cha 49, Kifungu cha 102, Kifungu cha 96(A) na Kifungu cha 115. Nikianza na Kifungu cha 12. Kifungu cha 12 kimewezesha kuingiza Mahakama za Watoto katika sharti la kuasili mtoto. Hii Mahakama mwanzoni haikuwepo, zilikuwa zile Mahakama nyingine ambazo zinaenda kufanyiwa utaratibu pale mtu anapotaka kumuasili mtoto kumleta katika familia yake.

Mheshimiwa Spika, sasa imewekwa na Mahakama hii ya Watoto. Hii ndiyo Mahakama yao, ndiyo Mahakama ambayo inahusu kushughulikia masuala ya watoto. Kwa hiyo, Serikali sasa imeleta na hili la kuasili mtoto liende nalo kwenye Mahakama ya Watoto.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa kuona umuhimu, tunapenda sana watoto wetu wachukuliwe wakaishi katika familia mbalimbali, wasikae sana kwenye makao, lakini zile taratibu za Mahakama zilikuwa ni ngumu sana kiasi kwamba mtu anaweza akakosa hata ile hamu ya kumtaka yule mtoto kutokana na masharti mengi. Sasa wameweka Mahakama ya Mtoto ishughulikie suala la uasili wa mtoto, hivyo hizo kesi na mashauri hayo tuna imani yatakwenda kwa haraka ili wale watoto sasa wapatiwe wazazi wa kambo waende wakalelewe katika familia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikija Kifungu cha 23, kinaongezea Kifungu cha 71(A) kinachoipa Mahakama kufuta na kubatilisha amri ya kuasili mtoto baada ya kupokelewa maombi na kujiridhisha. Tunatambua wapo watu wanapewa watoto hawa,

wanaenda nao kisheria na wanachukua watoto wanaenda kuishi nao nyumbani, lakini wanapofika huko, maisha yao wanakwenda kukuta ni kinyume na yale matarajio yao, wanaishi katika mazingira magumu, yale matarajio hata mahitaji muhimu ya kielimu, chakula na nini inakuwa ni shida.

Mheshimiwa Spika, hivyo Muswada huu umeweka kipengele hicho kuongeza hicho Kifungu cha 71(A) ili sasa mtoto yule atakapoona aidha ni yeye au mtu yeyote anayemsimamia kwenda naye kwenye Mahakama kwenda kubatilisha uasili ule. Ni jambao zuri kwa familia zetu na kwa watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, natoa rai kwa ndugu na jamaa, Kifungu hiki kimewekwa katika ulinzi wa mtoto. Wapo watu wengine wana roho mbaya, wakimwona mtoto yule amechukuliwa na mtu ana kipato watamshawishi kwenda naye Mahakamani akatolewe, 'Eeh, wewe huyo anakutesa, hivi na hivi' kumbe wanaangalia mali kuliko utu. Hili nalo Mahakama waangalie katika kanuni watakazoziandaa, kuna watoto watatolewa tu kwa roho mbaya kwa kuonekana huyu aliyemuasili mtoto huyu ana pesa nyingi atafaidika. Sasa hicho nacho tukiangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lengo ni zuri pale atakapoenda pabaya aende akatolewe lakini pale anapoenda pazuri akaishi wasimtoe kwa visa, wamwache huyo mtoto aweze kuishi na mlezi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kifungu kingine ninachochangia ni Kifungu cha 19(A) ambacho kinapendekeza masharti yanayomzuia mtu au mfumo wa kompyuta kufanya vitendo vya ugaidi kuweka adhabu kwa atakayehusika, lakini Kifungu hiki pia nitakichangia kwa pamoja na Kifungu cha 49 ambacho kinaweka sharti la adhabu kwa makampuni na taasisi.

Mheshimiwa Spika, tunaona sana vitendo vya kigaidi na vitendo mbalimbali vya hovyo vikitolewa kwenye mitandao, lakini hata watoto wakiwasema katika vyombo mbalimbali kuwaweka katika mazingira magumu. Kipengele hiki na kile cha 49 kinaweka sharti la adhabu kwa taasisi na kampuni itakayohusika.

Mheshimiwa Spika, pia Mkurugenzi wa kampuni anaweza asijue kitu gani kimefanyika katika eneo hilo. Yeye ana kampuni kubwa mfanyakazi wake mmoja ameenda kufanya vibaya anaweza akaitia hasara kampuni, lakini nahisi kwamba marekebisho yale ya Kamati tuliwaambia mwangalie pia iwapo mtajiridhisha Mkurugenzi hakuhusika, basi yule mhusika mwenyewe achukuliwe hatua za kisheria.

Mheshimiwa Spika, tusiichukulie tu hivyo, kuna watu wana chuki na kampuni za wenzao wataenda kuwabambikiza kesi ilimradi kampuni iadhibiwe. Uchunguzi ufanyike na yule ambaye amehusika *personal,* kwamba huyu ndiye aliyehusika, basi anaweza akachukuliwa adhabu yeye na wala isiwe kampuni nzima, lakini iwapo lile suala litakuwa la kampuni, basi kampuni nzima au taasisi ichukuliwe adhabu yote.

Mheshimiwa Spika, pia nitachangia Kifungu cha 102, Kifungu hiki kinaeleza kutomruhusu mtoto kuchanganyika na wahalifu watu wazima katika gereza au eneo lolote. Kweli tunaona kuna watoto ambao ni watukutu wanakinzana na sheria. Watoto hawa wanachukuliwa adhabu. Kama wanachukuliwa adhabu, basi waende kwenye mahabusu za watoto wenzao, kwenye shitaka lao wasichanganywe na watu wazima.

Mheshimiwa Spika, tunajua athari nyingi za watoto wetu katika malezi na makuzi, lakini pia katika kuishi, wanapoenda kuishi na watu wazima kule mahabusu au sehemu yoyote wanaweza kufanyiwa vitendo vingine ambavyo havistahili kufanywa kwa mtoto huyo. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali izingatie hilo kwamba wasiwachanganye na naishukuru sana Serikali kuleta Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, nitachangia tena Kifungu cha 96(A) kuhusu kuanzishwa kwa mabaraza ya watoto kuanzia ngazi ya Kijiji, Kata, Wilaya, Mkoa na Taifa. Mabaraza haya yalikuwepo huko katika Wilaya zetu na katika ngazi za Halmashauri tulikuwa tunayaona, lakini sasa Serikali imeona haja ya kuyaleta mabaraza haya kisheria. Kuyaleta mabaraza haya kisheria naomba kwenye kanuni zao waangalie sasa mabaraza haya dhamira yake ni nini.

Mheshimiwa Spika, tunaona mabaraza ya vijana mpaka leo hayajatulia, leo tena tunakwenda kwenye mabaraza ya watoto. Watoto hao watakuwa *level* gani? Umri wa mtoto tunajua ni kuanzia anapozaliwa mpaka miaka 18. Sasa je, watakwenda kuchukua watoto wa aina gani na lengo la mabaraza haya katika kujua haki zao, je, mtoto huyo ana uwezo wa kutambua haki yake au kuna mada gani na ajenda gani zitakazoenda kutolewa katika mabaraza hayo?

Mheshimiwa Spika, hatutaki yawe mabaraza ya kwenda kucheza tu ukuti ukuti, wanachezacheza tu wanaongea, tunataka yawe mabaraza ambayo yataenda kuwafanya watoto hawa wakakae kujadiliana kuhusu haki zao za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naenda kwenye Kifungu cha 115 ambacho kinaeleza mtoto ambaye atakinzana na sheria akipelekwa Mahakamani kuwepo na Afisa Ustawi wa Jamii. Afisa Ustawi wa Jamii ni mtu ambaye tunamtegemea sana katika malezi ya Watoto. Hivyo basi, tunaomba Maafisa hawa wa Ustawi wa Jamii waangaliwe.

Mheshimiwa Spika, Maafisa Ustawi wa Jamii ni wachache sana katika Halmashauri zetu. Utakuta Afisa Ustawi wa Jamii kesi moja ya mtoto anaanza nayo saa nne asubuhi mpaka saa 11.00 jioni hajamaliza, hapo hapo anatakiwa ambebe mtoto ambaye amekinzana na sheria aende naye Mahakamani akamsimamie. Je, mmewaangalia na je, hawa Maafisa Ustawi wa Jamii wanapewa malipo ya kazi za ziada? Wanafanya kazi kubwa sana, kwa hiyo, Serikali iwaangalie.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Afisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya ya Ubungo, niliwashuhudia kesi moja kuanzia asubuhi saa tatu mpaka saa 12 jioni. Mara wanamtoa mtoto nje, mara wanawaingiza wazazi, mara wanaenda wategemezi na mara wanafanya hivi, ni zaidi ya Mahakama siyo suala dogo. Serikali tuone basi jinsi gani ya kuwasaidia Maafisa Ustawi wa Jamii nchi nzima, pia waajiriwe Maafisa Ustawi wa Jamii ili kuongeza nguvu katika harakati za ulinzi wa mtoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naunga mkono mapendekezo yote ya Kamati na nampongeza Mwenyekiti wangu wa Kamati na Wajumbe wenzangu wote wa Kamati pamoja na Serikali, tumeufanya msaada huu kwa kushirikiana sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tecla Mohamedi Ungele, atafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya na Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ng'anzi Ulenge ajiandae.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii nami nichangie Muswada huu. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kwa zawadi ya uzima na afya njema.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza kwa kazi zako kubwa unazozifanya kuanzia kule Jimboni Mbeya Mjini, humu Bungeni, Tanzania na kule Rais wa Mbunge ya Dunia, hakika unafanya kazi kubwa na tunajifunza kila siku, kwa kweli Mwenyezi Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naipongeza pia Serikali kuleta Muswada huu, pia naipongeza Kamati ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, tumefanya kazi kubwa kwa ushirikiano wa Wizara na Mwanasheria Mkuu na Taasisi ama asasi mbalimbali zilizokuja kutoa maoni yao wakati ule tulipokuwa tunafanya *public hearing*.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu naelekeza katika mapendekezo ya Sheria ya Makosa ya Kimtandao Sura 443 *(The Cybercrimes Act, Cap. 443),* nachangia Kifungu cha 19(a). Nimefarijika kuona kwa sasa ulinzi na usalama wa mtoto umeelekezwa kwa kuwalinda watoto wetu hawa. Watoto hawa wanatumia mitandao na ni dhahiri kabisa mitandao hii ikitumika katika mambo mazuri na katika hali nzuri itachochea mafunzo, ustawi na maendeleo ya jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona mitandao hii inatumika kwa kufundisha na kwa kujifunza, ni jambo jema sana lakini katika Kamati tuliangalia na ndiyo maana tukaleta marekebisho mbalimbali kwa ajili ya mitandao hii ambayo ikitumika vibaya itakuwa ni shida kubwa.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo yaliyokuwa yameletwa yamejielekeza pia kwenye kudhibiti na kuzuia vitendo vya kigaidi kupitia matumizi ya mifumo ya kompyuta. Mfano mzazi unaweza ukajikuta una mtoto wako hapo lakini mtoto huyo anakuwa na vitendo vya kigaidi kupitia matumizi hayo ya mifumo hiyo ya kompyuta, mara ghafla unashangaa mtoto anabadilika na anakuwa na matendo ya hatari sana hata wewe mzazi huelewi. Hii ni hatari sana. Kwa hiyo, sisi ndani ya Bunge hili tuungane pamoja tuupitishe Muswada huu ili kulinda usalama wa watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nachangia Kifungu Na. 49 ambacho kinapendekeza kwamba makosa yanayotendwa na kampuni au taasisi husika yanayoashiria matendo ya uhalifu yanavyofanyika katika taasisi husika, huyo mwenye taasisi au mhusika achukuliwe hatua. Hilo ni jambo jema sana.

Mheshimiwa Spika, kama alivyochangia Mheshimiwa Mariam Kisangi kwamba itakapogundulika kwamba huyu Mkuu wa Taasisi husika hahusiki kabisa ila ni wale watendaji wake, basi asichukuliwe hatua, lakini taasisi hiyo inapohusika, basi na kiongozi huyo pia achukuliwe hatua ili angalau kuhakikisha mitandao hii ya ofisi husika inalinda usalama na ulinzi wa watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapendekezo haya yamekuja wakati muafaka, Waheshimiwa Wabunge hebu tuungane pamoja tupitishe Muswada huu ili kuendelea kuweka usalama wa Watoto wetu na ulinzi wa watoto wetu kwani kwa sasa hivi kizazi walichonacho watoto hawa ni kiazi ambacho ni cha kidijitali na tusipokuwa makini kwa kutengeneza sheria hizi na kuzipitisha ili zikatumike kwa usahihi, basi watoto wetu na kizazi kitakuwa kimeangamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa Muswada na sheria hizi, basi tuungane kwa pamoja na naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya atafuatiwa na Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ng'anzi Ulenge na Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba ajiandae.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata fursa ya kuchangia Muswada huu wa Ulinzi wa Watoto. Kwanza, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai ambao ametupa. Kwa kweli tunamuabudu na kumheshimu Mungu wetu na tunamshukuru sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niipongeze Wizara, lakini nimpongeze zaidi Mama Samia Suluhu Hassan kwa sababu ameonyesha nia ya dhati ya kulinda mtoto wa Kitanzania. Ameonyesha nia ya dhati kwamba anaguswa na masuala ya kijamii. Ameonyesha nia ya dhati hasa kwa kutengeneza hii Wizara kwa kujitegemea tu, tayari ameonyesha namna gani anataka mabadiliko na ulinzi wa watoto na jamii nzima ambayo inatuzunguka na makundi maalum. Hivyo basi, namshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Sheria hii, katika huu ulinzi wa watoto kuna maeneo matatu; maeneo hayo ni; Sheria ya Makosa ya Kimtandao Sura 443 *(The Cybercrime Act Cap 443)* pamoja na Sheria ya Mtoto Sura ya 13, *(The Law of The Child Act Cap 13)*. Pia, Sheria ya Msaada wa Kisheria Sura 21, *(The Legal Aid Act 21)*.

Mheshimiwa Spika, nitajikita kwenye maeneo mawili au matatu kama siyo yote. Eneo la kwanza ni Ibara ya 4; katika *The Cybercrime* au Sheria ya Kimtandao kuna eneo ambalo waliandika *child sexual abuse material* pamoja na *child sexual exploitation material* lakini wakaweka maneno *other activities that are not sexual*. Hatukuona umuhimu wa neno hili lakini tuliomba Serikali ifute na kwa sababu Serikali ni sikivu imeweza kufuta eneo hili.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, katika Ibara ya 5, Kifungu 13, inahusu matumizi ya nyenzo za unyanyasaji wa watoto. Katika eneo hili tuliona zile adhabu au kifungo au faini isiwe *may* badala yake iwe *shall* kwa sababu lengo kubwa la hizi sheria ni kumlinda mtoto. Sasa ukishaweka *may* maana yake mtu anaweza kuamua

anavyojisikia yeye kwa sababu amewekewa kigezo cha *may* lakini tukimuwekea *shall* maana yake tunamlazimisha kutoa kifungo pamoja na faini katika eneo hili. Kwa hiyo maana yake tunamlinda zaidi mtoto kwa sababu ndiyo lengo kuu la eneo hili la mabadiliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Sheria ya Mtoto, Ibara ya 23 Kifungu kipya cha 71A(2) kinaongeza sababu za kutengua uasili. Katika eneo hili tuliona kabisa mtoto anaweza akawa na mahitaji zaidi, yaani, kwa namna lilivyowekwa mwanzo lilikuwa ni *expected needs,* lakini tuliona iwe ni *basic* kwa sababu kuna mahitaji yale ya lazima ambayo mtoto anaweza akapatiwa katika eneo ambalo ameasiliwa na akawa *comfortable*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuliona ni muhimu sana eneo hili liwekwe *basic needs* na siyo *expected needs* kwa sababu hata watoto wangu mimi nyumbani wanasema; mama ninunulie gari au kitu gani ambacho labda mtu hana uwezo nacho lakini ana uwezo wa kumpa chakula, malazi, elimu na maeneo mengine. Kwa hiyo, tuliona ni muhimu sana hili eneo lisitumike *expected needs* badala yake itumike *basic needs*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 24, tulishauri Kamati hiyo miaka mitatu ya mtu kuishi katika wale wanaoenda kuasili ambao ni wageni kwa sababu maeneo yale ni lazima mtu atambulike zaidi. Ikiwa miaka miwili maana yake hatuwezi kujua zaidi kwamba huyu mtu ana lengo gani la kutaka kuasili, lakini miaka mitatu maana yake una uwezo wa kumsoma zaidi au vile vitengo ambavyo vinahusika vina uwezo wa kujua kama huyu mtu na nia ya dhati kweli ya kuasili ama vipi. Kwa hiyo, kama Kamati tulishauri miaka mitatu na tunaishukuru Serikali imeweza ku-*support* na kukubali ushauri huo.

Mheshimiwa Spika, pia, katika Ibara ya 27 Kifungu cha 95A eneo la mabaraza ya watoto tuliona kwamba Waziri atakapopewa mamlaka ya kutengeneza hizo Kanuni azingatie maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuangalia makundi maalum. Pia, kuwe na namna ya uendeshaji wa haya mabaraza kwa sababu tumeona mabaraza mengi ambayo hayafanyi kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili pia Kamati iliweza kushauri kuwe na fungu maalum la kuendesha haya mabaraza kwa sababu hakuna namna ya kuweka sheria halafu hili jambo lisifanyike. Sheria tuziweke lakini litekelezeke. Kama mabaraza haya yanaenda kuwa ni sehemu ya kusaidia watoto wetu basi tuone umuhimu wa kutenga pesa kwa ajili ya kusaidia watoto katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa ujumla wake niishukuru Serikali kwa kujua umuhimu wa kuleta hizi sheria, lakini kama Kamati tuliweza kushauri iletwe Sheria nzima ya Watoto tuiangalie. Kwa namna matukio yanayoendelea katika nchi yetu sasa hivi watoto hawana amani, hawana raha na nchi yao wenyewe. Matukio ya ukatili wa kijinsia au ukatili wa watoto yamekuwa ni mengi sana.

Mheshimiwa Spika, sasa, kama Serikali tungeweza kutenga siku moja tuzungumze masuala ya watoto tu tujue ni namna gani tunaweza tukalinda watoto kwa namna ambayo tunaweza tukasaidia jamii yetu ya baadaye kwa sababu wote tunafahamu sisi wote tusingekuwa katika maisha mazuri au malezi mazuri tusingefika hapa tulipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watoto wetu sasa hivi wamekuwa *exposed* na mambo mengi sana, kuna mabadiliko ya mitandao ya kijamii sasa, wanaona vitu ambavyo hawapaswi kuona. Kwa hiyo, hizi sheria tunazozitengeneza tuzitengeneze lakini pia twende kuzipeleka huko chini watambue kuna uwepo wa hizi sheria. Vilevile na utekelezaji wa hizi sheria, Mahakama zetu waweze kutusaidia, wajue ni namna gani tunaweza kusaidia jamii yetu kwa kuweka vigezo vikali au kuendesha hizi kesi kwa haki na si vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kuna jambo linaweza kutokea baina ya mtoto na mtoto, mtoto mmoja amempa mimba mtoto mwingine, kitu kama hicho. Sasa, tunamlindaje huyu mtoto mmoja na kutomlinda huyu mwingine. Tunamlinda mtoto wa kike badala ya kumlinda na mtoto wa kiume ambaye naye pia ana maisha baada ya hapo. Kwa hiyo, vitu vyote hivi

kama Bunge tuviangalie kwa undani wake ili tuweze kusaidia na kulinda jamii yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nikupongeze kwa kukubali Sheria hii iingie hapa Bungeni tuisimamie na kuipitisha. Pia, Mheshimiwa Waziri pamoja na jopo lako na Makatibu Wakuu kwa kukubali kuleta mabadiliko haya na kukubali ushauri wa Kamati ambao lengo letu ni moja, tunajenga Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ng'anzi Ulenge atafuatiwa na Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King ajiandae.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote naendelea kumshukuru Mungu mwenye ulinzi na mwenye kunusuru. Kipekee kabisa niipongeze Serikali hii inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa inayoifanya ya kuhakikisha inawalinda watoto wetu wa Tanzania. Nawapongeza sana kwa ujio wa Muswada huu wa Sheria ya Ulinzi wa Mtoto. Kipekee kabisa niwapongeze sana kwa kuwepo kwa kipengele cha marekebisho ya matumizi ya *Cybercrime* kwa ajili ya kumlinda mtoto, niwapongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona jitihada za Serikali yetu za kuhakikisha watoto wetu wa Tanzania wanakuwa na uelewa mpana wa teknolojia ya habari na wamekuwa wanafanya juhudi kubwa kuhakikisha watoto wetu wanapewa vifaa hivi vya ki-TEHAMA wakiwa wadogo kabisa na wote tukiamini ni hatua sahihi kwa maendeleo ya Taifa letu, Tanzania siyo kijiji. Nawapongeza Serikali kwa hatua hizi na kuhakikisha kama Taifa tunakwenda kukua katika uchumi wa kidijitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hili hakika mtoto asiachwe nyuma na *no one should be left behind*. Naipongeza Serikali na tumeona watoto wetu kwa hakika wamekuwa wagunduzi, wabunifu kwa kuitumia teknolojia ya habari. Hata hivyo, sisi wote ni mashahidi kwamba kwenye mitandao kuna vihatarishi. Kwenye mitandao

kuna vihatarishi ambavyo vinapelekea watoto wetu kupata udhalilishaji na ukatili kwa kutumia mitandao yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nimeiona Sheria hii na nimeuona Muswada huu, lakini naona umewekeza nguvu zaidi katika *pornography*. Natamani Sheria hii ikaangalie kwa msisitizo mkubwa maeneo yote ambayo mtoto anakuwa *exposed* mtandaoni; kwa mfano kuna *cyber bullying*. Kwa mujibu wa *UNICEF*, inaonyesha katika nchi 30, moja ya tatu ya watoto wanapata udhalilishaji mitandaoni kwa kupitia *cyber bullying* na moja kati ya watoto watano wameacha kwenda shuleni kwa sababu ya vitendo vya udhalilishaji kwenye *criteria* hii.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo, ku-*concentrate* kwenye *pornography* pekee bado inakuwa siyo *solution*. Tunatamani tuangazie maeneo yote ambayo yataweza kupelekea mtoto kudhalilishwa mtandaoni na faragha yake kuweza kuwa hatarini. Kwa mfano, watoto wanaweza kuingia kwenye udhalilishaji wa mitandaoni kwa sauti zao na hata picha zao zinapokuwa zinaonekana mitandaoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, utashangaa watoto wetu wanakua mapema, wanapata vifaa ambavyo vinawapelekea wanakuwa na uraibu wa mitandaoni. Muda mwingi mtoto anatumia kifaa ambacho kinampelekea anatumia muda mwingi kutumia mitandao na mwisho wa siku ndiyo tunazungumza faragha ya mtoto inakuwa hatarini na inapelekea yeye mwenyewe kuingia katika uhatarishi wa kuweza kudhalilishwa mitandaoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa Sheria hii naomba ikaangazie namna ya ku-*control* siyo tu suala la watoto kuwa *exposed* mitandaoni, lakini na namna gani itaweza ku-*control*. Kwa kutumia TEHAMA hii hii vipatikane vifaa ambavyo mtoto ataendelea kupata *exposure* ya mtandao na kuhakikisha tunazuia maudhui hatarishi yasimfikie mtoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona *YouTube Kids* wana *control* hiyo. Kwa hiyo, na sisi twende tukachukue *challenge* ile ya *YouTube Kids* tuweze kui-*customize* tuone katika mazingira yetu ya

nchini tunaweza kufanyaje kuweza kuhakikisha maudhui hatarishi hayamfikii mtoto. Pia, nimeona nchi kama Belgium na France wame-*ban* matumizi ya *smartphones* kwa watoto wa *primary schools*. Hii pia inaweza ikawa ni *means* ya ku-*control* matumizi mabaya ya watoto kwenye mitandao yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tumeona nchi kama Marekani imeshatoa takwimu kuonyesha ongezeko la *cybercrime* kwa watoto wetu. Pia, tumeona Umoja wa Mataifa kupitia *ITU*; *International Telecommunication Union*, wamekuja na mkakati wa *COP (Child Online Protection)*. Hata nchini kwetu nimeona hatua zimeanza kuchukuliwa kuingia kwenye mkakati huu madhubuti wa kumlinda mtoto mtandaoni. Kwa hiyo, ninachoona sheria na sisi wote tuweke nguvu katika namna ambayo tutaweza kumlinda mtoto mtandaoni kwa sababu hatutakuwa Taifa lenye tija na kwenda sambamba na hali ya kidunia kama watoto wetu watachelewa kuingia mitandaoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi wakati tumekwenda kuzindua *Digi-Truck*, *truck* ambayo inakuwa kama *mobile laboratory* ya TEHAMA na Naibu Waziri Mkuu ndiyo alikuwa mgeni rasmi. Mwenyekiti wa Bodi (Jaji yule) alikuwa anasema yeye ameweza kuutumia mtandao na kuingia kwenye mambo ya TEHAMA baada ya kufika Chuo Kikuu. Kwa hiyo, hatuamini kama Tanzania watoto wetu wachelewe kuingia kwenye matumizi ya mtandao mpaka wafike Chuo Kikuu na Serikali inaamini hivyo ndiyo sababu imefanya juhudi kubwa za kutosha.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kipekee haitoshi, lazima tuone namna gani tuna *control*, kwa kupitia teknolojia ya TEHAMA, maudhui hatarishi kufika kwa watoto katika umri mdogo. Vilevile, tuzuie uraibu mitandaoni. Watoto wasipewe vifaa ambavyo vitawapelekea ku-*concentrate* muda mwingi kutumia vifaa hivyo na kupoteza muda mwingi wa kufanya mambo mengine ya masomo na kuendelea kuwa waraibu wa mitandaoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naona kabisa sheria iangazie mambo mengine pia siyo *pornography* peke yake. Mambo

mengine yote ambayo yanapelekea watoto kuwa *exposed* mitandaoni ili maudhui hatarishi yasiweze kuwafikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ulenge. Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni ambao wameingia hapa Bungeni baada ya tangazo la awali la wageni. Nitawatangaza hao wageni ili wale ambao wanataka kutoka waweze kutoka.

Kwanza tutaanza na tangazo la wageni waliopo Jukwaa la Spika. Tunaye Mheshimiwa Christine Grau ambaye ni Balozi wa Umoja wa Ulaya Nchini Tanzania; ambaye ameambatana na Ndugu Joseph Minde ambaye ni Afisa Habari, Ubalozi wa Umoja wa Ulaya Nchini Tanzania.; Ndugu Natasha Abdulrauf Mzee ambaye ni Afisa Dawati la Umoja wa Ulaya, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; na Ndugu Sabinus George Mwita, Afisa Mambo ya Nje (Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki). Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine saba wa Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima ambaye ni Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Hawa ni wadau wa Sheria ya Ulinzi wa Mtoto kutoka Wizara na taasisi za Serikali. Yupo Ndugu Felista Mdemu, Kaimu Katibu Mkuu (Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum). Ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Monica Mbogo, Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Makosa ya Mtandao (Ofisi ya Taifa ya Mashtaka); Mheshimiwa Mwajabu Mvungi, Naibu Msajili (Mahakama Kuu ya Tanzania); na Ndugu Ibrahimu Liguo, Kaimu Mkurugenzi, Sera na Mipango (Wizara wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum). Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia, wapo wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Wageni 38 wa Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, Waziri wa Madini, hawa ni Taasisi ya Wanawake na Mwalimu Nyerere kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo ambao ni wanafunzi 76 na walimu saba wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Ursula kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 97 na walimu watano kutoka Shule ya Awali na Msingi ya Elshadai kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 68 na walimu watatu wa Shule ya Sekondari Baraa kutoka Jijini Arusha. Karibuni sana. *(Makofi)*

Jina hapa limeandikwa Shule ya Sekondari Baraa sasa sijajua kama ndiyo jina ama tumekosea. Kama tumekosea tunaomba radhi, kama liko sawasawa basi karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, matangazo mengine yatasomwa baadaye tukishahitimisha shughuli za Bunge. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, Mheshimiwa Erick James Shigongo ajiandae.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kwenye sheria hizi muhimu zinazohusiana na ulinzi wa mtoto. Kwanza kabisa nianze kukupongeza wewe mwenyewe kwa kuona umuhimu wa suala hili. Takribani robo tatu ya jukwaa lako la wageni umewaleta wale ambao tunawajadili, yaani watoto wasikilize tunajadili nini kuhusu wao, nakupongeza sana.

Mheshimiwa Spika, pili, niipongeze Wizara, katika moja ya Wizara changa ni Wizara hii ambayo inashughulika na watoto. Bunge limekuwa na *concern* kubwa sana kuhusiana na hali ya maadili na ulinzi wa watoto katika nchi yetu. Ndani ya muda mfupi wameweza kuja na mabadiliko makubwa sana ya sheria kwa ajili ya kuwalinda watoto wetu. Kusema kweli wamefanya kazi kubwa na wameleta mabadiliko makubwa. Japo yapo mengi ambayo wameyaacha, lakini kwa kuzingatia unyeti wa jambo hili, nawapongeza sana angalau tumeanza na hatua nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na uharaka katika kuleta mabadiliko ya sheria hii ili kuweza kulinda watoto wetu, kama ambavyo Kamati imeshauri, zipo sheria nyingi ambazo bado zimeachwa nje ambazo ni za muhimu, ambazo ni za msingi na ambazo bila kubadilisha sheria hizo unyanyasaji na ukatili wa kingono kwa watoto wetu hatutaweza kuukomesha. Bunge hili tumekuwa tukisema mara kwa mara, tunayo changamoto kubwa sana ya wazazi kuwaozesha watoto wao chini ya umri wa miaka 18. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi kama sehemu ya ma-*champion*, nimewahi kusema hapa mara kadhaa, nilivyosikia inaletwa Sheria ya Ulinzi wa Mtoto na Unyanyasaji wa Kingono kwa Watoto, nilidhani moja kati ya sheria itakayoletwa hapa ni Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 kwa ajili ya kubadilisha vifungu vile. Vifungu hivi viwili vimeshabatilishwa na Mahakama, Bunge hili limeshaazimia, Serikali ilishatoa ahadi na kongamano la kitaifa lilishakaa. Sasa, ni nini mkwamo unaofanya tusibadilishe sheria hii inayowafanya watoto wetu waolewe chini ya umri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, madhara ni makubwa sana, watoto wetu wanaolewa katika umri mdogo, wanapata watoto katika umri mdogo, inahatarisha maisha yao. Nilidhani sheria hii ingeletwa ili tuweze kuipitia na kuibadilisha tuweze kuwasaidia watoto wetu waende kwenye ndoto zao. Nimeona Serikali imeweka adhabu kali sana na imeongeza viwango vya adhabu katika makosa yanayohusiana na ukatili kwa watoto na hasa ukatili wa kingono, lakini kumfunga huyu mtuhumiwa jela pekee haitoshi. Yule mtoto aliyeathirika na huyu mtu aliyemfanyia ukatili anapata faida gani? Ni lazima tuweke vifungu vinavyoipa nguvu Mahakama, ya kumlipa fidia mtoto aliyefanyiwa ukatili wa kingono. Ni lazima tuweke vifungu hivyo. Nimeona mapendekezo ya wadau yameomba tuweke vifungu vya fidia kumfidia yule mtoto aliyefanyiwa ukatili wa kingono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona Mahakama zetu zimepewa nguvu ya kuboresha mazingira ya faragha katika kesi zinazohusu watoto; lakini hapa changamoto siyo mazingira ya faragha, changamoto ni mazingira ya Mahakama zetu jinsi yalivyo. Mahamaka zinazosikiliza kesi za watoto ni chache sana nchini na

zile zilizopewa nguvu ya kusikiliza kesi za watoto hazina mazingira mazuri kwa ajili ya kuweka faragha kwa watoto wetu. Hatuna changamoto kubwa sana ya kisheria hapa, tuna changamoto kubwa sana ya usimamizi, utekelezaji na bajeti inayopelekwa kwenye Mahakama hizi ili kuweza kuweka faragha kwa watoto hawa ambao kesi zao zinasikilizwa Mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali, imezungumzia suala la kuasili watoto katika Ibara ya 60 ya marekebisho haya ya sheria. Imekwenda mbali kwa kutoa kesi ambazo zinahusiana au mashauri yanayohusiana na kuasili watoto na kupeleka katika Mahakama za Watoto. Bado tuna changamoto, Mahakama hizi za Watoto ni chache sana nchini na zilizopo hazina uwezo.

Mheshimiwa Spika, wamekwenda mbali, wanasema katika suala la kuasili watoto eti yule mzazi ambaye anadhani mtoto wake ambaye tayari ameshaasiliwa anaweza kwenda Mahakamani kuiomba Mahakama mtoto yule arudishwe kwa sababu ya kumlinda yule mtoto asipate ukatili wa kingono.

Mheshimiwa Spika, wote tunafahamu hapa, kwanza watu wengi wanaowatoa watoto hawa kwa ajili ya kwenda kuasiliwa wanawatoa kwa sababu hawana uwezo wa kuwalea; wengine wanawatoa kwa sababu mazingira waliyonayo si mazuri kwa ajili ya kulea watoto hawa. Yule anayeasili yule mtoto anakwenda kuwekeza, atamsomesha, wakati mwingine watoto hawa wanaandikwa mpaka kwenye mirathi ya mali za wale wanaoasili. Unampa haki yule mzazi kumchukua mtoto baada ya muda fulani kwa sababu ataweza ku-*establish* kwamba yule mtoto ananyanyaswa kingono. Yule mtu aliyemuasili yule mtoto na kuwekeza kwenye elimu, mali, nguvu na malezi, ananufaika vipi?

Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa na suala la kuwalinda watoto wetu wasiende kwenye ukatili, lakini tunapoziba mwanya mmoja, tusifungue mwanya mwingine. Mtu anaweza kwenda kumnyang'anya mtu mtoto wakati yule aliyeasili hana mtoto, anamtegemea yule mtoto kama mrithi wake, anamtegemea yule mtoto kama mlezi wake, anakwenda kuchukuliwa mtoto yule. Je, huyy tunamlinda vipi? Ni lazima tuweke taratibu kwa namna ya kudhibiti hilo.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko madogo ya Sheria Ibara ya 102 na 103, inaongelea suala la kumsaidia mtoto asichangamane na mahabusu au wafungwa wengine ambao ni watu wazima. Ni kweli, hivi hapa changamoto ni sheria au ni miundombinu mibovu ambayo tunayo? Ninavyoona selo zetu, kwa maana ya mahabusu, magereza yetu bado hayajatengenezewa miundombinu mizuri kwa ajili ya kuwasaidia watoto wetu. Hapa kuna changamoto ya kibajeti, kuna changamoto ya utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu wazima wanapokuwa wafungwa wanapewa kazi za mikono kwa ajili ya kufanya kazi hizo. Watoto hawa wanawezaje kuendelezwa katika mtaala wa elimu ili atakapoonekana hana hatia, arudi kwenye mfumo? Wanapelekewa walimu kule magerezani? Wana hosteli zao kwa ajili ya kukaa? Hapa tuna changamoto ya kiutendaji. Ni kweli tunaweza tusiwe na walimu wa kutosha kutembelea magereza yote, tunabadilisha sheria ya mtandao hapa, tunawezaje kutumia TEHAMA kwa ajili ya kuwasaidia watoto waliopo kwenye magereza na selo wakiwa wanasubiri hatma ya kesi zao ili waweze kupata elimu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo kiukweli nadhani Wizara ilikimbia kwenda kulifanya wakati hatuna maandalizi, niseme ni *pre-mature*, ni suala la kuhusisha Maafisa Ustawi wa Jamii kusikiliza makosa madogo madogo yanayohusiana na watoto. Hili naliangalia katika nyanja tatu. Nyanja ya kwanza, chombo cha mwisho kwa mujibu wa Katiba cha kutoa haki ambacho ni Mahakama, ukisema maafisa ustawi wa jamii watatoa haki, unakuwa umepoka ile nguvu ya Mahakama ya kikatiba ya kusimamia kesi.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, ni lazima tuwe na kifungu maalum kinachosema, kwamba kama mtu hatoridhishwa na uamuzi uliofanywa na Afisa Ustawi wa Jamii, anaweza kwenda Mahakamani. Hiyo namba moja, namba mbili, nimepita kwa haraka haraka, mimi si mjumbe wa Kamati; nini maana ya makosa madogo madogo, tafsiri yake hasa ni nini? Hasa kwenye mazingira ambayo Kamati yenyewe imesema tuna upungufu wa

95.3% wa Maafisa Ustawi wa Jamii? Wengi ambao wanafanya kazi ya Maafisa Ustawi wa Jamii ni polisi wa kike au polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unavyosema makosa haya ni madogo, unamaanisha nini? Ni lazima tutoe tafsiri ya makosa madogo ni nini, lakini ni lazima Mheshimiwa Waziri aje hapa kutueleza unatoa mamlaka makubwa namna hii, tena wamepewa na mamlaka mengine, kwamba kwenye Mahakama zote mashauri yote yanayohusu watoto, Ibara ya 115, ni lazima shauri hilo awepo Afisa Ustawi wa Jamii; tunamtoa wapi? Tuna upungufu wa zaidi ya 95% ya Maafisa Ustawi wa Jamii nchini, *leave alone commitment* aliyoiweka Mheshimiwa Waziri kwenye bajeti ya mwaka 2023 kama sikosei, alisema anakwenda kuajiri Maafisa Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna *confusion* kubwa sana, au anawalenga Maafisa Maendeleo ya Jamii ambao sisi TAMISEMI tumeshawapa kazi nyingine, sasa hivi wanaenda kusimamia mambo ya mikopo. Kwa hiyo watasimamia mikopo hao hao, mashauri ya watoto hao hao, watawezaje? Ni lazima tupate majibu, tusitunge sheria ilimradi inafurahisha kwenye karatasi, lakini kimsingi haitekelezeki. Hawa Maafisa Ustawi wa Jamii hawapo. Kwanza Serikali inakwenda kukwamisha mchakato mzima wa Mahakama na kuchelewesha kesi, yaani Aqwfisa Ustawi wa Jamii mwenyewe yuko mmoja ile Manispaa nzima ya Shinyanga, leo aende Mahakamani huku, kesho aende Mahakamani huku, hajasimamia kesi za ndoa, mara kuna ubakaji; ataweza wapi?

Mheshimiwa Spika, nataka nipate ufafanuzi, wanavyotunga sheria hii wanafikiria itatekelezekaje? Kwa sababu katika mazingira ya kawaida haitekelezeki kwa sababu hawa Maafisa Ustawi wa Jamii hawapo, bajeti tulishapitisha, hakuna tangazo lolote la Serikali linalotoa kibali cha ajira cha kuajiri angalau 50%, watawatoa wapi Maafisa Ustawi wa Jamii ili waweze kushiriki kwenye kesi zinazohusiana na ukatili kwa watoto wetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, wameleta mabadiliko hapa ya Sheria ya Mtandao, lakini ni lazima tujue ukatili wa kingono kwa wototo kupitia mitandao unaanzia wapi. Mimi Serikali hii sina

wasiwasi, najua ina wataalam wazuri sana. Wanatushauri nini sisi, wanakuja na mapendekezo gani kwenye mazingira ambayo watoto wadogo wanapewa na kutumia hizi simu janja? Najua, watoto ni lazima wapewe chombo cha mawasiliano ili waweze kutoa taarifa pale wanapodhani wametendewa ukatili hasa ukatili wa kingono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, simu zenyewe ndizo hizi hizi ambazo sasa hivi, yaani zinakupa pendekezo ingia huku, ingia huku, ndizo hizi hizi? Je, Wizara ina mkakati gani, ikishirikiana na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari wa kuhakikisha kwamba simu wanazopewa watoto kwa ajili ya usalama wao na kutoa taarifa haziingizi mambo ambayo hayaruhusiwi kuonwa na watoto chini ya miaka 18? Nchi zingine wameweka vizuri kabisa, wapewe zile *landline* ambazo zina namba na *toll free number* ya Wizara itakuwepo pale, yaani mtoto ana namba maalum za kupiga na atawasiliana kwa sababu maalum. Lakini sisi leo unakuta mtoto ana miaka sita, ana miaka mitano ana *smartphone*. Akiingia kwenye *smartphone*, nyumbani kuna *free Wi-Fi*, akiingia kwenye *free Wi-Fi* anaweza kuperuzi chochote anachokitaka wakati huo wazazi tupo ofisini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, atafuatiwa na Mheshimiwa Erick James Shigongo, Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu ajiandae.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa hii nafasi. Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na uzima na leo kusimama katika Bunge lako hili Tukufu kuweza kutunga sheria hii ya kumlinda mtoto.

Mheshimiwa Spika, kuna msemo wa Kiswahili unasema "udongo upate ulimaji". Huu msemo una utata kidogo, maana unaweza ukasema kwamba udongo upate ulimaji kwa ajili ya ufinyanzi na utaufinyanga vile unavyotaka, utaukunja unavyotaka kwa sababu umeupata udongo wa maji. Ukikauka inakuwa

huwezi kuusanifu unavyopenda. Pia udongo upate ulimaji, panapo udongo mzuri, ukipata mkulima anayelima vizuri, basi ule udongo utaleta manufaa na mazao bora.

Mheshimiwa Spika, sasa, tunapozungumzia mtoto, maana yake ni kwamba, "Kambale mkunje bado angali mbichi", ndicho ambacho nasema. Kuwalinda na kuwatunza watoto ili kuweza kuwafundisha mambo mazuri. Nataka kuchangia katika Sheria ya Makosa ya Kimtandao ambapo wengi wamegusa hapa. *Cyberterrorism* Ibara ya 7 ya marekebisho haya Kifungu Kipya cha 19A ambacho kinazungumzia hayo makosa ya kimtandao mpaka inapofika kifungu kidogo cha (1) hadi cha (4) ambapo imezungumzia mpaka adhabu ambayo itatolewa. Naipongeza sana Serikali kwa kuleta wazo hili pamoja na kuleta jedwali la marekebisho ambapo wameongeza kitu pale, kwa hiyo naipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Spika, zipo sababu nyingi sana za kuzuia hivi vitu au kufanya visitokee. Leo watoto wanaangalia vitu hivyo ambavyo hujui wanajifunza kitu gani, lakini matokeo yake unakuja kumwona mtu ameshakuwa kijana anaweza kuikamata silaha, akamudu, akapambana na jeshi zima yeye peke yake. Unajiuliza huyu alijua wapi?

Mheshimiwa Spika, ziko taarifa ambazo katika nchi hii, kuna vijana wanasafiri wanaondoka wanakwenda nchi za kigeni, nchi za jirani, wanakwenda huko na unakuja kumkuta amejiunga na kundi la ugaidi, alianzia wapi? Pia ziko taarifa za makundi mengine ambayo yanaanzishwa humu ndani kwetu yanakuja kupambana na nchi yao, unakuja kujiuliza hawa watu waliandaliwa vipi? Walikuzwa vipi? Sasa, kwa haya naunga mkono kwa Serikali kuweka hii adhabu. Ila tuangalie na tuchuje vizuri maana isije ikawa akaingizwa mtu ambaye hahusiki, akiingizwa mtu ambaye hausiki, hii sheria itakuwa imeshaharibu.

Mheshimiwa Spika, nina ushauri sasa kwa Serikali, ni kweli mtoto unapomkosesha jambo fulani, atafuata jambo lingine na ndipo pale tunaposema kwamba; "akilikosa la mama, atanyonya hata la punda". Sasa, je hili la mama anapewa? Sasa, kama la mama hapewi, atakwenda kunyonya la punda; na jambo la

kwenda kutazama vitu hivyo ni sawa na kwenda kunyonya la punda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niseme kwamba, Serikali ianze kuangalia, kuwanyima fursa vijana hawa au jamii ianze kuwanyima fursa vijana kwenda kuangalia hiyo mitandao na kuangalia hayo mambo mengine ambayo hayafai. Vinginevyo, tutakuja kulaumu bure, lakini kwa sababu tuliwaachia fursa pana ya kuweza kuangalia vitu hivyo.

Mheshimiwa Spika, halafu udhibiti wa usambazaji wa hivi vitu. Nchi nyingine huko, ikishafika muda fulani, mitandao hii haipatikani. Leo mtoto mpaka analala kitandani, anaperuzi anachotaka. *TCRA* mko wapi? Watu ambao mnashughulika na *cybercrime* mko wapi? Watu wanafanya hivyo vitu wanavyovitaka.

Mheshimiwa Spika, kingine ambacho nataka nikiseme, leo kila mahali pamejengwa. Zamani kwenye mtaa kuna sehemu ya kwenda kuchezea watoto. Tumeshawanyima watoto fursa ya kucheza, watoto watakimbilia nini? Tumewanyima watoto fursa ya kucheza, watoto sasa hawachezi. Enzi zetu sisi kiwanja cha mpira tuko pale watu 20 tunalindana sisi wenyewe kwa wenyewe, lakini sasa, viwanja vyote vya mtaani vimeshajengwa, tunawanyima watoto, sasa wanakimbilia huko kwenye mitandao kwa sababu unakwenda kwenye mtaa, wote umekuwa *blocked,* hakuna hata sehemu ya kucheza.

Mheshimiwa Spika, kingine, mambo ya michezo. Mambo ya michezo katika shule na katika mitaa yahamasishwe kwa sababu yatapunguza watoto kwenda kujishughulisha na mambo ambayo hayana maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine, vifaa ambavyo watoto wanatumia au programu ambazo watoto wanatumia ziwe *accessible*. Vinginevyo hizi programu za watoto zikikosekana watoto ndiyo watakwenda kuhusika na mambo hayo. Kwa hiyo hatua hizi kama tutazichukua, tutapunguza hili suala la watoto kuingia mitandaoni wakaangalia vitu vingine.

Mheshimiwa Spika, kingine, kuna michezo ya watoto kama bembea na vitu vingine; kwa nini visiondolewe kodi wakawekewa vile vitu ambavyo wanatavitaka watoto wakawa wanacheza, tukawadhibiti hawa watoto katika njia hiyo?

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kuchangia katika mapendekezo ya Sheria hii Ibara ya 27 ambayo imependekeza kifungu kipya cha 96A cha Mabaraza. Kwenye mabaraza hapa kumetajwa kwamba kuanzia la vijiji mpaka mkoa, TAMISEMI watashughulika na Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, lakini kuanzia Taifa, pale Wizara hii ndiyo itakayoshughulika. Wasiwasi wangu, hapa kuna *budget implication* katika Wizara ya TAMISEMI na katika Wizara hii. Siku zote hicho ni kilio ambacho nasema. Haya majukumu, kwamba hii sekta iko kwa Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, lakini sasa mlezi wa mabaraza ni TAMISEMI. Sasa, ikiwa mlezi wa mabaraza yale ni TAMISEMI, hii bajeti inawezekana Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii anataka lakini kule kwenye TAMISEMI siyo *priority* yao. Haya mabaraza yameanza kutajwa kuanzia vijiji na kuendelea na sheria yenyewe hii yote ukiitazama, wanatajwa Maafisa Ustawi wa Jamii, watashughulika na vitu ambavyo vipo.

Mheshimiwa Spika, amezungumzia pale dada yangu Mheshimiwa Salome, kuhusiana na mambo ya uajiri. Serikali imesema itaajiri Maafisa Ustawi 400; lakini Maafisa Ustawi wale 400 watakaoajiriwa ni kutokana na mwelekeo wa kule nyuma si kwa mujibu wa utungaji wa sheria hii. Sheria hii sasa imekuja na vitu vingine, wanahitajika watu zaidi ya 400. Ina maana kwamba, ajira kwa Maafisa Ustawi ni lazima na hapa *gap* imeshatajwa na Kamati, kwamba *gap* ilikuwa, na hii ni Ripoti ya *CAG* ndiyo inayosema hivi, kwamba kuna upungufu wa 95.3% ya Maafisa Ustawi. Tunaajiri pale lakini tutakwenda kufanya nini baada ya hapo?

Mheshimiwa Spika, lingine kabla ya kengele kulia nataka kuzungumzia masuala ya kuasili mtoto, kuasili mtoto kwa mgeni nilikuwa naona tuweke masharti; kwa nini tunasema kumlinda mtoto? Tunamlinda mtoto ili apate haki zake. Katika nchi yetu sisi haki za mtoto zinakuwa-*defined* tofauti na haki za mtoto

zinavyokuwa-*defined* katika nchi nyingine. Hivyo hapa katoka mtu Marekani akaenda kumuasili mtu Malawi, sitaji kwa majina lakini yule mtoto badala yake amekuwa kinyume kimaumbile, alikuwa mwanaume lakini sasa siyo mwanaume tena anavaa mpaka nguo za kike ni kutokana wao ile haki ya mtoto wana-*define* vipi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pamoja na kutoa miaka hiyo mitatu kwamba mtu akae achunguzwe, lakini tutazame, kuna mataifa, kwamba hata wale watu wabaya, hata wale mashoga wanapoandamana hapa ndio wanapokelewa huko. Sasa anakuja mtu anataka kuasili atakaa miaka mitatu si ana lengo lake haoni tabu, kwa sababu anasubiri afanikiwe aondoke na watu aende zake akafanye mambo yake. Kwa hiyo, katika kuasili, naomba tuangalie yale mazingira na utamaduni wa wale watu.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine, nataka ije sheria, itoe tafsiri hasa nini maana ya mtoto; maana anaweza akapigwa mtu ana mimba ya miezi sita halafu mama akaathirika na mtoto akafa na akaenda kuzikwa. Sasa je, huyu aliyekufa tumboni sio mtoto? Huyu mtoto hakupata chakula bora alikuwa na haki ya kupata chakula ili asiwe mdumavu, lakini bado ikiwa mama hakupata kitu kizuri, hakumtunza, hakwenda *clinic* kwa wakati mtoto akazaliwa akawa mdumavu, tumemkosesha haki ya kuja kuishi, baada ya kupata ule udumavu, ambao kaupata tumboni. Ila Mungu yeye ndio alisema kwamba amemuumba mwanadamu kutokea tumboni kwa mama yake kwa sababu hata na tabia zinatokea huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa na sisi tujaribu kutoa tafsiri ya mtoto na hata mtu hapa leo akienda kumpiga mjamzito ataambiwa kaua mtoto, sasa tuwe na tafsiri pana ya mtoto ili tujue kwamba mtoto ni nani? Tukianza kutokea *zero* mpaka 18 tujue huku nyuma pia iko hivyo hivyo, kwa sababu hata Mungu anasema kwamba msiwauwe watoto wenu kwa kuogopa shida. Kuogopa shida maana yake kwamba mtu amekwenda amefanya zinaa, halafu anaona aibu kisha anatoa mimba ndio ameua mtoto, kwa Mungu iko hivyo. Sasa sisi mtoto tunam-*define* vipi? Naomba sisi kama Taifa hili tum-*define* mtoto vizuri apate haki zake, kwa sababu pia tunakumbana na tatizo la udumavu wa watoto na udumavu huo tutakuja kuzaa Taifa ambalo litakuwa sio zuri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ila itakapofika katika Ibara ya 7 ya mapendekezo katika kupitisha kwenye Kamati kuna jambo nitaomba kidogo nichangie. Nashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Eric James Shigongo atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu na Mheshimiwa Daktari Pindi Hazara Chana ajiandae.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kumshukuru Mungu kwa kunipa nafasi ya kusimama ndani ya Bunge hili kutimiza wajibu wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana na nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu nzima ya Wizara yake na Kamati kwa ujumla kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa mabadiliko ya Miswada hii mitatu. Wamefanya kazi nzuri, wanastahili pongezi na mimi binafsi kabla sijazungumza sana, naomba niunge mkono hoja. Nimesoma sheria hizi nakubali mabadiliko yote tuyapitishe na yakafanye kazi kuokoa maisha ya mtoto wa kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Daktari Samia Suluhu Hassan alipoingia tu madarakani, alifanya jambo moja kubwa, ambalo Watanzania wote tulishuhudia kuonyesha kwamba, kweli amedhamiria kumlinda mtoto wa kitanzania.  Mara moja akishirikiana na *TCRA* wali-*burn* mitandao yote ya *pornography* kwenye Taifa letu. Baadhi ya watu walianza kulalamika, kama yale mambo hayaonekani, haya mambo hayaonekani, kwa sababu Mheshimiwa Rais aliamua kulinda watoto wa nchi hii, nampongeza sana kwa jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa kama baba wa watoto ambao kila siku nataka wakue waje wawe watoto wenye faida kwa familia, kwa Taifa na kwa ulimwengu. Kwa hiyo, kama mzazi nitaongea kwa nafasi yangu, maana ninalo jukumu la kutimiza wajibu wangu wa kuwalinda watoto wangu na kulinda watoto wa Taifa hili ili kusudi waweze kuja kuwa faida kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sisi wote hapa ni matunda ya watu walioishi kabla yetu, mimi ni matunda ya wazazi wangu, ni matunda ya wazee wetu wa mwanzo Mwalimu Nyerere na wenzake ambao kwa ujumla wao walitunga sheria, walitunga kanuni ambazo zimenifanya niwe raia niliyeko hapa. Kama ni raia mzuri sifa zote zinaenda kwao kwa kazi nzuri waliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi pia nina wajibu kwa watakaofuata baada ya mimi, ndio maana niko ndani ya Bunge hili Tukufu natunga sheria kuwalinda wale ambao watafuata baada ya kizazi changu. Kama walivyofanya waliotangulia na mimi niko ndani ya Bunge kufanya kwa wale watakaokuja baada ya mimi, nafikiri ndio kazi yetu na ndio maana tupo mahali hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nahisi nina wajibu wa kufanya jambo hilo siku ya leo kwa kutunga sheria, kutunga sheria ndio kazi yangu ndani ya Bunge hili na katika sheria hizi nimezisoma kwa kweli nakubali kabisa, tunao wajibu wa kuwalinda watoto wetu ili wasije wakaharibika.

Mheshimiwa Spika, hakuna mama hata mmoja ambaye huwa anazaa jambazi, wakasema leo mama fulani amezaa jambazi, leo mama fulani amezaa mwizi, leo mama fulani amezaa daktari, hapana wanawake wote huwa wanazaa Watoto, lakini hawa majambazi huwa wanatoka wapi? Hawa wezi huwa wanatoka wapi? Hawa wezi wanatengenezwa na mazingira katika kukua. Mtoto alitakiwa kuwa Daktari anaishia kuwa jambazi, alitakiwa kuwa *Engineer* anaishia kuwa kibaka, alitakiwa kuwa mchungaji anaishia kuwa mtumiaji wa madawa ya kulevya, mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukishindwa kutimiza wajibu wetu kama Bunge wa kuwalinda watoto wetu waliotarajiwa kuwa madaktari wataishia kuwa mtaani wanavuta madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Spika, nafurahi sana kuwa sehemu ya mchakato huu, nafurahi sana kuwa nashiriki kutunga sheria ambayo itamlinda mtoto wangu, itamlinda mtoto wa Mheshimiwa Kunambi ili aweze kuwa mtoto mzuri siku za baadaye aweze kutumikia nchi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watoto hawa huzaliwa hawajui chochote, wanaingia duniani hawajui chochote, ni kama *sponge* ikitiwa maji inajaa wanakuja watoto wazuri kabisa, lakini katika kukua kwetu mambo tunayowatendea, mambo tunayowaonesha watoto wetum wanabadilika, wanaharibika wanakuwa tofauti. Nimekutana na akinamama wanalia, nimekutana na wazazi wanalia, watoto wao wameharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi hii tunayoifanya leo ni kazi ya msingi sana kusaidia watoto wa Taifa hili ili waweze kuwa na faida kwa nchi yetu. Kazi hii nitaifanya kwa uaminifu wangu wote kwa sababu najua kama sisi tuliomo humu ndani leo tuna faida kwa nchi yetu na sisi tutengeneze watoto ambao watakuwa faida kwa nchi yetu miaka 30 ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukatae tukubali, miaka 100 ijayo, wote tutakuwa tumeshakufa, hakuna mtu hapa ndani atakuwa hai miaka 100 ijayo, wote tutakuwa tumeshakufa. Lakini nchi hii itakuwepo na watakuwepo watu wapya kwenye nchi hii, ambao wataangalia nyuma maamuzi tuliyoyafanya wakasema maamuzi yaliyofanywa na Bunge la Daktari Tulia Ackson Mwansasu yametusaidia kuwa watoto bora. Ndio maana nasimama hapa kwa ujasiri kabisa kukupongeza wewe, kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kutuletea Miswada hii, tupitisheni sheria hizi zikasaidie nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina ushauri wa mambo manne tu, ili niweze kuokoa muda niwape na wenzangu wazungumze.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, tunaishi kwenye nyakati za tofauti, tunahitaji maamuzi ya tofauti, wazungu husema *we live in extra ordinary times; we need extra ordinary decisions,* kwa hiyo, tuko kwenye nyakati tofauti, maamuzi yawe tofauti, Sheria zetu hizi ziwe tofauti, ziendane na wakati. Miaka 10 iliyopita hapakuwa na *TikTok,* miaka kumi iliyopita hapakuwa na *snapchat,* leo hii tunatunga sheria huwezi ukajua kesho asubuhi wenzetu watagundua nini. Kwa hiyo, kesho wanaweza kuja na *Taptap, Taptap* hiyo ambayo inaharibu maisha ya watoto wetu. Suala la

kubadili sheria, suala la kurekebisha sheria lazima liwe ni suala la mwendelezo.

Mheshimiwa Spika, tunabadilisha leo, kesho asubuhi wazungu wakituletea jambo la tofauti linaloharibu watoto wetu, Mheshimiwa Waziri alete sheria kesho asubuhi tubadilishe hapa. Mwisho wa siku ni lazima tulinde akili za watoto wetu ili waweze kuwa watoto sahihi. Tuna sheria hizi tatu, nimefurahi sana nimesoma, sio mjumbe wa Kamati, mwanasheria wangu hapa Mheshimiwa Taya alikuwa ananieleza, ananifundisha mambo mbalimbali ya kisheria, nimesoma amenipitisha, nimeelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina ombi moja kwa Waheshimiwa Wabunge, tuilete hapa Sheria ya Vileo, Sheria ya Vileo tuipitie. Haiwezekani kwenye Taifa hili inataka kufika mahali kama tunatengeneza jamii ya watoto watumiaji wa pombe na walevi, haiwezekani! Waziri alete sheria ya vileo hapa tuifanyie marekebisho. Pombe zimekuwa bidhaa ya bei rahisi sana kwenye Taifa letu, kuna pombe za 500, mtoto anaenda shule ananunua kinaitwa kisungura kwenye duka la Mangi na Mangi anauza hiyo pombe wala hana leseni. Leseni ya vileo ipo, halmashauri zetu zipo wala hazisimamii, watoto wetu wanaishia kutumia madawa, wanakuwa walevi wa pombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pombe badala ya kuuzwa kwa bei kubwa inauzwa 500, hebu fikiria 500, mwanangu nikimpa nauli anachukua 500 anaenda shuleni na mfuko wa madaftari anaenda kwa Mangi ambaye hana leseni anapimiwa na siku hizi inapimwa anakunywa anaenda shule amelewa. Hapana! Sheria tatu tunazirekebisha, Waziri alete Sheria ya Vileo hapa tuipitie na yenyewe tusaidie watoto wetu. Tusipowalinda watoto wetu, wataishia kuwa tofauti sana na tunavyotarajia na rahisi sana kusema watoto wangu mimi hawawezi kupatwa na matatizo haya, ni rahisi kusema hivyo mtoto wangu hawezi kuvuta unga. *No one is safe anywhere, anytime*. Sisi hapa tuliokuwa hapa kesho asubuhi tusipobadilisha sheria watoto wenyewe wataumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sitaki jambo hili litokee kwa mwanangu, sitaki jambo hili litokee kwa Mbunge yeyote, naomba sheria ziendelee kuletwa tuendelee kuzibadilisha. Wazazi wa nchi hii wanisikilize, wasiiachie Serikali peke yake watoto wetu, hapa ndani tutatunga sheria nzuri sana, lakini sheria pekee haitoshi, wazazi tutimize wajibu wetu kwa watoto. Tupeleke watoto wetu kanisani, tupeleke watoto misikitini wajifunze hofu ya Mungu, itatusaidia sana kutengeneza Taifa la watoto ambao watakuwa na faida kwa nchi yetu. Haiwezekani mzazi yupo tu anasema Serikali imetunga sheria nzuri sana leo ya *protection* ya mtoto, halafu yeye amekaa tu. Anaacha mtoto wake muda wote yuko kwenye mitandao, anasoma mambo mbalimbali, mwisho wa siku anasoma mambo yanayom-*radicalize*, mtoto anakuwa *radical,* kwani magaidi walitokeaje? Watoto wetu walikutana na *content* kwenye mtandao zinawabadilisha akili, wazazi tutimize wajibu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho ni *child labour,* tuwakinge watoto wetu dhidi ya kufanya kazi ambazo sio sawasawa. Umoja wa Mataifa walipitisha Azimio mwaka 1990 la kum-*protect* mtoto. Miongoni mwa maazimio kwenye ile *Article 41* iko moja inazuia ajira kwa watoto, tuwalindeni watoto wetu dhidi ya ajira kwa watoto.

Mheshimiwa Spika, ukipita Mwenge sasa hivi Dar es Salaam kwenye mataa, kuna watoto wadogo wanaosha vioo vya magari. Kwa sheria tuwaondoe watoto barabarani tuwapeleke shuleni, *RC* anapita hapo hapo, *DC* anapita hapo hapo, *RPC* anapita hapo hapo, watoto pale Mwenge wako wengi tu, Mwanza *Hotel* pale Mwanza wako wengi tu, lazima tuwasaidie watoto wetu wawe watoto bora, kwa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kusema jambo moja tu. Wabunge tuna kazi moja tu ya kuitumikia nchi yetu kwa moyo wetu wote, akili zetu zote ili tuweze kusaidia kizazi kijacho cha nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ahsante kwa kunipa nafasi Mungu akubariki sana. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu atafuatiwa na Mheshimiwa Daktari Pindi Chana, mtoa hoja ajiandae.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Niwapongeze Wizara kwa huu mwanzo ambao tumeanza, lakini nikubaliane na Kamati kwa yale mapendekezo yao na hasa lile pendekezo la kwanza linalosema, sheria zote zinazohusiana na masuala ya watoto zipitiwe upya, kwa lengo la kuhusianisha na kusomana kulingana na mazingira ya sasa.

Mheshimiwa Spika, tunapoongelea kuwalinda watoto, lazima pia tuangalie hawa watoto wanatoka wapi. Sisi kama viongozi, wajibu wetu ni kuona kama wale ambao walileta watoto kuna sehemu fulani haziendi sawa ndio tutengeneze utaratibu wa kuwasaidia ili kuona namna ambavyo hawa watoto wanaweza kuwa salama. Leo tunaandika hapa, wamesema Waheshimiwa Wabunge, tuna sheria, tunataka watoto wasijihusishe na masuala ya *phonology,* watoto wasitumiwe kwenye masuala ya *terrorisms.* Tunatengeneza hii sheria kuwalinda, lakini mlinzi wa kwanza kabisa wa huyu mtoto ni yule ambaye alimleta duniani. Bahati nzuri Mwenyezi Mungu amempa uwezo yule aliyemleta duniani, aweze kuwa na nafasi naye kwa wakati wote na kuweza kum-*groom* na kutoa maelekezo na kuzisaidia hizi Serikali kuandaa sheria ili kumsaidia mtoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo mambo yanayofanyika kwenye *level* za familia zetu, kwenye ndoa zetu ambazo hata tukitunga sheria gani humu, kama wale wenyewe walioleta yule mtoto duniani hawajajua wajibu wao, bado watoto wataendelea kuwa kwenye mazingira hatarishi mno. Sisi tutasaidia kwa namna ambavyo tunasaidia, lakini ingeletwa kwanza ile sheria ya ndoa yenyewe tuisuke. Kasema Mheshimiwa mmoja hapa, sasa hivi tunajadili Watoto, lakini kwa Tanzania tunautegemea mhimili wa mahakama usimamie Sheria ya Watoto. Ukifika mahakamani pale pale wanapata mkinzano kati ya Sheria ya Ndoa na hii inayotambua mtoto ana umri gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi ni wajibu wetu kuzitunga sheria hizi, amesema vizuri Mwanasheria Mheshimiwa Salome, mimi bahati mbaya siyo Mwanasheria, yeye ameielezea vizuri, lakini sisi wajibu wetu ni kuhakikisha tumeweka sawa na Kamati hapa inasema kwa mazingira ya sasa tuhakikishe sheria hizi zote zinabadilishwa. Leo tuelezane zamani ilikuwa ni haki kweli na kutokana na mazingira yalivyokuwa yamejengwa watoto umri waliokuwa wanakwenda shule; unakuta watu wengine walikuwa wanakwenda shule wakiwa watu wazima sana. Shule zenyewe zilikuwa ni chache, shule zenyewe zilikuwa mbali. Watoto wenyewe kukutana, yaani binadamu kwa binadamu kukutana ilikuwa pia haiwezekani kirahisi.

Mheshimiwa Spika, ndio maana wakati fulani hata mzazi alikuwa anaweza kupewa *power,* kwamba anaweza akamshawishi mtoto au akamtafutia mtoto mume au mke, lakini kwa mazingira ya sasa watoto wameshapewa fursa ya kusoma, mazingira yameshawekwa, Serikali imeshajenga, tumeshasema *compulsory education* ni mpaka kidato cha nne tunaelekea kidato cha sita, kuna sababu gani ya kuendelea tena kulea sheria kwamba bado tusitambue umri wa mtoto kwamba ni chini ya miaka 18, mtoto ni miaka 18, ili kumpa mzazi wajibu ajue anawajibika kumsimamia huyo mtoto mpaka amalize elimu yake ya msingi ya kidato cha nne awe amefikisha miaka 18.

Mheshimiwa Spika, leo tuna Sheria ya Ndoa imewekwa watu waoane na watu wataingia kwenye ndoa na kuna nyingine ambayo kuzalisha watoto kunakuwa nje ya utaratibu wa ndoa. Yaani watoto wanaweza wakazaliwa tu ndani ya ndoa na nje ya utaratibu wa ndoa. Lazima tuje hapa tuweke utaratibu, mtu yeyote aliyeamua kuzalisha tunda ambalo ni mtoto, atamlea vipi? Uwe ulimzalisha ndani ya ndoa au nje ya ndoa. Watu wanaingia kwenye ndoa wanaamua tumekaa miaka miwili, mitatu tumezaa watoto wetu, mtu anaamua tu anamwacha mtoto wa umri wa mwaka mmoja anampeleka kulelewa na bibi yake yeye, anaamua kuolewa tena, anaanzisha familia nyingine.

Mheshimiwa Spika, Sheria inambanaje huyu? Kuhakikisha amem-*support* mtoto wake mpaka kufika umri anaoweza kujitegemea kukaa mwenyewe. Hivi ndio vitu tunatakiwa tuje

tuisuke ile upya hapa. Sawa achaneni wewe umeona huyu hafai, umeamua kuachana lakini sisi tunachotaka hili tunda mlilozalisha lifikisheni katika hatua ya kukomaa. Wewe dada utatakiwa huyu mtoto uvumilie usubiri mmemlea afike miaka saba na wewe bwana vumilia miaka saba mpaka mtoto wenu atakapofika katika hatua nzuri mumlee kwa pamoja, ndiyo hiyo wanayosema *co-parenting,* mumlee kwa pamoja mpaka mtoto afikie hatua nzuri. Ndiyo maana leo kwenye majumba yetu kumekuwa makaburi ya watoto wetu. Unaongelea mtoto kwenda kujifunza kuwa gaidi, wakati mzazi uko wapi? Unaongelea mtoto kutumika kwenye *ponology* wakati wewe mzazi uko wapi? Unaongelea mtoto kuingizwa kwenye makundi ya kijambazi, mpaka mtoto anaingizwa kwenye makundi ya kijambazi uko wapi?

Mheshimiwa Spika, sasa hivi watoto wanatumika, tumeongelea hapa, hii Sheria imeeleza vizuri sana kutaka kum-*pinch* hata yule anayetumia *advantage* kwa sababu tu, anategemea akamtumie hata kwenye biashara haramu. Leo tuna watoto wa mitaani wanatumika, kwa ajili ya kuuza dawa za kulevya, wamekuwa *traffickers* wale, lakini wametumika kwa sababu ya ile hali yao ya kuwa hawawezi kujitegemea. Wanataka apewe afanye kila kitu, ili ale, lakini yule mzazi yuko wapi?

Mheshimiwa Spika, nimepata kesi moja Iringa, mama ananipigia simu mtoto wangu amebakwa na jirani yangu, ana miaka mingapi? Miwili. Amebakwa na jirani yangu alikuwa amelala na kaka yake wa miaka tisa sijui, kumi na moja. Nikamuuliza wewe ulikuwa wapi mpaka mtoto anabakwa? Usiku mzima wewe ulikuwa wapi?

Mheshimiwa Spika, anasema mimi nilienda kazini nikakosa nauli kurudi kwa hiyo, nikamwacha mtoto. Huo ndiyo uzazi sasa, ndiyo aina ya watu tulionao, lakini leo wanakwenda hizi Sheria zetu za Maendeleo ya Jamii, mtu anakwenda Maendeleo ya Jamii wanampigia hesabu. Wewe mshahara wako kwa sababu, mume wako ana kipato cha kuzalisha tu laki moja kwa mwezi, kwa hiyo, hela anayotakiwa achangie familia ni shilingi elfu kumi kwa mwezi, amemwachia mwenzie watoto watatu. Hiyo elfu

inamsaidiaje sasa yule mama anayekwenda kupewa elfu kumi, ili asaidie wale watoto? Inamsadiaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya ndiyo mambo. Inatakiwa ile Sheria iletwe hapa isukwe watu wajue kabisa, mtu ajue. Mtu mzima anapenda kukutana na watu wazima wa aina mbili, mwanaume na mwanamke, wajue watazalisha tunda ambalo ni mtoto na wakizalisha tunda ambalo ni mtoto, Serikali inawataka wao wafanye.

Mheshimiwa Spika, leo wananchi wanaondoka wanakwenda kuchoma Kituo cha Polisi, wanakwenda kupiga gari la Polisi kwa sababu, mtoto amepotea haonekani. Wewe ulikuwa wapi mpaka mtoto amepotea? Kwa hiyo, tunategemea kwamba, watoto hawa wasipotee, itakuwa ni wajibu wa Polisi kuangalia mtoto ametoka ameenda shule, amerudi, hii itawezekana vipi? Haiwezekani, ukitaka Serikali ndiyo ikutunzie watoto inakutunzia vipi? Kwa hiyo, Sheria inayotakiwa ije hapa, pamoja na kupitisha hii, ije Sheria ya Ndoa tuisuke upya hapa. Watu wawe wanajua tukishakutana kwenye uroda tutazalisha tunda ambalo ni mtoto, tuna wajibu wa kumtunza. Na kama ni mtoto kazaa mtoto tujue nani atakuwa *responsible* kumtunza yule mtoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu wanazaa watoto wanawarudisha kwa akinabibi vijijini, bibi mwenyewe analelewa na *TASAF*. Ukimuuliza, mama ameondoka ameacha mtoto wake ameenda kuolewa, baba ameacha mke wake naye ameenda kuoa. Wameanzisha kila mtu familia, wanatuzalia tena watu wengine kule, wataanzisha tena na huyo anazaa, wataachana tena, wataendelea, wanatuachia *TASAF*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunamchukua bibi, tunamchukua babu, tunachukua na wategemezi wake, mtu yuko kule anaendelea kuzaa, anaendelea kuzaa. Haiwezekani, lazima tufike kama viongozi tukubaliane inawezekana kwa sababu na sisi humu siyo malaika, inawezekana tumo, lakini hata kama tumo tutungiane sheria. Ukishazaa mtoto wako hakikisha mtoto huyo na wazazi wawe *responsible*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa tumeweka kwenye *software,* tunawaangalia wanaharibiwa kwenye *computer* kwenye *hardware? Software* ndiyo hii *phonograph,* si ndiyo? Kwenye *hardware* nyumbani, nani anamwangalia? Anajifunza matendo ya ngono kwenye nini? Anajifunza matendo ya ngono kwenye *software,* si ndiyo? Kwenye *hardware?* Nyumbani mama ameingiza mchepuko? Baba ameingiza mchepuko, tumeziba vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu watoto wa siku hizi wana akili. Wewe unafikiri mtoto wa siku hizi, mmekaa wewe una chumba kimoja, mmepanga, mmelala huko chumbani, yeye mmemlaza sebuleni, unafikiri anawasubiri, ninyi mnaendelea huko na mambo yenu, anawasubiri, anakuja anachungulia kinachoendelea ni nini? Haya tunatunga sheria ya kuwatetea kwenye *soft copy,* kwenye *hardware* inakuwaje? Mitaani inakuaje? Watu inakuaje wanafanya mapenzi barabarani? Kwenye miti? Watu wanafanya mapenzi nyumbani sebuleni, inakuaje? Watoto watalelewaje?

Mheshimiwa Spika, Sheria hii tumetunga, tumesema hapa kwamba, mtoto atengwe asiishi na mzazi mhalifu hata kama ni ndugu. Sasa, yaani atatengwa vipi? Kuna mababa majambazi wanaishi na watoto wao, Sheria inataka tutunge mtoto asiruhusiwe kuchangamana na wahalifu, baba yake jambazi, baba yake mwenyewe mbakaji, yuko mle mle ndani, tunawatenga vipi? Yaani, hapa hatuwezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa ni kuwawajibisha waliomleta mtoto duniani kwanza na sasa hivi tumekwenda mbali sana *DNA* zipo. Mtu kama hujafanana na mtoto wako kama mtoto wa nanii, kama watoto wale wa nunu wanafanana sana, wale *kitten,* wale watoto wa paka. Kama hujafanana na mtoto wako tunakupima damu, huyu mtoto ni wa fulani, halafu wewe mtoto si huyu wa kwako. Mzee sikiliza wala siye hatuna umaarufu wako na ujanja wako bwana, tunakushukuru sana kwa sababu, utaratibu upo, unaweza ukatumia njia hii upate mtoto, hutaki, kuna njia za kutumia usipate mtoto. Ulikuwa una nia ya kumpata huyu mtoto, sasa bahati mbaya au siyo bahati mbaya utajua wewe, sisi tunachotaka mtoto huyu asome. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, iletwe sheria hapa mtoto anakuwa adapted. Leo Afrika mambo ya ku-*adapt* yapo kweli, lakini siyo kihivyo na tunatesana tu, mtu mwingine yuko kijijini, mtu mwingine yupo mjini, ana kazi ya kuzaa. Huyu atatunzwa na mjomba wake, anaongeza, mwaka huu atapelekwa kwa shangazi yake, anaongeza, mwaka huu nampeleka kwa bibi yake, anaongeza. Watu wakiwajibishwa watapunguza mambo hayo, ili sasa tuwe na jamii inayoeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata mtoto analewa, visungura muda wote. Jamani watoto wanakwenda shuleni, mwalimu ndiyo anajua mtoto anabakwa, miezi miwili mzazi anayeishi naye hajui kama mtoto ameingiliwa? Halafu hatumwajibishi? Walimu wengine wanamuita mzazi wanamwambia, unajua mtoto wako ana tatizo? anasema mtoto wangu mie hawezi kuwa hivi. Anakwenda kupimwa anaonekana mtoto amebakwa miezi zaidi ya mitatu, mzazi nyumbani hujui; humuogeshi mtoto, humuangalii mtoto na ukatili.

Mheshimiwa Spika, Serikali walete Sheria hapa ya Ukatili wa Ndoa. Ukatili wa ndoa ndiyo chanzo cha mambo yote haya, kama umekubali kuolewa ujue umekubali kuolewa kwa sababu ya kuhusiana kiunyumba siyo kutafuta hela wala siyo kutafuta magari wala nguo kwa sababu, hata kwa baba yako ungepata hela, ungepata magari, ungepata nguo, pale umekuja, kwa ajili ya tendo la ndoa. Unakataa kutoa tendo la ndoa, baba anaingia kumbaka mtoto, unakataa kutoa tendo la ndoa anaingia mitaani anatuharibia watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watoto wetu wa shule wadogo wadogo wanaanza kuwa-*seduced,* anawapa ujauzito kabla ya umri. Sasa kama umeingia kwenye ndoa kubali kutoa tendo la ndoa, hutaki kutoa tendo la ndoa, sema mimi sitaki ndoa, bwana huyu apate fursa. Nitaambiwa sasa hasa nawatetea wanaume, bwana huyu apate fursa ya kuoa mke mwingine. Ndicho kilichopo na wewe baba umekubali kuoa, hakikisha unatekeleza wajibu wako ili tutoe ukatili. Kwa sababu, watu wanatoka na mahamuhamu yao, kwenye ndoa wamefanyiana ukatili, wanamalizia kwa watoto wetu. Tunajiuliza baba huyu anawezaje kubaka mtoto wa miezi mitatu, lakini ametoka pale ana mahamuhamu, hana lolote, akili

imeshajizima *data*, anamwingilia mtoto wa miaka miwili. Tuanze na wale walioleta mtoto duniani, tu-*deal* na hardware kabla hatujaenda kwenye *softcopy*. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca, makofi yamekuwa mengi. Kwa hivyo, nashindwa kuweka vizuri jambo moja hivi; lakini la kwanza kuna neno ulikuwa unalisema sasa, ili mtu atakayekuja kusoma Taarifa Rasmi za Bunge aelewe ulikuwa unasema nini? Kuna neno ulikuwa unasema *phonology,* ulikusudia kusema *pornography?*

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, nakusudia kusema *pornography* zile. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Haya ahsante. Jambo lingine, siyo lako wewe ni la kwangu mimi kwa sababu, ndiyo naongoza mjadala.

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na yote yaliyosemwa hakuna sababu, yoyote inayoweza kumwongoza huyu mwanaume kwenda kufanya ukatili kwa mtoto kwa sababu tu, kuna jambo limetokea mle ndani. Yaani hiyo yeye amesema aonavyo, lakini hakuna sababu, yoyote kwa kweli, hakuna sababu yoyote, nilikuwa natafuta neno la Kiswahili, lakini tunatunga leo Sheria hii kwa Kiingereza. Kwa hiyo, naruhusiwa kuweka neno la Kiingereza hapo, hakuna *justification* yoyote ambayo inamfanya huyu aende huko aendako, asiende kabisa na asijaribu.

Waheshimiwa Wabunge, nilishamtaja Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana. Mtoa hoja ajiandae.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba niunge mkono hoja na nimesimama kuelezea yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa michango yote ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge na ninazungumza toka Meza ya *Chief Whip,* Serikali imesikia na tutaendelea kuboresha. Yako masuala ya kuangalia upande wa kodi, labda vifaa vya michezo vya watoto, mabembea, Serikali imeshaanza kuangalia namna ya kupunguza kodi na

tumeshafanya upande wa taulo za watoto wa kike na huo upande wa kodi tutaendelea, lakini yako maeneo mengi ya maboresho ambayo Waheshimiwa wengi wamezungumza. Serikali imesikia na tutaendelea kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, nizungumze kuhusu Mahakama. Hivi sasa tumeendelea kuboresha sana Mhimili wa Mahakama zikiwemo Mahakama za Watoto. Sasa hivi kuna kitu kinaitwa *backlog,* mlundikano wa kesi, kwa upande wa Mahakama za Watoto kesi zote huchukua takribani miezi sita kukamilika. Mpaka sasa tuna *backlog* ya kesi takribani 49 kwenye Mahakama za Watoto. Kwa hiyo, *backlog* tunaita 0.1, lakini Mahakama za kawaida tumeharakisha sana maamuzi, tuna *backlog* ya *almost* asilimia tatu.

Mheshimiwa Spika, katika Mahakama za Watoto tunatumia Maafisa Ustawi wa Jamii ambao kimsingi siyo waajiriwa wa Mahakama. Hawa wanakuwa ni waajiriwa wa upande wa Wilaya ndiyo ambao wanatumika, lakini hoja nyingi hapa zimetolewa namna gani tuendelee kuboresha.

Mheshimiwa Spika, tunazo Mahakama takribani katika Wilaya 137 nchini ambako kote kwenye Mahakama zetu kuna Mahakama za Watoto, tunaendelea kuboresha Majengo ya Mahakama. Sote ni mashahidi tunaendelea kuhakikisha maamuzi yanatoka haraka katika Mahakama zetu, hususani maamuzi yanayohusu watoto kwa sababu, Serikali inafahamu watoto wana haki ya elimu.

Mheshimiwa Spika, pia, katika Mahakama zetu tumeanza kufunga/tumefunga *video conference* kiasi kwamba, kuna kesi zinaweza zikaendeshwa wakati wale watuhumiwa au wahalifu wakiwa bado magerezani na kulikuwa kuna hoja, tuone ni namna gani sasa tunaendelea kutumia *e-learning* watoto wakiwa katika vifungo vyao. Magereza waone kuwepo na haki ya wao kupata elimu, hayo yote ni maboresho ambayo kimsingi tunaendelea nayo.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa

kuendelea kuteua Majaji na Mahakimu ambao wanasimamia kesi hizi za watoto na Jaji Mkuu kwa kusimamia vizuri sana Mahakama za Watoto na hivi tunaendelea vizuri. Msajili anaendelea vizuri na Mtendaji wa Mahakama kuhakikisha kwamba, Mahakama zetu, hususani zinazosimamia kesi za watoto, zinaendelea vizuri kabisa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo kuna hoja mbalimbali zimetolewa, namna gani ya kudhibiti mitandao na uharibifu wa mitandao, hususani kwa watoto. Nashukuru sana Wizara yetu ya Habari na Mawasiliano imeendelea kufanya hivyo na hivi sasa mnafahamu kuna baadhi ya *link* zimeendelea kuzuiliwa, kwa ajili ya kuwalinda watoto wetu, ikiwa ni jukumu letu kuhakikisha kwamba, watoto wanakua salama.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo limezungumzwa hapa kutoka kwenye Kamati ni kuona namna gani Serikali inaendelea kuleta Sheria zinazohusu watoto, ili ziendelee kuboreshwa. Haya yamesemwa na kamati na sisi, kama Serikali na Mwanasheria Mkuu, tuko naye hapa na yeye nampongeza sana kwa kazi kubwa nzuri. Tutahakikisha Sheria mbalimbali zinazohusu watoto katika maeneo mbalimbali zinaendelea kuletwa na zinaendelea kuboreshwa kwa maslahi ya kuhakikisha kwamba, watoto wanalindwa.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe mwenyewe umetuwekea Kamati ya Sheria Ndogo, umetuwekea Kamati ya Katiba na Sheria, umetuwekea Bunge Maalum, lina kipindi cha Miswada ya Sheria na hivi sasa tuko katika Bunge la Miswada ya Sheria. Kwa hiyo, sisi kama Serikali ni wajibu wetu kuhakikisha tunaleta Sheria Bungeni ambazo zinafanyiwa maboresho ili ziweze kuendana na wakati huu wa sasa ambao tunaenda nao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima uje uhitimishe hoja yako.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa

fursa hii tena kuja kuhitimisha hoja yangu ambayo nilikuwa nimeianza siku ya leo. Naomba nianze kumshukuru tena Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kama ambavyo imesemwa hapa na Waheshimiwa Wabunge kwa kuianzisha Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum yenye umri sasa wa miaka miwili na miezi nane.

Mheshimiwa Spika, kwa kudra za Mwenyezi Mungu tumeweza kufanya yale tuliyoyafanya na sasa tumeleta huu Muswada wa Sheria mbele ya Bunge lako Tukufu. Sote tutakubaliana kwamba, changamoto za dunia ya leo zinatuonyesha jinsi gani Mheshimiwa Rais alifanya uamuzi sahihi, uamuzi makini, kwa wakati muafaka kwamba, kuwe na Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi tu sisi tutaendelea kuwa wasikivu katika kutekeleza maelekezo yake mwenyewe Mheshimiwa Rais, viongozi wote wa kitaifa pamoja na yote yanayotolewa na viongozi wote, ukiwepo wewe mwenyewe kwenye Bunge lako Tukufu. Michango na maelekezo mnayoyatoa yameleta msukumo mkubwa sana katika kufanikisha haya tunayoyafanikisha na hata hili la leo hii ni kazi ya kwenu Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, naomba tena niishukuru Kamati yangu ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Ustawi na Maendeleo ya Jamii, chini ya uongozi makini wa Mheshimiwa Fatma Toufiq, Mbunge, pamoja na Mheshimiwa Lulida, Makamu wake, kwa jinsi ambavyo wamekuwa wakituongoza. Kufikia hapa wameuchambua huu Muswada siku nyingi huko nyuma, ni kazi ya mikono yao, tunasema ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge wote waliochangia ahsanteni sana. Jumla ya Wabunge tisa wameweza kuchangia, wametoa maoni mazito, maoni makubwa ambayo pia, yameendelea kufungua zaidi mwelekeo wa fikra zetu, kama Wizara na kama Serikali, twende vipi katika eneo hili la kuboresha ulinzi kwa watoto. Nakiri kuwa, michango yenu makini tumeipokea, tutaitumia kwenye kuendelea kuandaa Kanuni za Utekelezaji wa

Sheria hii na naamini kabisa Muswada mtaupitisha, lakini pia, katika kuandaa Sheria nyingine endelevu.

Mheshimiwa Spika, kwa mjadala ulioenda hapa tunaanza kuiona kazi iliyoko mbele yetu. Si tu kwamba, ni sheria hii tu tuliyoileta hapa, Muswada au Sheria ya Ndoa, kumbe hapa kuna masuala mazima kabisa ya Sheria ya Mzazi. Hivi huyu mzazi tumemtengenezea Sheria ya Mtoto, sasa mzazi yeye ana sheria gani? Amesema Mheshimiwa Msambatavangu hapa; tumelichukulia kwa umakini, lakini masuala haya yote ni maadili. Kwa ujumla tunasema maadili, tuna Sheria gani ya maadili? Je, vifungu vyake vimesambaa kwenye Sheria ngapi hapa nchini kwetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hizi ni ajenda ambazo tunazichukua twende tukazifanyie kazi, ili tunapoendelea kurejea maboresho mbalimbali, kama alivyosema Mheshimiwa Shigongo, haya ni maisha na maisha ni endelevu na sasa hivi yanabadilika kwa kasi sana. Hata sisi mabadiliko ya Sheria zetu pamoja na Kanuni zetu inabidi yawe kasi ya kutosha, ili tuweze kuiweka jamii yetu kwenye mustakabali mzuri wa ustawi pamoja na maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hivyo, kwa utangulizi huu na kwa muda nilionao ambao umenipatia naweza nisimjibu kila mtu kwa mstari mmoja mmoja, lakini nitajitahidi kupita tu kwa maeneo machache yaliyosemwa na mengine tutayawasilisha kwa maandishi na tutaendelea kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, nikirejea kwa Mheshimiwa Maige alichangia kwamba, sheria zote zinazohusu watoto zirekebishwe pamoja na bajeti ya mabaraza. Ni kweli tuna kazi kubwa ya kuendelea kuvigusa vipengele mbalimbali vya sheria ambazo zinachangia kwenye kumlinda huyu mtoto. Hii kazi tungesema tuimalize yote kabisa, pengine haya ambayo tunasema ni *quick wins* tungechelewa kuyaleta na bado kuna kundi la watoto wangeendelea kukosa haki zao kwa kusubiri yale mengine makubwa yanayohitaji mjadala mpana wa kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba tumepokea tunakwenda kuendelea na hii kazi na hatutaogopa kila mwaka

kuwa tunakuja hapa na marekebisho, kwa sababu maisha ya watoto ni mapana sana na watoto wapo kwenye marika mbalimbali pia Sayansi ya Dunia inazidi kubadilisha mwelekeo wa maisha haya. Tutaendelea kufanyia kazi na kuziunganisha hizi sheria, zikiendelea kufanyiwa marekebisho kadri inavyostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu bajeti ya mabaraza, ni kweli mabaraza haya tumeyaanzisha na tumepokea hapa michango mizuri kabisa kwamba, mtoto miaka 0 – 18 ni parefu, wanabadilika hawa kutokana na *category* zao. Mabaraza haya yasiwe tu bora baraza la kwenda kucheza, hapana. Yawe ni mabaraza yenye tija. Tunajielekeza kwenye kuhakikisha bajeti hizi zinazokuja kila ngazi kuanzia halmashauri, mkoa, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na kisekta, tuwe na bajeti zinazosema kwamba watoto wetu mpango wao ni huu, tunataka wakienda kwenye *level* hii, watoke na kitu hiki hapa.

Mheshimiwa Spika, hili tutalisimamia kwa sababu ni la kisheria kila *accounting officer* kule alipo tutahakikisha amepelekewa maelekezo kwamba, apange na Waziri wetu wa Fedha aone kwamba kumepangwa kule, liwe ni hitaji mojawapo la kupitisha hiyo bajeti yake kwa sababu tumeamua kama Taifa kuwalinda watoto wetu. Tunatarajia mwitikio uwe ni mkubwa. Kwenye kanuni tunazoenda kutengeneza tutahakikisha tunatengeneza za kubana pia hawa waajiri au *accounting officers* (Maafisa Masuuli) kuhakikisha kwamba, wanaweka ndani yake bajeti za mabaraza haya kule walipo kila ngazi.

Mheshimiwa Spika, nirejee hoja chache za Mheshimiwa Mariam Kisangi ambapo amezungumza kwamba kanuni hizi tuziweke katika mustakabali kwamba mtoto atakapoasiliwa ikaonekana kule imeshindikana, taarifa zitakapokuja, tunapokwenda kumtoa lazima tuwe na jicho pana la kuangalia; je, hili suala ni la usahihi au ni watu wametengeneza mazingira ili kumkosesha ustawi na maendeleo huyu mtoto au kumuumiza mtu ambaye amemuasili? Hili ni jambo zito, tutazingatia na kanuni zetu zitaweka utaratibu tunafikaje mpaka kwenye kusema tumekataa hili shauri au hili shauri tumelikubali ili huko kuasiliwa kutenguliwe. Siyo suala la kuliendea kwa uharaka hivyo tutakwenda kulifanyia

kazi kwenye kanuni zetu, tutaweka vizuri sana utaratibu utakaotumika.

Mheshimiwa Spika, vilevile ameongelea kuhusu masuala ya mabaraza ambayo nimeshayajibu naomba nisirudie. Niende kwa Mheshimiwa Khadija Taya, ambaye ametoa pongezi zake kama wengine lakini pia amezungumzia sheria ziende chini zikatekelezwe bayana. Hakika hii sheria itakuwa ni kipimo kimojawapo kitakachomfanya hata *CAG* aangalie hivi tuliyoyasema haya yanatekelezwa au hayatekelezwi? Nani hatekelezi na *administratively* itakuwa *addressed* vipi kwa yule ambaye hatekelezi? Mojawapo ya hilo tutakaa na *CAG* tuongee naye, ili aweze kuweka katika utaratibu wake wa kufuatilia utekelezaji wa masuala haya, kuhakikisha tumeweza kufika kule chini kwenye ngazi ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ulenge na yeye amechangia. Nitasema machache kuhusu masuala ya *cyber bullying*. Tumeweza kugusia kwenye Muswada huu tukirejea pale kwenye Ibara ya 41 ambapo tumezungumzia masuala mbalimbali ambayo mtoto hatakiwi kufanyiwa. Iwe ni kwa maneno, kumtazama tu, kumgusa, au kumchora kwa vyovyote vile kumdhalilisha anapokuwa mtandaoni. Sasa kwa sababu tumeweka pale kwenye Ibara ya 41 tunaamini kwamba, kwenye utekelezaji huu kama kutakuwa na mapungufu ambayo hata kwenye kanuni hayatajitosheleza tutaendelea kufanya *revisit* ya hili eneo ili kuboresha kulingana na jamii yenyewe inavyobadilika siku kwa siku.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *COP*. Tunashukuru tulizindua hii Kampeni ya *COP* hapa Tanzania ya kumlinda mtoto mtandaoni, tunakwenda kuiimarisha zaidi na kwa msaada wa sheria hii, ndiyo itakuwa imeweza kufika mahali pake. Kama kuna mapungufu tutaendelea kuyaboresha. Nimshukuru sana Mheshimiwa Salome Makamba ambaye na yeye amechangia kwa upana sana, lakini amegusa maeneo makubwa na ya msingi sana kwamba, zipo sheria nyingi bado zimeachwa, ni kweli. Kama nilivyosema awali tungesubiri yote tuyamalize, ulimwengu wa sheria ni mpana sana unaomgusa mtoto, tusingeweza kuja hapa leo na kuna watoto

wangeendelea kuumia hapa. Hivyo, tumezingatia hili tunakwenda kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masuala ya Sheria ya Ndoa; namshukuru Mheshimiwa Waziri Pindi Chana atakuwa amegusia lakini Serikali ilileta mara ya kwanza yakatolewa mapendekezo. Bado inaendelea kufanyia kazi eneo hili. Kwa mjadala wa leo tunaona kwamba, kumbe tunatakiwa kufikiria zaidi kama alivyosema Mheshimiwa Shigongo; tufikiri na kufikiri nje na tufikiri kwa haraka hapa je, huyu mzazi yeye sheria yake ni ipi na Sheria ya Maadili ni ipi itakayotufanya hata mtu anapoingia kuwa mzazi aweze kujua wajibu wake ni huu na kitu gani asichofanya, hukumu yake ni ipi? Hili ni jambo la msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni rahisi tu kuongelea Sheria ya Ndoa wakioana sawa, lakini Sheria ya Mtoto sawa. Huyu mzazi yeye mwenyewe anapoamua kuitwa mzazi amepewa hata semina ya kujua kwamba kule ninapokwenda kwenye maisha haya natakiwa kufanya nini? Haya ni mambo tunayoenda kuyajadili tukiunganisha na maelezo yote haya, tuje na vitu vipya vingine kulingana na ulimwengu wa sasa ili tuwasilishe mtupatie malekezo twende mbele.

Mheshimiwa Spika, limeongelewa suala hapa la kumlinda huyu ambaye amefanya *adoption,* kwa jinsi uwekezaji wake alioufanya hili nalo linakuwaje? Tunaenda kuliangalia kwenye kanuni. Tutaweka ulinzi gani ili asinyang'anywe huyo mtoto. Vilevile fidia inatolewa vipi kwa mtu aliyefanyiwa ukatili? Siyo tu kumfunga huyu mtuhumiwa akikutwa na hatia lakini kama atakutwa na hatia, fidia kwa huyu manusura inakuwaje? Tumeizungumzia kwenye Ibara ya 42 kuhusu masuala haya ya fidia. Kwa hiyo, tumegusa hilo eneo tutakwenda kuweka kanuni nzuri, ili watu waone. Siyo tu kufungwa miaka 30 au 20. Utaendelea kuwajibika kwa huyu uliyemfanyia ukatili kwa kadri Mahakama itakavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, tunajua kwamba kweli miundombinu yetu siyo mizuri kwenye magereza. Naomba niongelee namna gani hawa Maafisa Ustawi wa Jamii ambao ni wachache tutaweza kuwa na tija nao. Katika kipindi hiki tulichonacho kwa

uchahe wao ule ule, tuliweza kuwagawanya kwenye kila Mahakama inayoshughulikia masuala ya mashauri ya watoto, kuwe na Afisa Ustawi mmoja ambaye kazi yake ni ku-*deal* na mashauri tu. Hatusemi kwamba inatosha, ndiyo maana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alitoa kibali cha ajira kwa Maafisa Ustawi 350 katika bajeti ya mwaka uliopita. Ajira zinaendelea na bado hawatoshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *commitment* yake kuhusu eneo la ustawi wa jamii ni kama tunavyoona kwamba sasa sheria hii ambayo imekuja mbele yenu itakwenda kuleta msukumo kwenye hizo ajira. Pia, maboresho ya mnyororo wa hakijinai umegusa mahitaji ya Maafisa Ustawi wa Jamii. Kwa hiyo, tutaona kwamba kuanzishwa kwa Wizara hii anakwenda hatua kwa hatua na tutaona sasa wimbi kubwa la Maafisa Ustawi wa Jamii wakiendelea kuajiriwa ili kukidhi matamanio haya ambayo yameshaanza.

Mheshimiwa Spika, masuala ya simu janja tuna-*control* vipi, tutaenda kuketi tuzungumze vizuri na Wizara yenye dhamana na masuala haya ya teknolojia ya mawasiliano na sisi tuangalie. Amechangia Mheshimiwa Salome Makamba, tunafanyaje sasa kwenye dunia ya kwetu huku Tanzania? Ina maana sisi hatuna watu wa kuweza kutusaidia kubuni vitu vitakavyosababisha watoto hawa basi kuwe hata na simu sokoni za bei nafuu kabisa au kwa namna yoyote ile wawe na *channels* zao maalum za kuangalia vitu wanavyovihitaji. Hivi ni vitu ambavyo vitaingia kwenye mjadala wa kuboresha safari yetu ya ulinzi wa watoto.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme yamesemwa mengine na Mheshimiwa Shigongo kuhusu masuala ya vileo, nayo tunaona bei inakuwa rahisi watoto wanajiingiza huko, watoto wengine wapo mtaani tunawaondoaje? Hizi ni ajenda ambazo tunazo pale Wizarani. Huwa napenda kusema Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kipengele cha ustawi wa jamii peke yake ni kama bahari tatu hapo zimekutana (India, Pasifiki na Atlantiki). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni eneo nyeti na ambalo lina mambo mengi mapana ya kisekta. Hivyo, hizi ajenda ambazo tumepewa hapa, zitakuwa sasa kianzio na mwendelezo wa *commitment* ya Serikali kuzijadili kisekta na kuwa tunatoa taarifa na mazao ya sheria mbalimbali au kanuni katika kuboresha safari ya ulinzi wa watoto.

Mheshimiwa Spika, mambo ya kuzungumza ni mengi siwezi kuyamaliza. Itoshe kusema tumepokea, tunakubali na tunakwenda kufanyia kazi na kazi ni endelevu kwa sababu maisha ni endelevu hasa ya ulimwengu wa kidijiti, yanayoendelea kukua kwa haraka, hakuna namna mabadiliko ya sheria na kanuni inabidi nayo yawe endelevu na kwa kasi ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, mapungufu yote yaliyojitokeza kweye Muswada huu tutaendelea kuyafanyia kazi kwa uendelevu wake. Niombe tu kwa siku ya leo Muswada huu ikiwapendeza Bunge lako Tukufu waupitishe, tukaanze kazi huku tukiendelea kukaa sawa kuendelea kufanyia kazi haya ambayo wametuelekeza. Nimshukuru Waziri, Mheshimiwa Pindi Chana kwa mchango wake, naungana na mchango wake huo pamoja na Mawaziri wote na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, katika kuendelea kufanyia kazi haya ambayo tumeelekezwa na tumeyapokea kutoka kwenye Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

Sasa, kabla sijamwita Katibu ili tuweze kuendelea na ratiba, tuna wageni ambao wameingia baada ya tangazo nililotangaza. Hawa ni wageni waliokaa jukwaa la Spika.

Tunaye Mheshimiwa Giuseppe Sean Coppola ambaye ni Balozi wa Italia Nchini Tanzania. Ameongozana na Ndugu George

Mwakyembe ambaye ni Afisa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Pia, yupo Ndugu Jemim France ambaye ni Afisa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Karibuni sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Ulinzi wa Mtoto wa Mwaka 2024 *[The Child Protection Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024]***

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2
Kifungu cha 3

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

Kifungu cha 4

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 4 Waheshimiwa Wabunge kina Marekebisho ya Serikali, wakati huo huo Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, hapa ukurasa wa nne wa Muswada Kifungu cha 4C kina maneno hapa yameandikwa *sexual activities, other activities* halafu ukishuka huku tena kinakuja kusema *shows a child to be involved in such activity.* Hii ni lugha ya kisheria au mimi ndiyo nimepitiwa siku hizi. Hizi si huwa zinaitwa *act* ama *acts, activities?*

Hebu watusaidie, mimi najua zinaitwa *sexual acts* kama unataka kuziweka wingi au umoja ni *sexual act*, lakini kwamba ni *activities* hapo sasa ndio kidogo mtihani.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unamaanisha hiyo tuliyo-*delete?*

**MWENYEKITI:** Aah! Ninyi mmefuta ipi?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *other activities that are not sexual is deleted.*

**MWENYEKITI:** Sasa, kabla ya hayo maneno hii *schedule of amendment* inaitwaje kwa Kiswahili? Ama tunatunga sheria kwa Kiswahili kwa hiyo, hii *schedule of amendment* ina jedwali la marekebisho. Ahsante sana.

Haya, kwenye hii *definition* inasema *child sexual abuse material or child sexual exploitation material,* mstari wa tatu *contents which depicts sexual activities involving a child whatever and then,* ndiyo tupo hapo. Zinaitwa *activities* au *acts?*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, zinaweza kutumika kwa *synonyms* kwa pamoja *either way*.

**MWENYEKITI:** Sisi tumejaribu kuangalia huku kwenye *Penal Code* hamna neno *activity* hata moja. Ni Kiingereza kipya au cha kumwezesha Waziri aweze kutafsiri sheria vizuri? Kama tunaweza kuzitumia zote kwa pamoja basi itumike moja ambayo inatumika kama lugha ya kisheria kwenye sheria nyingine pia.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo lilikuwa ni ku-*reflect* zile *activities* ambazo zinafanyika na kuja kupelekea na kumfanya yule mtoto aweze kuwa *influenced* na *sexual acts.* Ndiyo maana tukatumia neno *activities.*

**MWENYEKITI:** Sawa, sasa, mimi nataka tu kujua kwa sababu katika utungaji wa sheria huwa siyo lazima utunge sentensi mpya unaweza ukawa umechukua kwenye sheria ya watu wengine huku, ukaamua kuweka hapa na wapi ndio utungaji wenyewe

wa sheria, lakini hii lugha ya *activities* ndiyo mimi nawaza yaani neno *activity* siku hizi inatumika kwenye *legislation?* Neno *activity* badala ya neno *act* ama *acts,* sasa hivi tunaziita *activities?* Ndiyo swali langu.

Maana mimi sipo kule. Kwa hiyo, nipo huku kwenye siasa kidogo, ndiyo maana nakuuliza zaidi wewe Mwanasheria upo kule ambako mnapika zaidi haya mambo, huenda mambo yamebadilika. Unaweza kulitazama. Humu ndani wanasheria leo tupo wawili tu?

Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, jamani mbona unatuacha peke yetu hapa? Wewe si Mwanasheria mwenzetu ama? Mwanasheria mwingine yupo wapi? Hakuna? Hata wewe siyo mwanasheria lakini? Au wanasheria waliosoma hivi karibuni.

Naona wanasheria wawili mmesimama.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya maneno mawili yana tafsiri tofauti. Ukisema *activities* unazungumzia shughuli, lakini ukisema *act* ni kitendo, *acts* ni vitendo.

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Tadayo.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hapa sheria ilikusudia yale matendo mengine ambayo yanaweza yakapelekea kile kitendo chenyewe. Kwa hiyo, nadhani…

**MWENYEKITI:** Ile sehemu ya matendo mengine yameondolewa kwa hivyo hapa yamebaki yale mahsusi.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana ilikuwa *repetition* sasa kwa sababu kama wangesema *sexual activities and other activities* tayari hapo ilikuwa *repetition* ndiyo maana wameondoa moja. Kwa hiyo, labda kama tunasema *sexual activities* kama kuna haja ya kuongeza *sexual acts* pia ni sawasawa, lakini nadhani hapo walikuwa hawamaanishi ile *sexual act* yenyewe, walikuwa wanamaanisha vitendo vingine ambavyo vinaweza vikapelekea hiyo *sexual act*.

Nakubaliana na wewe kwamba, katika maana ya *sexual acts* sheria haina *activities,* lakini hapa inazungumzia vitendo vingine ambavyo vinaweza vikapelekea kwenye *sexual act*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ndivyo nilivyoelewa.

**MWENYEKITI:** Sasa hapo umenichanganya kidogo. Vitendo vingine vimeshatoka, mimi nataka tu kujua neno *activity* kwenye sheria inayohusu, kwa sababu haya ni matendo, *these are criminal acts*. Hiki Kifungu tunachokitunga hapa kina uhusiano na *criminality*, sasa nataka tu kujua, hilo ni neno la kisheria au siyo ili tuliweke hapa, wala sina shida kama neno *activity* ni neno la kisheria kwa muktadha huu tuliweke, kama siyo tuliondoe.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tuna-*refer* kwenye *Criminal Act* siyo neno la kisheria.

**MWENYEKITI:** Naam?

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tuna-*refer* kwenye *Criminal Act* siyo neno la kisheria.

**MWENYEKITI:** Ni *criminal* kwa sababu hapa tunazungumzia *child sexual abuse material or child sexual exploitation material*.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *context* hiyo siyo.

**MWENYEKIETI:** *Means any kind of material or virtual display including image, videos, audio or written content which depict sexual activities, involving a child or portray the child in a sexualize manner and ...*

Nataka tu kujua ni neno la kisheria au? Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunacholenga hapa kutoka kule kwenye sera ni ku-*address* zile shughuli tunasema za kingono *(sexual activities)* ambazo

ukizifanya zitaenda kupelekea hizo *acts,* hizo *criminal acts,* kwa hiyo hapa maneno tuliyoyatumia ya *activities*.

**MWENYEKITI:** Hebu fungua *dictionary* kwa sababu jamani *Criminal Law* si tulisoma wote mwaka wa kwanza? Mliwahi kukutana na neno *activity* ama tufungue hapa *Sexual Offenses and Special Provision Act* tutafute neno *activity*. Kwa sababu *whatever the definition that you want to put*, mimi *I want here to put the legal language*. Kama *activity* ni *legal language* tuiweke, kama siyo *legal language* tuweke *acts*.

Mwanasheria mwingine!

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umetuongoza vizuri. Kwa mujibu wa *sexual offences* ambayo ndiyo msingi wa kosa hilo la *Sexual Offense*, hakuna neno *activity*, zinatambulika kama *Sexual Acts*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, hata kama wao wakiiandika *acts* wakawa wanarejea *activities* bado litaleta tu maana japokuwa kwenye sera yao wameandika *acts*.

**MWENYEKITI:** Haya!

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hicho ulichokisema wewe ni lazima iwe *sexual acts* au *sexual act* na siyo *activities*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa, sasa kwa sababu uzuri Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wakati Waziri akihitimisha hoja amesema hili zoezi ni endelevu. Kwa hiyo, tutaendelea na sisi kufanya nini, kuboresha kwa kadri muda unavyojitokeza. Ila kwa sasa kwa sababu hatujajiridhisha vizuri kama hili neno limebadilishwa linaweza kuitwa *activities* nadhani tutumie *acts,* lakini kwa sababu kuna nafasi ya kubadili tena tutalibadili tu kama tunaona hili *acts* halileti ile maana tuliyokusudia. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekubali tutumie *acts*.

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante sana. Halafu hapa mwishoni kabisa, *"... which cannot be easily differentiated from a real child"*. Je, zile ambazo *you can differentiate* tunaziondoa? *Why did we have to put these words*? Kwa nini tusiwe tu na *which can not be differentiated from a real child*? Kwa sababu *easily be differentiated, what if it is difficult*? *I don't know*!

*So, we want to address the one that are difficult, what about others? Anyway* sijui*!* Hebu isome hiyo sentensi Mheshimiwa ili tujue nimeelewa sawasawa au Hapana, kwa sababu tumesema *which can not easily be differentiated from a real child*. Kwa hivyo, hapa hatutaki zile ambazo *you can easily differentiate,* ndiyo nia yetu? Ama tuchukue tu zote zile ambazo *we can not differentiate from a real child*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri tuchukue tu zote.

**MWENYEKITI:** Tuchukue zote kwa sasa ili huko baadaye kama kuna sababu ya kubadilisha tutabadilisha, lakini kwa sasa tuweke zote si ndiyo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, tuko pamoja? Haya, *which can not be differentiated*. Haya ahsante sana, tunaendelea.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 5

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 5 kina marekebisho ya Serikali. Kifungu cha 5 hapa *"A person shall not through computer system produce ..."* yote hayo yametajwa. Sasa, nilikuwa najiuliza *what about a phone*? Ama ile siku hizi ukishasema *computer system* unamaanisha na simu ziko humo ndani ama zile *devices* nyingine kama sijui tunaita nini? *Storage* ama *flash drives*, hizo zinakuwa zimekaa wapi? Maana hapa tumesema *"A person shall not*

*through a computer system produce child sexual abuses".* Aki-*produce* kwa kutumia simu? *Offer or make available child whatever*, zote zinahusu *computer system*. Akitumia simu ama simu siku hizi inakuwa sehemu ya *computer system*?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, simu ni sehemu ya *computer system* kwa mujibu wa watu wa *TCRA* na wataalam wa mawasiliano ambao tulikuwa tunatengeneza nao huu Muswada. Kwa hiyo, *smartphone* na ...

**MWENYEKITI:** Kama ndivyo, hizo ninadhani zinaitwa *electronic systems* badala *ya computer system*, ama neno *computer* linaitwaje?

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani neno zuri hapo ni *electronic devices*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Eeh, *either device* ama *system*, *one of those two,* lakini tukitumia *computer* kwamba tutamkamata mtu aliyetumia simu na hapa juzi si mmeona tumepata changamoto kidogo? Watu walitumia nini, simu. Sasa, ile tunaweza kubishana kweli mbele ya Jaji tukasema simu ni sehemu ya kompyuta? Ama tuite *electronic*.

Mheshimiwa Waziri, *computer*? Jamani twendeni *faster*, wataalam wa *IT* humu ndani ni akina nani? Ukisema kompyuta unamaanisha na simu ama tutumie neno *electronics*? Mimi siyo mtaalam.

Haya kule nyuma, enhe Mheshimiwa Twaha Mpembenwe.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kulitumia neno hilo, *it has to be electronic devices,* kwa sababu huwezi uka-*include computer and then* unakwenda kumkamata mtu aliyekuwa ametumia simu, *is not going to work*. Kwa hiyo, *it has to be electronic devices of which* ina-*include* mpaka *computers* na *device* nyingine, hizo *telephones and all those sorts of things*. *Thanks*! *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Dkt. Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisema *device almost you are talking about the hardware,* lakini ukisema *system* una-*include* kila kitu, na wakati ukiwa unataka kutengeneza kitu, *pornography or whatever*, utatumia *system* kwa hiyo lazima tutumie *electronic system*.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, tutumie *electronic system* au tutumie *computer system*?

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *electronic system.*

**MWENYEKITI:** *Electronic system*? Aah, Mheshimiwa Balozi Mulamula! *(Kicheko)*

**MHE. BALOZI LIBERATA R. MULAMULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, tukiongelea *electronic devices* ni nyingi sana, kwa hiyo, naona tutumie *electronic digital devices*. Maana yake ukisema *electronic device* ni hata pasi. Kwa hiyo iwe *electronic digital devices.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya, neno *device* limeondolewa limebaki *electronic system*. Sasa naambiwa hapa hadi pasi, kweli leo huku ni kupatwa. Haya, nimewaona Waheshimiwa. Mheshimiwa Dkt. Kiruswa.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa Kiingereza siyo lugha yangu ya kwanza wala ya pili, lakini kuna neno pia linatumika sana kwenye hizi nyanja za kielektroniki, inaitwa *electronic appliances*. Kwa maana inajumuisha vitu vyote mpaka *microwave* na *TV* na kila kitu ambacho kinaweza kikam-*expose* mtu kwenye vitu vinavyoweza kutumika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Enhe leo kumekucha. Haya, Mheshimiwa Esther Matiko!

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Nadhani ili tuweze kuweka sawa, ukisema

*electronic system to me* ina-*sound like the applications*. Kwa hiyo, mimi ningeweza kusema *electronic system and devices*, itakuwa iko *well* ime-*combine*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Enhe, jamani hebu maadam mko na simu zenu hapo, hebu angalieni *electronic system* huko wamesema ni nini, halafu mtafute na *computer system*.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Naam, Mheshimiwa Salome!

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli *electronic system* zinaenda mpaka kwenye pasi na *microwave* lakini tukiangalia kwenye muktadha wa sheria hii tunaongelea *electronic systems* ambazo zinaweza zikaleta *sexual offense*. Kwa hiyo, hapo *automatically* pasi na *microwave* zinatoka. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante. "*Electronic system that is powered by electricity and it processes information, data or any raw material from input into a desired output for further usage in life*", hii ndiyo *electronic system*. *(Makofi)*

Haya, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba niwasomee sheria iliyopitishwa na Bunge hili, Sheria ya *Cyber Crime*.

**MWENYEKITI:** Naam!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya *Cyber Crime* ime-*define* kwamba, "*Computer System means a device or combination of devices including network, input and output devices, capable of being used in conjunction with external file which contain computer programs, electronic instructions, input data and output data that perform logic arithmetic data storage and retrieval communication control and other functions*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, siyo *electronic system* ni *computer system*. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Umekisoma vizuri hiki Kifungu chako kinataka ku-*cure* nini? Hiki kifungu chako tumeanza hapa kinataka ku-*cure* hoja za *child sexual abuse material or child sexual exploitation material*? Sasa, *anyway*! Waheshimiwa hapa nimeletewa zote mbili, *definition* ya *computer system* pale tumesomewa tuliyotunga sisi kwenye sheria, hapa kwenye simu inasema, "*It is a system that encompasses hardware data and software*". Hapa kwa haya maneno yanayosemwa ninaiona hiyo changamoto Mheshimiwa *AG*, kwa sababu tunachotaka ku-*cure* ni cha hawa watoto, sasa sijui!

Hapo kwa nini hawakutaja *phone* kwa mfano, kwenye hiyo *definition* kwa nini hatukutaja neno *phone*?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *impliedly* imetaja, ukisoma maudhui ya ile *definition* mliyoitoa wakati mnatunga Sheria ya *Cyber Crime*.

**MWENYEKITI:** Hebu taja moja! Sema wakati tunatunga, maana yake na wewe uko humu ndani na mimi sijui *Cyber Crime* kama nilikuwepo hapa mbele, nilikuwa kule nyuma ama nilikuwa nje ya Bunge, ama nilikuwepo kabisa Mbunge. Sema tuliyotunga, maadam uko humu ndani. Enhe! *(Kicheko)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefuta maneno, nimefuta maneno. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Hebu tafuta neno moja hapo litakaloashiria simu halafu tupite.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudia tena, "*Computer System means a device or combination of devices including network, input and output devices, capable of being used in conjunction with external file which contain computer programs, electronic instruction, input data and output data.*

**MWENYEKITI:** *Computer program* unarudia tena. Hivi neno *computer* peke yake maana yake nini? Hebu tafuta neno *computer* peke yake bila neno *system*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitafute *definition* ya neno *computer*?

**MWENYEKITI:** *Computer* tu bila neno *system*, hebu tafuta!

Eeh, lazima tuseme hivyo kwa sababu tutakapokutana huko Mahakamani ndiyo hivi tutakavyokuwa tunabishana halafu mtu atatolewa halafu tutaanza sisi wenyewe tena kutafutana. Jamani nadhani, maadamu tumesema tutaendelea na maboresho, si ndiyo jamani? Tumesema tutaendelea na maboresho, lakini pia ikipatikana changamoto tutakuwa tumejifunza, twende na *computer systems*. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** *Yes.*

**MWENYEKITI:** Wewe unaitika *yes*, mtakuja hapa ndani, maana mnakumbuka *Law of Evidence* imetupeleka *speed* huko, watu wanashinda keshi wananchi wanalalamika mpaka tumerudi hapa, ndiyo maana hapa tulitaka hicho tuondokane nacho.

Haya, kwa mfano huku mbele hii hii *Section*, *Section 5* ambayo ina-*amend Section 13*, ukienda kwenye *Sub-Section 2* inasema, "*A person shall not propose, groom or solicit, through computer system, to meet a child, whatever...*" nikiamua kutumia, yaani unajua tunajaribu kuweka hayo mazingira. Nikitumia simu wewe unasema hapo *impliedly* itakuwemo. Mimi nitatumia simu, nani anaenda kutafuta simu, anatumia kompyuta kum-*solicit* huyu mtoto. Si atatumia simu yake? Maadamu mmesema simu na yenyewe imetajwa, haya twende. Hiki hapa tunawaachia hivi mlivyokileta, kikileta changamoto mtarejea tutaendelea.

Waheshimiwa Wabunge, hiki tusonge nacho ama? Mheshimiwa Salome!

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata *definition* ya *computer* au tumeachana nayo?

**MWENYEKITI:** Aah *definition* ya nini?

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *computer*, ulisema tukutafutie. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Hebu, enhe!

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inasema, *"Is an electronic device for storing and processing data, typically in binary form according to instructions given to it in a variable program"*.

**MWENYEKITI:** Haya, jamani tumeambiwa hapa *flash drive*, sijui simu sijui kitu gani, vyote vimo humu kwenye *computer*.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti,...

**MWENYEKITI:** Nani amesimama tena? Haya Mhandisi!

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri ni bora kuzungumzia *ICT devices*. Inakuwa ina-*include laptop, computer, smartphones and so forth*, *is much better* kuliko kusema *computer devices, computer system*. *ICT devices is much better.*

**MWENYEKITI:** Sasa hapa tunataka *soft* na *hardware*, si ndiyo tumeambiwa? Waheshimiwa Wabunge, nadhani tunaweza kwenda nayo hii *computer system*.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti!

**MWENYEKITI:** Naam!

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nirejee kwa mujibu wa Sheria ya Ushahidi *(Electronic Transaction Act) Cap. 442, Revised Edition 2022*. Yenyewe inasema, ina-*define*, *"Computer System means a device or combination of devices including network, input and output devices, capable of being used in conjunction with external files*

*which contain computer programs, electronic instructions, input data and output data that perform logic, arithmetic, data storage and retrieval communication control and other functions*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ninadhani inafanana au inaelekeana na uliyosoma Mheshimiwa *AG*? Zinafanana?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo zinafanana!

**MWENYEKITI:** Basi, ninadhani sheria zote kama zinaenda hivyo tubaki nayo hii, ama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mbunge, umesimama tena!

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani kidogo! Ninafikiri *is better to use electronic system* kwa sababu *we have a definition here of electronic system*. Kama utaniruhusu naomba niisome kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasema, "*An Electronic System is a set of interconnected electronic components and devices designed to perform a specific task or functions. It typically includes various hardware components such as microprocessor, sensors and actuators and may involve software to control and manage these components. Example of electronic system include computer, smartphone, automative control system and household appliances. They rely on the principle of electronic and electrical engineering to process and manage electrical signal for a wider range of application*". *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *having said so, an electronic system should be the right word to be used over there. Thanks! (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa, sasa *that definition it would seem does not appear in any of our statutes, that is what we are facing right*

*now. So, we go with computer system, and should need arise we shall change it. (Makofi)*

*Now,* tupo hapa kwenye *subsection (2)(a)* kuna neno *activities*. *AG* unapaona hapo? Kuna neno *activities* kule tulishabadili kuwa *acts*.

Haya twende kwenye *sub section four* ya hii *five*; *A person who is convicted of an offence under this section may*, hii *may* mmeweka *shall* sasa hivi siyo? Mmeweka *shall*, *shall in addition to any other punishment be ordered to compensate the victim of the offence*. Sasa hii *order* ya *compensation assumption* ni kwamba ni Mahakama ndiyo inayotoa si ndiyo?

Kama hivyo ndivyo na inayotoa ni; kama inayotoa ni Mahakama hapa sisi tukitumia neno *may* kifungu hiki namna kilivyo kitakuwa kipo sawa maana yake kunaweza kukawepo ama kusiwepo. Tukiweka neno *shall* bila kutaja ni, yaani bila kutaja *parameters* za hiyo *compensation* maana yake Jaji aseme ajengewe nyumba huyo aliyepata hii changamoto au apewe pesa? Apewe shilingi 1,000, apewe shilingi milioni 100, apewe milioni ngapi, yaani apewe nini? Kwa sababu tukiweka *shall* maana yake ni lazima kuwe na *compensation*, ambayo siyo nia mbaya ni nia njema, lakini tukiweka bila kuweka ule wigo wa hii aina ya *compensation* tukitumia neno *shall* tunaweka mazingira magumu.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unachokisema ni sahihi kabisa na sisi tulikuwa tumeweka *may,* lakini Kamati walitushauri tutumie *shall*, kwa hiyo kama tutasema turudi kwenye *may* tunaona ni sawa tu.

**MWENYEKITI:** Kamati ilipowashauri ninyi kuweka *shall*, ninyi si ndiyo wataalam? Mlipaswa mwende sasa hiyo *shall* mkaiwekee mazingira kwamba *shall but* hapa mpaka hapa, mkiacha tu hivi Dunia kweli jamani hii *compensation* itakuwa inatolewa kwa sura gani? Ama mimi ndiyo sielewi? Kwa sababu hii mmeiacha wazi anakuwa *compensated* kwa kufanywa nini?

*A person who is convicted of an offence under this section may;* na hii *section* ndiyo tuliyokuwa tunazungumza hapa. Yale yote ya *computer devices* amem-*solicit* akaenda kuonana naye *compensation* ya aina gani? Amem-*solicit* akamuonesha hizo *materials* ambazo zina-*coerce* sijui zinafanya kitu gani; *compensation*. *Compensation* ya aina gani Bunge halijasema kwa hivyo hata akisema shilingi 1,000 ni sawa, shilingi 500 sawa.

Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati nia yetu ilikuwa njema hapa lakini kwa ngazi hii kwa sababu hatuna uwezo wa kuweka hiyo mipaka ya hii *compensation* inatuwia ngumu kidogo lakini ninyi muendelee kukaa nalo hilo ili marekebisho yatakapokuja hili neno *shall* liwekewe hizo *parameters* kwa sababu bila ya hivyo naona tutakuwa tumefungua sijui, tumefungua nyumba mlango, madirisha na kila kitu. *AG*, tumeelewana vizuri?

Naam.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri maudhui hapa yamejikita zaidi kwenye kuiachia Mahakama *flexibility* katika ku-*determine* hiyo *compensation* kulingana na mazingira ya shauri husika.

**MWENYEKITI:** Sawa, sasa hiyo Mahakama huku kwingine Mheshimiwa *AG*, si hapa juu tu kwenye hii tatu tumeweka, *A person who contravenes this section commits an offence and on conviction shall be liable to a fine of not less than fifty million shillings or three times the value of undue advantage received, whichever is greater. Why did we put it? Why would we want to leave this open? Which is talking about compensation?*

Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naona ushauri wako ni sahihi kwa sababu sisi kama Kamati na tulikuwa tuna wanasheria pale tulijaribu kuiweka hivyo ili kusudi ionekane kwamba ni kitu cha lazima, lakini kama ni budi tufanye hivyo basi sisi kama Kamati tunakubaliana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hata wakati nachangia nilisisitiza sana, pamoja na kwamba hawa watuhumiwa wamepewa adhabu kali, waathirika mara nyingi huwa wanaachwa bila chochote na athari inakuwa ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa busara ileile ambayo tumetumia kwenye vifungu vingine tunaweza kuliacha neno *shall* kwa sababu ndiyo *spirit* ya Bunge na tukaiachia Mahakama itumie *wisdom* ya namna ambavyo *gravity* ya hiyo *offence* ilivyo na *compensation* iweje mpaka pale ambapo Serikali italeta marekebisho mengine madogo kwa ajili ya kuweka *ceiling* ya adhabu kwa kosa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukisema tuiondoe kabisa na *institutional memory* ya Bunge hili pengine ikaja hata Bunge lingine, hii *spirit* ambayo tunayo inaweza ikajikuta tu ime-*disappear*. Kwa hiyo tuiache hivyo na itumike busara ya Mahakama kwenye kiwango cha *compensation* mpaka pale ambapo Serikali italeta marekebisho ya ukomo wa *compensation* hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Hapana lazima tutoe *guidance*, kwa sababu sisi ndiyo tunatunga sheria. Lazima tutoe *guidance* ya *compensation* kama tunatumia neno *shall*. Tukitumia *may* kwa sababu unajua *may* uzuri ile sheria yetu ya tafsiri *may includes shall*, *shall ina-exclude may*; sijui kama tunakumbuka hilo? Ukitumia neno *may* lina-*include shall* kulingana na kesi itakavyokuwa imepelekwa, Jaji atajua tu kwamba hapa kwa kweli huyu anastahili nini, anashathili *compensation* lakini tukiweka *shall* maana yake chochote kitakachosemwa lazima. Sasa tukiweka lazima, lazima tutoe *guidance*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubaliana na ushauri wako mzuri na nadhani ni vyema tukatumia *may* badala ya *shall* kama Serikali ilivyowasilisha mwanzo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ndiyo na Mwenyekiti uzuri pia ameelewa. Yaani ili tuweke neno *shall* itabidi hili jambo pia Kamati waendelee kulitazama, adhabu wanataka wapendekeze katika *margins* zipi ili kutokuweka hayo mazingira ambayo Mahakama zitaanza kulalamikiwa. Tukisema *may* wao wenyewe wataamua huyu anastahili *compensation* shilingi milioni 100 wampe lakini tukisema *shall* halafu tukaweka mazingira fulani hivi itakuwa kidogo mtihani.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 6

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 7

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa King.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Marekebisho ya Serikali yamekuja kuongeza *subsection (2)* halafu wanakuja wana-*renumber*. Sasa hii *subsection (2)* ya mwanzo inazungumza "*A person who contravenes subsection one commits an offense*." Sasa inaiacha hii *two* ambayo imekuja kuingia pale. Kwa hiyo kwa maoni yangu nilikuwa naona kwamba iwe, *A person who contravenes subsection (1) and (2)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu imeingizwa na *two* hapa, inarekebisha 19A. 19A(1) imesoma hapo kama ilivyo. Sasa *subsection (2)* inakuwa *replaced* na hii halafu hii inakuja kuwa *renumbered*, hii ya *two* inakuwa *renumbered*.

**MWENYEKITI:** Ndiyo.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ya *(2)* inakuja kutaja hiyo adhabu lakini inataja kwa *subsection (1)* pekeyake.

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Mbunge, wameleta *further schedule of amendments* na wameweka hiyo, kwa hivyo inasomeka, hapo palipokuwa panasomeka *subsection (1)*, sasa hivi eeeh! Ngoja, ngoja.

Palipokuwa panasomeka *subsection (1)*, sasa patasomeka *subsections (1) and (2)*, si ndiyo hiyo Mheshimiwa Ali?

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 8
Kifungu cha 9
Kifungu cha 10
Kifungu cha 11

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 12

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 13
Kifungu cha 14
Kifungu cha 15
Kifungu cha 16
Kifungu cha 17
Kifungu cha 18
Kifungu cha 19
Kifungu cha 20

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 21

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilifutwa na Kamati ya Bunge Zima)*

Kifungu cha 22

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 23

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 23 kina marekebisho ya Serikali lakini pia hili nalo ni la kiuandishi. Mwanasheria Mkuu wa Serikali, hii sehemu ya mwisho kabisa hapa kwenye hicho Kifungu cha 23 kinachorekebisha kifungu cha 71A, hapa mwishoni inasema *is satisfied that the adoption is not for the best interest of the child*. Nadhani hii *for* huwa inaitwa *in*, ni sawasawa? Umefika hapo?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo hapo sema sijakuelewa vizuri.

**MWENYEKITI:** 71A upo hapo?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *yes* nipo hapo.

**MWENYEKITI:** *One* inasema, *the court may, upon application by a child guardian ad litem parent, guardian or any other interested person, revoke an adoption order if it satisfied that the adoption is not for the best interest of the child*. Nadhani huwa inasomeka *is satisfied that the adoption is not in the best interest of the child*, si ndiyo? *For* mta-*replace* na *in*.

Kifungu cha 23 pamoja na marekebisho ya Serikali na kuongeza neno *in* kinaafikiwa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 24

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 24, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kabla ya 24 hapa 23, *71A(2)*(f). Hiki Kiingereza kimeandikwa hapa kidogo ni kigumu sijui. *The adoptive parents developed health issues or disability causing them difficulty to raise the child*, hapa kidogo Kiingereza kimetutupa mkono. Nadhani kuna neno limekosewa, siyo kukosewa, nadhani kuna neno halipo ama sentensi yenyewe yaani hapa mwishoni hapa.

*Or disability or causing them difficulty*, hii ya *or disability causing them difficulty* ni kama Kiswahili fulani hivi cha Kiingereza. Kwa hiyo hapa mkapatazame na kwa sababu ni kitu kidogo unaruhusiwa na sheria zetu kufanya hizo *adjustments*. Ahsante sana.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**MWENYEKITI:** Hicho ni cha 24, kwa hiyo tuelekee 25. Aah 23 nimerudi pale tu ambapo sijafanya marekebisho yoyote, ataenda kufanya Mheshimiwa *AG*. Nimesharudi, 24 si ulikuwa umeshakitaja? Kwa hiyo nimeshahoji endelea na 25.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

Kifungu cha 25
Kifungu cha 26

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 27

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 28

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** 28 kina marekebisho?

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakina.

**MWENYEKITI:** 28, Mwanasheria Mkuu, *"Child in conflict with Law"* kwa nini mmeongeza maneno *in contact? How does the child contact the Law? Why did you add that word?*

Mheshimiwa Waziri, mmeongeza la nini hilo neno *contact*?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mimi niliuliza kutoka kwa wasomi, nikaambiwa kwamba anaweza akaingia kwenye *conflict* kabisa kwamba kukawa na mjadala kwamba ameikosea sheria lakini kwenye *contact* ni kwamba ameenda tu ku-*seek service* za sheria, siyo lazima kwamba awe labda ameikosea. Sasa anaweza akanisaidia *AG* kuelezea maana yake vizuri.

**MWENYEKITI:** Mtoto ameenda ku-*seek*? Nimevipitia vile vifungu vinavyotokea kwenye hii *part nine* sijaelewa kabisa hiyo *in contact with Law* mmeitoa wapi? Yaani imeingia hapo kwa sababu zipi? Yaani kwamba anakutana na sheria akiwa ameenda kutafuta huduma? Ndiyo uliambiwa hivyo?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani kwamba siyo lazima awe labda amekosa ana mgogoro wa kisheria yule mtoto lakini anaweza akawa anakwenda kupata huduma za msaada wa kisheria, labda...

**MWENYEKITI:** Kwenye hii sehemu ambayo mmebadilisha, hii sehemu ya tisa nimejaribu kutazama hivi vifungu sijaona hicho unachokisema, ama kinachoelekeana na huko.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maudhui ya kifungu hichi; *child in conflict* maana yake ni yule muhalifu *or in contact with law* ni yule *witness*. Kwa sababu wakati mwingine watoto wanakwenda kutoa ushahidi kule Mahakamani.

**MWNYEKITI:** Sasa hapa kweli hii *part* kuna mahali ukiacha kwamba huyu *witness* anaenda kwa ajili ya yule *child* ambaye yupo *in conflict with the law*; huyu *witness* unataka kufanya naye nini mpaka unataka *part* kum-*consider* na yeye? Kwa sababu huyu *witness* si anaenda kwa sababu kuna mtu ambaye yupo *in conflict with a law?*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *provisions* huku utaona kwamba yule *witness* (shahidi mtoto) atakapokwenda kule tumeweka *conditions* sasa hivi kwamba aende na Afisa Ustawi wa Jamii.

**MWENYEKITI:** Si hii hapa 115 kwenye ile sheria yenyewe? *A child as a witness?*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kipo huku mbele nafikiri tutakikuta lakini kipo kifungu ambacho tumeweka hiyo *condition* kwamba mtoto atakavyokwenda Mahakamani kutoa ushahidi asiende peke yake.

**MWENYEKITI:** Ni sawa, nimekuelewa hapo, anaenda kutoa ushahidi kwa ajili ya nini yaani? Si kwamba kuna jambo kule? Sasa yaani, sijui labda nashindwa kutoa maaelezo vizuri. *(Kicheko)*

Yaani hii sehemu, ni sehemu inayohusu watoto ambao wameenda wapi, Mahakamani kwenye kufanyaje? Wameenda Mahakamani; ngoja, hii sehemu inahusu, jamani jamani. Utungaji wa sheria umeshakuwa...

*Child in conflict with a Law, Juvenile court* inazungumzwa hapo, ikishamaliza *Juvenile court* inaenda huku nyuma. Maana yake *Juvenile court* inamzungumzia mtoto ambaye amekosea si ndiyo? Haya tunaenda huku mbele, *a child as a witness* ambacho huku kinahusu kifungu kipo 115 kinasema *child witness;*

*where in any cause or matter, a child is called as a witness*, sasa huyu yeye anawekewaje kule kwenye *part* jamani?

*Anyway*, tunaweza kusonga nacho lakini kwa kweli ni mambo ambayo juzi tulisema yanakuwa *superfluous* (unakuwa umejaza mambo ambayo kwa kweli hayana, yaani hayaongezi chochote). Kwa sababu huyu anaenda kule kwa sababu moja tu, kwa sababu kuna mtu kakosea yeye kaitwa. Haya tusonge siyo jambo la kufa na kupona hili, kwa hiyo linaweza kuachwa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 29
Kifungu cha 30
Kifungu cha 31

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu Kipya cha 32

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 32
Kifungu cha 33

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 34

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 35
Kifungu cha 36
Kifungu cha 37
Kifungu cha 38

Kifungu cha 39
Kifungu cha 40

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 41

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 42

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 42, kina marekebisho ya Serikali; atu wa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali hizi adhabu zilizopendekezwa hapa zote zipo kifungu kimoja, lakini inaonekana zinapishana sana. Hebu twende kwenye Kifungu cha 158 ambacho ndicho kinachorekebishwa. Upo hapo Mheshimiwa? 158 kwenye ile sheria mama *158*A. Upo hapo Mwanasheria Mkuu? Nilikuwa nasubiri ufikie. *(Kicheko)*

Haya. Kifungu cha 158 kinazungumzia "*A person who contravenes this section commit an offense and is reliable on conviction to a fine of not less than 2,000,000 shillings or to imprisonment for a term of not less than five years but not exceeding 15 years or both*".

Halafu hiki siyo cha kubadilisha sasa hivi, halafu 159 "*Any person who contravenes any provision of this Act where no specific penalty has been provided commit an offense and shall on conviction be liable for fine of not exceeding 50,000 thousand shilling or to imprisonment for a term of not more than three months or to both.*" Hii siyo ya mabadiliko, lakini hii sheria moja inakuwa na adhabu ambayo moja ukipima kwa fedha zilizowekwa na miezi au miaka iliyowekwa kwingine inakuwa mara 40 ya hiyo adhabu iliyotolewa.

Sasa hizi kwa sababu huwa zinajitokeza ni la jumla na nimelisema kwenye Kamati ya Bunge Zima siyo pale Bungeni ili sheria zinapotengenezwa zile adhabu ziwe siyo zinafanana lakini

zina mwelekeo ambao kwa kweli unaweza kusema una-*justify*. Kwa sababu kama mwingine umemwambia miezi mitatu kwa 50,000 mwingine 2,000,000 kwa miaka mitano yaani hiyo adhabu hesabu ni kama haijapigwa vizuri. Ahsante sana.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 43
Kifungu cha 44

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na marekebisho yaliyofanyika kuna *renumbering* kuanzia 22 mpaka 44 kuwa 21 mpaka 43 mtawalia.

*(Mpangilio wa Vifungu vilivyotajwa hapo juu ulipitishwa na Kamati ya Bunge Zima)*

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge Zima imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi. Mtoa hoja, taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2023, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Ulinzi wa Mtoto wa mwaka 2024 *(The Child Protection Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024),* Ibara kwa Ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Ulinzi wa Mtoto wa mwaka 2024, kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima, sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsanteni sana. Sasa nitawahoji kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Ulinzi wa Mtoto wa Mwaka 2024 *(The Child Protection Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024)*.

Hakuna asiyeafiki, wote mmeafiki, ahsanteni sana. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Tatu zinazohusu Ulinzi wa Mtoto kwa ajili ya kuondoa upungufu uliojitokeza wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika Sheria husika *(A Bill for an Act to amend certain Written Laws in order to keep the Laws updates with some challenges observed in the provision of the respective Laws***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

*(Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Ulinzi wa Mtoto wa Mwaka 2024 (The Child Protection Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024 Ulipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada umeshasomwa kwa mara ya tatu na kwa hivyo tumemaliza utaratibu wetu wa

Kibunge wa kutunga sheria. Hivyo, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Ulinzi wa Mtoto wa Mwaka 2024 *(The Child Protection Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024),* umepitishwa rasmi na Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote chini ya Ofisi yake pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuleta Muswada huu Bungeni mpaka sasa umepitishwa rasmi na Bunge na kwa kusikiliza mawazo ya Waheshimiwa Wabunge mbalimbali ambao wameyatoa ngazi ya Kamati na wengine wakati wa maoni. Walipoyaleta kwenu mmeyazingatia hayo yote, kwa hiyo tunawashukuru sana. Kwa sababu baadhi ya mambo ambayo sheria hii imekuja kuyafanyia kazi Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakiyapigia kelele. Kwa hiyo, tunawashukuru lakini pia tunawapongeza kwa kazi nzuri.

Tunawatakia kila la heri kwenye utekelezaji wa sheria hii hasa ukizingatia kuwa kuna mambo mengine ambayo ni mapya kabisa ambayo mojawapo ni hilo la kuanzisha Mabaraza ya Watoto, tunasubiri tuone huo utekelezaji wake na mambo yatakayokuwa yanafanyika huko. Pengine hata hoja nzito alizozitoa Mheshimiwa Mbunge wa Iringa Mjini zinaweza zikapungua yakianzishwa haya mabaraza. Kwa hiyo, tunawatakiwa kila la heri kwenye utekelezaji wa hayo yote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Wajumbe wa Kamati hii ahsanteni sana kwa kazi nzuri na Wabunge wote, ahsanteni sana wote kwa pamoja. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo kuna jambo moja ambalo Mheshimiwa Waziri hili inabidi likafanyiwe kazi kwa sababu ni kweli kwenye sheria yetu hayo mazingira hatujayaweka, kama tumeyaweka labda Spika ndiye hajayaona. Kwa sababu kuna mazingira ambayo mtoto wa kike anaweza kuwa amepata athari lakini zile athari amezipata kutokana na mtoto mwingine wa kiume.

Sasa hawa wote ni watoto na wote wamekutana na hayo mambo. Sasa hapa Mheshimiwa nimesema hili likatazamwe tu kwa ujumla kwa sababu Wizara yako ndiyo inasimamia ustawi wa jamii, inabidi kutazamwa kwa ujumla wake, lakini kama lina hitaji sheria basi nafikiri itabidi lifanyiwe kazi kwa sura hiyo ya Kisheria, kama siyo Kisheria basi kwa njia ya utawala ili watoto wote hawa waweze kuwa wanalindwa.

Sasa wakati Mheshimiwa Mbunge wa Iringa Mjini akizungumza kuhusu hawa watu ambao wamezalisha kiumbe hiki nikawa natamani kumpa taarifa kwamba wakati mwingine hawa wanaozalisha kiumbe wote ni watoto. Kwa hiyo, ukiwaambia kwamba wote kila mtu akalee huyo mtoto wote ni watoto sasa wataleleana watoto kwa sababu wamesababisha hayo matokeo. Kwa hiyo, nafikiri hili jambo tunatakiwa kuendelea kulitazama sisi wote kwa mapana kabisa na pia Mheshimiwa Khadija Taya, amelizungumza. Kwa hiyo nafikiri kuna haja ya kuwa na mjadala mpana kabisa juu ya mambo kama haya ili kama Taifa tuwe na ustawi wa sura hiyo. *(Kicheko/Makofi)*

Mengi yamezungumzwa pia kuhusu Sheria ya Ndoa, kwa kweli hili jambo nalo ni endelevu tuendelee nalo, japokuwa nilishasema kabisa, kwa kweli hiyo sheria hata itakapofika hapa ikitokea kwamba imeletwa miaka 18 nitashangaa sana, kwa sababu sioni namna gani mtoto wa miaka 18 anaweza kuwa kwenye ndoa. Kwa hiyo, tunaisubiri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna matangazo mawili hapa; tangazo la kwanza, linatoka kwa Katibu wa Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba Benki ya *NMB* wapo viwanja vya Bunge nyuma ya Ukumbi wa Msekwa kuanzia leo tarehe 30 Agosti, mpaka tarehe 6 Septemba, kwa ajili ya zoezi la kurekebisha taarifa za akaunti binafsi za wateja wa *NMB*. Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Bunge, mnao,bwa kwenda na kitambulisho kimojawapo kati ya vifuatavyo: Kitambulisho cha *NIDA*, cha Mpiga Kura, leseni au pasi ya kusafiria. Kwa hiyo, ukienda navyo hivyo wao watarekebisha taarifa zako vizuri ili uendelee kutumia huduma hizo.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwangu. Tunafanya marekebisho kidogo ya ratiba yetu:-

(1) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024)* uliokuwa uingie Bungeni tarehe 4 Septemba, 2024 sasa utaingia tarehe 2 Septemba 2024.

(2) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Bill, 2024]*, uliokuwa uingie Tarehe 4 Septemba, 2024 sasa utaingia tarehe 3 Septemba, 2024.

(3) Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, itaingiza taarifa yake tarehe 4 badala ya tarehe 5 iliyokuwa imewekwa hapo awali. Marekebisho haya Waheshimiwa Wabunge yatawekwa kwenye vishikwambi vyenu, itaondolewa ile ratiba iliyokuwa imeletwa awali.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana kwa uvumilivu wenu na niwakumbushe tu kwamba kesho tutakuwa tunakutana viwanjani kwenye mashindano. Kila mtu naamini amechagua eneo lake atakalokuwa anashindana na naamini wale ambao huwa wanashindana na mimi wamejipanga vizuri. Nawatakiwa kila la heri. Kesho nitashiriki michezo mingi zaidi ikiwa ni pamoja na mchezo wa kula, mbona unaniambia *basket?* Mchezo wa kula. Kwa hiyo, nitashiriki huo. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru tena, ahsanteni sana kwa uvumilivu wenu. Naahirisha Shughuli za Bunge mpaka Jumatatu, saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 8.35 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 2 Septemba, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*